# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Mei 1, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579906

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





Burundi inavyohaha kujiunga SADC

Ukurasa 19

Ukurasa 18

Guinea Bisau yachagua wabunge

siasa

JUMATANO MEI 1, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

RIPOTI YA SIPRI: matumizi ya kijeshi yaongezeka duniani

Ukurasa 17

MEI MOSI

‘MAY DAY’; Jadi inayofifia ya mshikamano wa wafanyakazi

Na Anil Kija

MEI MOSI ni siku inayosherehekewa kote duniani kila mwezi wa Mei unapoanza, lakini tofauti na siku zingine maalum zenye itikadi inayoeleweka. ‘May-Day’ kama inavyoitwa kwa lugha inayofahamika zaidi kote duniani ina hisia tofauti, kulingana na mazingira ya nchi.

Ni sikukuu iliyokuwa na nguvu sana miaka ya 1960 hadi 1980 ilipokwisha, na baada ya hapo imepoteza nguvu na mwelekeo karibu kila mahali duniani.

Sababu ni kuwa iliendana sana na kipindi kilichofuata Vita Vikuu vya Pili ambako nchi za Magharibi ziliingia katika dira ya ‘social democracy;’ ambayo kimsingi ilichanganya ubepari na malengo mahsusi ya ustawi wa jamii, wafanyakazi.

Hapa nchini kwa mfano, May Day ilikuwa hasa ni siku ya mashirika ya umma, ambako walikuwa wanaonyesha wanachokifanya katika sikukuu nyingine za kitaifa kama Sababa (iliyogeuka kuwa ya maonyesho ya biashara) na Nanenane (ya wakulima).

MayDay ilikuwa hasa ni siku ya ainisho la kiitikadi la kuenzi siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, iliyoanza kufifia miaka ya awali

INAENDELEA UK.16

Ukurasa 14

Rais Tshisekedi ‘anavyoteseka’ kuunda serikali

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu Jenista Mhagama. **PICHA: MTANDAO**

Viongozi Sudan Kusini bado wajitafuta licha ya ’mguso’ wa Papa Francis Ukurasa 15

## Mvua yakwamisha zaidi ya abiria 1,000

UKURASA 4

UKURASA 13

# JPM: Mwakyembe alinyweshwa sumu

• **Ammiminia** sifa kwa uchapakazi jimboni kwake... *Endelea ukurasa wa 2*



Msongamano wa magari yaliyokwama kwa zaidi ya saa tano katika Barabara Kuu ya Moshi – Arusha, eneo la Kwa Msomali, wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro jana, baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha maji kupita juu ya Daraja la Bijiri. **PICHA: MARY MOSHA**

## Mbunge ahoji Tulia ziara ya Rais

UKURASA 5

## Biashara baa Dar saa 24 kuanza mwezi huu

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA RASMI KUIVAA SEVILLA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM: Mwakyembe alinyweshwa sumu

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amesema Waziri wa Michezo, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alinyweshwa sumu kutokana na kusimamia haki.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana katika mkutano wa hadhara wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya alipokwenda kuzindua Barabara ya Mbeya Mjini - Matema Beach.

Alisema hata kufanikiwa kwa mradi huo kumetokana na jitihada kubwa zinazofanywa na Dk. Mwakyembe. Barabara hiyo imepewa kipaumbele na serikali kwa kujengwa kwa kiwango cha lami licha ya kwamba haiunganishi mikoa wala wilaya.

"Lazima kuna mtu alihangaikia suala hili, Mwakyembe alikuwa Naibu Waziri wangu (Wizara ya Ujenzi), alinisumbua sana, hili nasema wazi, aliwahi kunyweshwa sumu, akapelekwa nje kwa sababu ya kusimamia haki, inawezekana watu wa Kyela hamumjui Mwakyembe," alisema.

Rais Magufuli aliongeza: "Sikuja kumpigia kampeni, lakini nina haki ya kusema ukweli kwa sababu ukweli utabaki kuwa ukweli, ndiyo maana mnaona leo barabara ipo, Sh. bilioni 60 zimelala pale, wana-Kyela ile barabara isiwe ya mapambo."

Oktoba 2011, Dk. Mwakyembe alipelekwa India ili kutibiwa ugonjwa wa ngozi unaojulikana kitaalamu Exfoliative Dermatitis, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na familia ya waziri huyo kipindi hicho.

Alipelekwa huko kwa matibabu zaidi ya ugonjwa huo wa ajabu ulioanza miezi mitatu iliyotangulia. Ilielezwa kipindi hicho kuwa mwili wa waziri huo ulianza kuvimba na ngozi kuharibika.

Viongozi kadhaa akiwamo Waziri wa Ujenzi wakati huo, Dk. Magufuli walikuwepo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam kumsindikiza Dk. Mwakyembe kwenda India kupata matibabu ya kibingwa.

# ...afichua kiini mgogoro wa Tanzania na Malawi

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amefichua kiini cha mgogoro wa kimpaka kati ya Tanzania na Malawi, akieleza kuwa unachochewa na mabeberu.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana akiwa kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika wilaya ya Kyela mkoani Mbeya ambako alizindua barabara ya kutoka Mbeya Mjini-Matema Beach.

Akizungumza kuhusu maeneo yaliyopo wilaya hiyo ambayo ipo karibu na mpaka wa Malawi, Rais Magufuli aliwataka watanzania wafanye biashara na Malawi kwa sababu wao ni ndugu.

"Sisi ni waaafrika ni taifa moja ndio maana katika nchi za Sadc (Nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika) nimeanzia Malawi kwenda kuwasalimu kuwaonyesha kwamba sisi ni ndugu zao," alisema.

Rais Magufuli alisema shida zilizopo Malawi ndizo zilizopo kwa Watanzania na ndio maana amewataka waishi kindugu.

"Sisi Waafrika tunatakiwa kuishi kindugu saa nyingine tunachonganishwa na mabeberu na nyinyi mnakuwa vibeberu vidogo vidogo vya kushindwa kuelekea mwelekeo mzuri wa kujenga uchumi wa nchi," alisema.

Aliongeza: "Nataka niwaambie wana Kyela, Mbeya na Watanzania katika kipindi changu cha uongozi wangu, kamwe Malawi wataendelea kuwa ndugu zetu na marafiki zetu," alisema.

Rais Magufuli alisema ndiyo maana serikali imejenga meli mbili ambazo zimekamilika ambapo ipo ya abiria iliyotumia zaidi ya Sh. bilioni 20.

Alisema wanataka wananchi wasafiri waungane hata wakipata mchumba Zuzu waende wakazuzure naye moja kwa moja.

"Na wao wakija hapa Kyela wakyelemi vizuri mambo yaende sawa sawa sisi ni wamoja tufanye biashara ambazo zilikuwapo tangu enzi za mababu zetu, sisi serikali lazima tuimatishe huo umoja ndio maana tumeanza kujenga Kituo cha Pamoja cha Biashara pale Kasumulo, ambacho itatumiwa na nchi zote mbili," alisema.

Rais Magufuli alisema tayari serikali imeshapata fedha kutoka Benki ya Dunia (WB) na alimtaka Ofisa Mtendaji Mkuu akausaini mkataba huo

INAENDELEA UK.26



HABARI KITAIFA

# Biashara ya baa Dar kwa saa 24 kuanza mwezi huu

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema mpango wa biashara mbalimbali zikiwamo za baa kufanyika kwa saa 24 katika jiji hilo upo katika hatua za mwisho za kukamilika na unatarajiwa kuzinduliwa mwezi ujao na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Makonda aliyaeleza hayo jana, wakati akizungumza na wakuu wa wilaya, makatibu tawala, wakurugenzi na watendaji wa Wilaya zote za jiji hilo, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Makonda alisema taratibu za kufungua biashara kwa saa 24 jijini humo zimekamilika isipokuwa baadhi ya mambo ya usalama ambayo yanakamilishwa na Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

"Kuna mpango wa kuanza kufanya biashara mchana na usiku katika jiji hili, tunachosubiri sasa ni Kamanda Mambosasa akamilishe taratibu na tunatarajia kumualika Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, atuzindulie na tutafanya uzinduzi baada ya kumazika mfungo wa Mwezi Mkutufu wa Ramadhani," alisema Makanda.

**"Kuna mpango wa kuanza kufanya biashara mchana na usiku katika jiji hili, tunachosubiri sasa ni Kamanda Mambosasa akamilishe taratibu na tunatarajia kumualika Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, atuzindulie na tutafanya uzinduzi ...**

Katika mambo ambayo yalikuwa yanafanyiwa kazi na watendaji wa mkoa huo ili kufanya kazi kwa saa 24 ni kuwa na taa maeneo yote ya biashara na kuimarishwa kwa usalama wa maeneo hayo.

Miongoni mwa biashara ambazo Makonda alisema zinapaswa kufanywa kwa saa 24 ni za baa, maduka na usafiri ili kuongeza mzunguko wa fedha na makusanyo.

Sambamba na hilo Makonda aliwahimiza watendaji wa wilaya zote kusimamia ukamilishwaji wa kuwa na maeneo ya vituo vya pikipiki na bajaji ili wafanyabishara hao watambulike na kufanya kazi kwa uhuru.

Makonda pia aliagiza watendaji hao kutengeneza vivuli vya kupumzikia abiria katika vituo vya magari 980 vilivyopo katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo ambavyo vinaweza kutumika kuweka matangazo na kuiingizia serikali mapato.

Aliwasihi watendaji hao pia kuweka utaratibu wa kuwa na maduka yanayotembea katika maeneo yote ya jiji badala ya wafanyabishara kutumia miavuli iliyochakaa na kusababisha kuwa na muonekano mbaya.

# Upepelezi kesi ya kina Dk. Tenga wakamilika

**Na Elizabeth Zaya**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Mawasiliano ya Six Telecoms Limited, akiwamo Wakili Dk. Ringo Tenga, umedai upelelezi wa shauri hilo umeshakamilika na upo kwenye mchakato wa kuwasilisha taarifa muhimu Mahakama Kuu.

Wakili wa Serikali, Batilda Mushi, alidai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, wakati shauri hilo lilipopelekwa kwa kutajwa.

Batilda alidai upelelezi tayari ulishakamilika na wako kwenye mchakato wa kuwasilisha taarifa muhimu, hivyo anaomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya taarifa hiyo, Hakimu Simba aliahirisha shauri hilo hadi Mei 10, mwaka huu na washtakiwa walirudishwa rumande.

Mbali na Dk. Tenga, washtakiwa wengine ni Mhandisi Hafidhi Shamte au Rashidi Shamte ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, mfanyabiashara na Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa fedha wa Kampuni hiyo Noel Chacha na Kampuni ya Six Telecoms.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya utakatishaji fedha.

Katika kesi ya msingi, Dk. Tenga ambaye ni Mkurugenzi na Mwanasheria wa Kampuni hiyo na wenzake wanadaiwa, kati ya Januari mosi, 2014 na Januari 14, 2016, jijini Dar es Salaam, walitoza malipo ya mawasiliano ya simu za kimataifa chini ya kiwango cha Dola za Marekani 0.25 kwa dakika kwa lengo la kujipatia faida.

Pia katika kipindi hicho, wanadaiwa kuhujumu miundombinu ya Mamlaka ya Mawasiliano nchini(TCRA), kwa kutoza gharama chini ya kiwango na kushindwa kulipa kiasi cha Dola za Marekani 3,282,741.12 kwa TCRA, kama malipo ya mapato.

Washtakiwa hao, wanadaiwa katika kipindi hicho walishindwa kulipa ada za udhibiti za Dola za Marekani 466,010.07 kwa TCRA.



# Mbaroni kisa mafuta transfoma

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watuhumiwa tisa kwa tuhuma za wizi wa mafuta ya transfoma na vifaa vingine ambavyo vimekutwa dukani vikiuzwa. Kamanda wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa aliwaambia waandishi wa habari kuwa watuhumiwa hao walikamatwa baada ya Jeshi la Polisi kushirikiana na Shirika la Umeme la Tanesco. "Katika maeneo mbalimbali ya jiji tulifanya operesheni ya kuwasaka wahujumu miundombinu ya Tanesco na tulimkamata mtuhumiwa Shukuru Hamis (39) mkazi wa Tabata akiwa kwenye ghala la shirika hilo lililopo Kigamboni," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema mtuhumiwa huyo alikutwa kwenye ghala hilo akiiba mafuta katika transfoma yenye namba T.26840 aina ya TCO ya mwaka 2007. "Alipohojiwa aliwataja watuhumiwa wenzake ambao ni Mahmoud Ramadhani (39), Witnes Elimasia (35), Japhet Senyagwa (34), Yusuph Salum (38), Shaban Juma (42) na Richard Adamu," alisema. Alisema watuhumiwa hao walieleza kuwa wamekuwa wakiyauza kwa Praygod Kimaro na Seleman Baraka ambapo Jeshi la Polisi lilipofika kwenye stoo ya Praygod na duka la Baraka yaliyopo Tabata Dampo walikamata madumu 68 ya lita 20 ya kampuni mbalimbali za mafuta.

Alitaja kampuni hizo ni Total, CAT, FUCHS, PERFOMAX, CASTROL Oil, BP, MOGAS, LUBEX na pia walikuta maboksi 127 yenye nembo ya kampuni hizo.

"Tulikuta machujio mawili ya mafuta, kitabu chenye oda mbalimbali za wateja na mapipa mawili yenye ujazo wa lita 200 yakiwa na mafuta ya transfoma. Tunaendelea kuwasaka Praygod na Baraka," alisema. Alisema katika operesheni nyingine waliwakamata watuhumiwa wengine wawili wakiwa na vibati maalum vinavyokaa ndani ya transfoma vinavyosaidia kuzalisha umeme na mashine tano za kuchomea zilizotengenezwa kienyeji.




Wachuuzi wa bidhaa wakifanya shughuli zao chini ya transfoma ya umeme mkubwa, kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari endapo itatokea hitilafu ya umeme. **PICHA: JOHN BADI**

# Mvua yakwamisha zaidi ya abiria 1000

**Na Waandishi Wetu**

ABIRIA zaidi ya 1000 waliokuwa wakienda mikoa mbalimbali kupitia barabara ya Moshi, Arusha, wamekwama zaidi ya saa tano baada ya mvua kubwa iliyonyesha kwa saa saba mfululizo na kusababisha maji kupita juu ya daraja Bijiri, maeneo ya kwa Msomali, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro.

Aidha, mkoani Arusha mvua kubwa imeharibu miundombinu ya barabara.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya abiria, Samson Mwakatobe alisema, mvua hizo zilizonyesha kwanzia saa sita usiku zimesababisha maji mengi yaliyopita juu ya daraja na kusababisha kukwama kwa mawasiliano wa takribani saa tano.

Msafara huo wa magari unaodaiwa kuanzia eneo Mailisita, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro hadi Kingori wilayani Arumeru, mkoani Arusha.

"Tangu saa 12 asubuhi tuko hapa katika eneo la Kwa wasomali tumeshindwa kupita kutokana na daraja kujaa maji yakitokea maeneo ya mlimani," alisema Faustine Moleli

Baadhi ya madereva Elikizanda Msuya, walielezea kilio chao na kusema kuwa japo kuna mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea na mvua za masika hazitabiriki, lakini eneo hilo limekuwa korofi na upo umuhimu wa serikali kulifuatilia kwa umakini.

"Daraja hilo ni dogo, maji yanapokuwa mengi yanashindwa kuhimili wingi wa maji na hivyo kusababisha mafuriko kila mwaka," alisema Hasani Mwaka.

John Bunda, alisema ipo haja ya serikali kutipia Wakala wa Barabara (Tanroads), kuangalia uwezekano wa kupanua daraja lile na kudhibiti mkondo wa maji kutokana na mara kwa mara magari kukwama mvua inaponyesha na kusababisha adha kwa wananchi.

"Ifike mahali serikali ione mateso wanayopata watumiaji wa barabara hiyo na kuongeza jitihada... wapo wageni wameshindwa kuondoka na ndege, watu wamechelewa maeneo ya kazi hali inayosababisha kushuka kwa uchumi wa taifa," alisema.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya abiria waliokuwa wakisubiria magari hayo huku wakilalamikia kucheleweshwa kwenye safari zao na kuiomba serikali kuchukulia hatua za upanuzi wa daraja hilo.

Aidha Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alikiri kuwapo kwa mafuriko yao na kusema tayari wamechukua jitiada za kuhakikisha magari yote yanaendelea na safari zake za kila siku.

Meneja wa Tanroads Mkoa wa Kilimanjaro, Ntije Nkolanta, amesema hatua za haraka zimeshachukuliwa katika kuhakikisha watumiaji wa barabara hiyo wanaendelea na safari zao.

"Ni kweli mafuriko hutokea hapa mara kwa mara na baadhi ya abiria wamekuwa wakipata adha ya usafiri mara kwa mara, lakini serikali kwa kuliona hilo tayari tuliweka kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 ili tuweze kupanua njia za kupitisha maji," alisema.

"Mvua hizi zimesababisha madhara makubwa kwa miundombinu katika mkoa wa Kilimanjaro na hata wenzetu wa Arusha hivyo tuwaombe radhi wasafiri wote waliokubwa na adha hii na serikali ipo bega kwa bega kuhakikisha inatatua changamoto hii," alisema.

YAKATA BARABARA ARUSHA

Mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Arusha kuanzia usiku wa kuamkia

INAENDELEA UK. 8

# Majaliwa aagiza taasisi zipitiwe upya kuepusha mkanganyiko

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa, amemwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu), Jenista Mhagama, akutane na mawaziri wa sekta nyingine na watafute namna ya kuondoa mkanganyiko uliopo kwenye vyombo vya udhibiti hapa nchini.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo juzi Bungeni jijini Dodoma, kwenye mkutano wa 15 wakati akihitimisha hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2019/2020.

Alikuwa akitoa ufafanuzi kuhusu masuala yaliyogusa vyombo vya udhibiti kama vile Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mkemia Mkuu wa Serikali, mamlaka nyingine za udhibiti pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), OSHA, BRELLA na Taasisi ya Mionzi ambayo yaligusiwa na wabunge.

Alisema licha ya serikali kujenga mazingira wezeshi na rahisi ya kufanya biashara na uwekezaji, bado kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara na wawekezaji kama walivyoeleza wabunge wakati wa kuchangia hoja hiyo.

"Changamoto nyingine ambayo imeonekana kuwa kikwazo cha biashara na uwekezaji ni mwingiliano wa majukumu ya taasisi hizo. Kwa mfano, uwapo wa majukumu yenye kufanana kwa TFDA, TBS, Mkemia Mkuu wa Serikali, Bodi ya Maziwa, Bodi ya Nyama, Baraza la Mifugo, Ewura, Sumatra na Tanroads ni kikwazo kikubwa katika kurahisisha mazingira ya kufanya biashara," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu mamlaka hizi na namna ya utendaji kazi wake. Miongoni mwa kero hizo ni mchakato wa muda mrefu wa kupata leseni za biashara; gharama za usajili wa bidhaa zinazotozwa na TFDA; suala la viwango vya TBS; madai ya kuwapo kwa unyanyasaji unaofanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kushirikiana na polisi dhidi ya wafanyabiashara.

Pia walibainisha changamoto nyingine kuwa ni umbali wa kutoka makao makuu na maabara za taasisi ya mionzi hadi eneo wanalofanyia kazi kama vile bandari na viwanja vya ndege.

"Tayari nimeshatoa maelekezo na yameanza kufanyiwa kazi na mawaziri wa sekta husika chini ya uratibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera na Uratibu) kwamba wakae pamoja kupitia sheria na mgawanyo wa majukumu wa taasisi za udhibiti ili kuondoa mkanganyiko uliopo sasa," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mfanyakazi wa kampuni ya Vodacom Tanzania, Neema Mgombelo, akionyesha mfano wa jinsi ya kumtambua mgonjwa aliezimia, katika semina ya mafunzo ya huduma ya kwanza, iliyofanyika makao makuu ya kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwalimu wa mafunzo hayo, Adam kutoka kampuni ya Knight Support. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge ahoji Naibu Spika ziara za viongozi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE hasa wapinzani wanaohoji ni kwa nini Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, muda mwingi anazunguka kwenye ziara za viongozi wa kitaifa na kuaacha shughuli za Bunge, wana tatizo la 'Post Traumatic Stress Disorder (PTSD)'

Tatizo hilo linalowasumbua baadhi ya Wabunge kuhusu kutoonekana Bungeni kwa siku kadhaa kwa Dk. Tulia, lilielezwa jana na Mwenyekiti wa Bunge, Mussa Azan 'Zungu' wakati akijibu muongozo ulioombwa na Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Mch. Peter Msigwa.

Msigwa aliomba muongozo huo akisema, Mheshimiwa Mwenyekiti (Zungu), ninaomba muongozo kwa Kanuni ya 68 (7) kwa mujibu wa Katiba yetu, nchi yetu ni Republic, sio Monarch ina mihimili mitatu yaani Executive (utawala), Judiciary (Mahakama) na Parliament (Bunge).

Lakini hivi karibuni Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu limekuwa na viongozi yaani Spika na Naibu Spika.

"Lakini kwa hivi karibuni Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya muhimili wa Bunge amekuwa akiambatana na Executive muda wote (viongozi wa juu wa serikali) katika ziara za Executive, jambo analolifanya ni sawa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia angekuwa anakaa hapa gallery (jukwaa la Bunge) anaangalia shughuli za Bunge zinavyoendelea anaacha shughuli za executive (utawala)."

Mch. Msigwa alisema, au sawa Makamu wa Rais angekuwa anakwenda kwenye Kamati za Bunge anaangalia shughuli za Executive. Sasa ninachopenda kujua, ningeomba muongozo wako kwa sababu tuna

**INAENDELEA UK. 8**

# Mbatia awaombea walimu nyongeza mishahara kwa JPM

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAKATI Bunge likiwa limepitisha jana bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mbunge wa Vunjo (NCCR Mageuzi), James Mbatia, amemwomba Rais John Magufuli leo kutangaza kuongeza mishahara ya walimu na stahiki zao kwa upendeleo wa makusudi, kwa kuwa walimu ndio sekta kuu ya uzalishaji katika taifa.

Mbatia alikuwa akichangia mjadala wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20 ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

"Kwani sote sisi humu ndani ni zao la walimu, Rais wetu Mwalimu John Joseph Pombe Magufuli, rai yangu kwake awe mstari wa mbele kesho (leo) Mei mosi awe wa kwanza kuongeza mishahara ya walimu na stahiki zao kwa upendeleo wa makusudi, kwa kuwa walimu ndio sekta kuu ya uzalishaji katika taifa letu," alisema.

Alisema ili kukuza na kuhifadhi utu wao utakaowawezesha kuwa na furaha ya ndani na wawe na uwezo na utu wa kufundisha ili tutoke tulipo ni lazima kuondoa itikadi zao na tofauti zao na kujikita kwenye kuiangalia Tanzania kwa miaka 30 au miaka 50 ijayo.

Mbatia ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha NCCR-Mageuzi amelieleza Bunge kuwa ameanza na jambo hilo kwa sababu anaiangalia elimu ya Tanzania

**INAENDELEA UK. 8**

# Precision yaongeza safari

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kukuza sekta ya utalii nchini, Shirika la Ndege la Tanzania la Precision Air, limeimarisha zaidi safari zake mkoani Kilimanjaro baada ya kuanzishwa kwa kituo chake kidogo mkoani humo.

Hatua hiyo ni sehemu ya shirika hilo kuendeleza kupanua mtandao wake wa mawasiliano katika mikoa ya kaskazini kwa kuanzisha safari zake kutoka Kilimanjaro saa 12 asubuhi kuelekea Dar es Salaam na kutoka Dar es Salaam saa tatu usiku kuelekea Kilimanjaro.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Shirika hilo jana ilisema safari hizo, zinaifanya Precision Air kuwa na safari nyingi zaidi mkoani Kilimanjaro kwa kuruka mara sita kwa siku kuelekea na kutoka Kilimanjaro.

Akizungumzia mpango huo, Meneja Masoko wa Precision Air, Hillary Mremi, alisema wasafiri wanaweza kuunganisha safari zao kadhaa kutoka Kilimanjaro kwenda Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Dodoma, Entebbe, Nairobi na zaidi. "Wasafiri wa kudumu na wapya sasa wanaweza kwenda na wakati katika shughuli zao za kiofisi, kibiashara, au hata za matukio muhimu."

"Daima Precision Air ipo kuhakikisha kuwa Tanzania inaunganishwa ipasavyo ili kurahisisha shughuli zinazochangia uchumi wa nchi kukua. Pia, tunatambua jitihada zinazofanywa na Rais Dk. John Magufuli katika kukuza uchumi wa nchi na kama wadau wa maendeleo, tunamuunga mkono kwa kuendeleza sekta ya usafiri kwa kutoa huduma za usafiri za uhakika," alingeza.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyakazi waboreshewe mazingira ya kufanyia kazi

**WATANZANIA** leo wanaungana na wenzao duniani kuadhimisha siku ya Wafanyakazi Duniani maarufu kama Mei Mosi.

Kimsingi Mei Mosi ni siku ambayo wafanyakazi huitumia kwa ajili ya kutathmini kazi wanazofanya pamoja na kudai mazingira bora zaidi ya kufanyia kazi.

Ni wakati ambao wafanyakazi huelezea changamoto wanazokutana nazo wakati wakitekeleza majukumu yao waliyopangiwa na waajiri. Kwa kawaida wafanyakazi hudai nyongeza ya mishahara na haki nyingine ambazo wanastahili kuzipata.

Kwa upande mwingine, waajiri nao huitumia fursa hiyo kuwazawadia wafanyakazi ambao kwa namna moja au nyingine wametekeleza vizuri majukumu yao, hivyo kuwazawadia ikiwa ni kuthamini mchango wao.

Tumaanini kuwa hata leo wafanyakazi wa Tanzania wataitumia nafasi hiyo kueleza changamoto wanazokumbana nazo ili waajiri wao na serikali kwa ujumla kuzipatia ufumbuzi.

Kwa upande wake, Serikali inabeba jukumu kubwa katika kushughulikia changamoto za wafanyakazi wote bila kujali kama ni wa sekta ya umma au sekta binafsi.

Tinasema hivyo kwa kuwa serikali inaweza kutengeneza mazingira mazuri kwa wafanyakazi wote kwa mfano, kushusha baadhi ya kodi ambazo zinawagusa moja kwa moja wafanyakazi wote ikiwamo ya mshahara.

Baadhi ya watumishi wa umma hususan walimu wamekuwa wakiidai serikali malimbikizo ya stahiki zao mbalimbali, huku serikali ikiwaahidi kuwalipa. Wako pia baadhi ya watumishi ambao walikuwa wanasubiri kupandishwa madaraja kwa muda mrefu pamoja na nyongeza ya mshahara.

Hata hivyo, serikali imeshaahidi kuwa itawalipa na Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora) hivi karibuni wakati wa kuwasilisha hotuba ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha 2019/20 ilieleza kuwa watumishi kadhaa watapandishwa vyeo.

Tunatarajia kuwa leo changamoto zaidi zinazowakabili watumishi wa umma na wa sekta binafsi zitaelezwa mbele ya viongozi wa kitaifa katika maadhimisho ya Mei Mosi ambayo kitaifa mwaka huu yanafanyika mkoani Mbeya.

Hata hivyo, pamoja na wafanyakazi wa Tanzania kutaka waboreshewe zaidi mazingira ya kazi, tunaona kuwa kuna haja nao kuzidisha juhudi zaidi katika kuchapa kazi.

Umuhimu huo unatokana na kupanda kwa hali ya maisha katika nchi nyingi zikiwamo za jirani, ambazo tumekuwa tunawasikia wafanyakazi wakilalamika pamoja na kugoma kutokana na mazingira yasiyoridhisha ya kazi.

Hatukatai wafanyakazi kutodai haki zao za msingi, lakini wazidai, huku nao wakitimiza wajibu wao wa kufanyakazi kwa juhudi, bidii, weledi, uaminifu na uadilifu.


Hakuna mwajiri anayeweza kuwa na mfanyakazi ambaye hatoi mchango katika kuleta tija na ufaniki kwa taasisi iliyomwajiri. Kwa maneno mengine, wafanyakazi wadai haki zao kwa waajiri, lakini nao wawajibike kwa kufanyakazi kwa tija na ufanisi.

Tunawatakia kila la kheri wafanyakazi wote nchini katika maadhimisho ya siku ya leo, huku tukiwakumbusha waajiri wajibu wao wa kuwapa wafanyakazi wao haki zao za msingi ili waweze kutimiza wajibu wao inavyostahili.

Tunaamini waajiri, ikiwamo serikali watasikia kilio cha wafanyakazi na wawe tayari kufanyia kazi changamoto hizo ili nchi yetu isonge mbele katika safari ya kuelekea kwenye uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Jamii iwarekebishe wanafunzi wanaovaa mtindo wa mlegezo

**MTINDO** wa uvaaji wa suruali katikati ya makalio ambao ni maarufu kama 'kata k,' unazidi kujipatia umaarufu miongoni mwa vijana wakiwamo hata wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Baadhi ya vijana wanaopenda mtindo huo huwa wanavaa suruali au kaptula na kuzishusha ili nguo zao za ndani zikiwamo 'boksa' zionekane nje na kutembea bila wasiwasi kana kwamba wamevaa vizuri.

Imekuwa kama jambo la kawaida kukuta mwanafunzi amevaa sare ya shule hasa suruali inayobana na ikiwa imeshuka chini ya makalio huku akining'iniza kitambaa katika mfuko wa nyuma.

Sidhani kwamba kuna shule yenye utaratibu wa aina hiyo kama si wanafunzi wenyewe tu kulazimisha uvaaji wa aina hiyo ambao hauendani na utamaduni wa asili ya Mtanzania.

Hii yote inatokana na utandawazi uliokuja kupoteza wale wanaoupokea bila kuchuja mambo kwa kuiga na matokeo yake ni kulazimisha kufanya yale yasiyostahili.

Muungwana anaamini kwamba utandawazi ni kiunganishi kikubwa cha maisha ya kisasa kinachobadilisha baadhi ya vijana na kujikuta wakifanya mambo ya ajabu kama hayo ya kuvaa ovyo.

Wanafunzi wanaofanya hayo ni vyema wakatambua kuwa utandawazi umeifanya dunia kuwa kijiji, lakini kwa gharama za kuupoteza utambulisho wa tamaduni asilia kwa upande mwingine, hivyo jambo kama hilo la 'kata k' halifai kabisa.

Kwa ujumla vijana katika nchi maskini wanakuwa ni waathirika wakubwa wa utandawazi bila kujua au kwa kujua, kwani hujikuta wakionekana kituko mbele ya jamii kwa uvaaji huo.

Hebu fikiria kwamba mzazi amemnunulia mtoto wake sare ya shule ikiwa inamtosha vizuri, lakini yeye anaichukua na kuipeleka kwa fundi kupunguza upana na hata urefu ili iwe kama anavyotaka.

Ninaamini kwamba wazazi na walimu wanaliona hilo na kama hawalioni, basi washtuke na kuchukua hatua dhidi ya wanafunzi wa aina hii ili wasipotoshe wenzao kwa mavazi ya ovyo.

Kuenea kwa tehama (teknolojia ya habari na mawasiliano) kusiachwe kuendelee kuathiri malezi bora ya watoto wetu, bali ni vyema kujua kwamba televisheni, redio, simu za mkononi, kompyuta na intaneti vina umuhimu wake iwapo vitatumiwa vizuri.

Hata hivyo, visiachwe kuwa mlezi wa watoto, kwani mwisho wa siku vitawaharibu, kutokana na ukweli kwamba hawajui ni lipi la kuchukua na lipi la kuacha, hivyo ni muhimu kuchukua kitu wanachokiona kina manufaa na kukifanyia kazi.

Kwa maana hiyo uangalizi kwa watoto ni suala la muhimu sana ili wasiige vitu vya ovyo kwenye vyombo vya mawasiliano au kutazama wawapo nyumbani ama kwa marafiki zao.

Hilo likifanyika na kusimamiwa vizuri, uvaaji huo wa suruali kwa mtindo wa mlegezo ambao kimsingi ni ulimbukeni kwa vijana wa kupenda kuiga kila wanachokiona kutoka kwa wazungu, utakoma.

Nikisema kwamba kulegeza suruali ni ukiukaji wa mfumo wa uvaaji nitakuwa sijakosea, kwani katika jamii ya Kitanzania hakuna mtindo wa kuvaa nguo chini ya makalio kama siyo kuiga tu.

Ingependeza iwapo wanafunzi wanaopenda mtindo huo kama wangeelekeza nguvu zao kwa ajili ya kusoma kwa bidii ili wafike mbali kielimu badala ya kupoteza muda kwa vitu visivyo na manufaa kwa maisha yao ya baadaye.

Mwanafunzi ambaye yuko makini kwenye elimu hawezi kupoteza muda wake kupeleka sare kwa fundi zipunguzwe ili ziwe nyembamba eti kwa sababu ya kwenda na wakati.

Kabla ya kufanya hivyo ni vyema wakajiuliza kwamba huo wakati unawapeleka wapi, kuliko kuvamia mambo tu na kujikuta wakienda kinyume na maadili au mila na desturi za Kitanzania.

Inasikitisha kuona wanafunzi wakiiga uvaaji wa baadhi ya makondakta wa daladala na wahuni mitaani, ambao kwao mlegezo na kuning'iniza kitambaa katika mfuko wa suruali na kaptula ni jambo la kawaida.

## BARUA/MJADALA

### *Dawasa Boko turejesheeni maji wakazi wa Mafuriko Zahanati*

**Mhariri**

*NINAELEZA utendaji usioridhisha wa baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) katika ofisi yao iliyoko Boko au Basihaya kama inavyojulikana kwa wengine jijini Dar es Salaam.*

*Pamoja na kuhudumia maeneo mengine, ofisi hii inahudumia pia wananchi wa maeneo ya Tegeta, Wazo Hill, Kisanga na kitongoji cha Mafuriko.*

*Kwa muda wa siku sita sasa, baadhi ya wakazi wa eneo la Mafuriko jirani na Zahanati ya serikali ya Mafuriko au Kisanga kwa jina jingine, wamekosa huduma ya maji ambayo wanaipata kupitia tanki kubwa la Dawasa lililoko eneo hilo, jirani na Kanisa Katoliki Parokia ya Wazo.*

*Baada ya kufuatilia kwa nini wanakosa maji, wakazi hao waligundua hujuma ya kukatwa kwa kipande cha bomba chenye urefu wa mita tatu wakatoa taarifa mara moja kwa wafanyakazi wa Dawasa walioko katika tenki hilo, wakiomba hatua za kurekebisha dosari hiyo zichukuliwe.*

*Sasa walichofanya wafanyakazi hao ni kufunga maji ili yasiendelee kumwagika kitu ambacho ni cha msingi. Hata hivyo, wananchi walitarajia kwamba baada ya kufunga bomba ili lisiendelee kumwaga maji, basi matengenezo yangefanyika mara moja ili kurejesha huduma ya maji kwa wananchi walioikosa.*

*Kumbe walikuwa wanajidanganya kwani Dawasa mpaka sasa hawajafanyia matengenezo ya kipande cha mita tatu kilichokatwa.*

*Aidha, wafanyakazi wa tenki hilo wametoa sharti kwa wananchi kwamba wakae na kukubaliana namna gani watakuwa wanapata maji kwanza, ndipo Dawasa warejeshe huduma hiyo.*

*Kinachosikitisha zaidi ni kwamba taarifa hii imetolewa katika ofisi ya Dawasa ya Boko kwa maelezo ya kina, lakini mpaka barua hii inatoka wananchi hao hawana maji.*

*Ninachojiuliza mimi ni kwamba moja ya mambo yanayohimizwa na serikali ya Dk. John Magufuli ni watumishi katika ofisi za umma kuhudumia wananchi kwa ukamilifu, sasa inakuwaje bado kuna baadhi ya watumishi wasioelewa muelekeo wa serikali hii? Kupitia barua hii naomba Dawasa Boko warejeshe huduma ya maji kwa wananchi wa eneo hili waliyoyakosa kwa muda wa siku sita leo.*

**Muathirika-Wazo**
**Mafuriko, DSM**


**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**


# Jamii iungane na watetezi kupinga adhabu zisizojenga kwa wanafunzi



**Na Mwandishi Wetu**

**MOJA** ya matukio ambayo jamii imeendelea kushuhudia ni ukatili dhidi ya watoto katika mikoa mbalimbali nchini na hata wakati mwingine kuuawa kama vile hawana haki ya kuishi.

Mwaka 2018 na hata huu unaoendelea kumekuwapo na matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto ikiwamo ile ya adhabu wanazopewa wanafunzi shuleni na walimu wao, hali inayowasababishia baadhi yao madhara makubwa.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya wabunge kuanza kuhoji ili kujua kauli ya serikali juu ya walimu wanaokiuka sheria za adhabu kwa wanafunzi kwa kuwachapa hadi kuwaumiza.

Serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, William Ole Nasha imepiga marufuku walimu kutoa adhabu ya viboko kwa mwanafunzi bila kibali cha mwalimu mkuu wala kutembea na kiboko shuleni.

Licha ya serikali kupiga marufuku adhabu hizo shuleni, bado hakuna miongozo yoyote iliyotolewa na serikali juu ya usimamizi wa nidhamu shuleni na watoto wanaendelea kupigwa na kuumizwa.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya watetezi wa haki za watoto wanajiuliza kuwa hata sehemu ambayo ingepaswa kuwa salama kabisa ndipo ambapo watoto wanapoteza maisha kwasababu ya vipigo kutoka kwa walimu?

Watetezi hao walio chini ya mradi wa Data Driven Advocacy (DDA) kwa uratibu wa mashirika ya Women in Law and Development in Africa (WiLDAF) ni pamoja na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA).

Wengine ni Tanzania Child Rights Forum (TCRF), Tanzania Domestic Workers Coalition (TDWC), Mwanza Youth and Children Network(MYCN),Tanzania Early Childhood Development Network (TECDEN) na Zanzibar Women Lawyers Association (ZAFELA) kwa kuwataja baadhi.

Wanaamini kwamba shule ni mazingira salama kwa watoto, ambayo yanawafanya kujisikia huru na salama katika kufikia malengo yao ya elimu.

Kwamba elimu ni haki ya msingi ya mtoto yeyote ila pia ni lazima kuwe na mazingira salama kwa ajili yake na yasiwe kikwazo kufikia malengo ya haki ya elimu kwa mtoto.

Lakini wanashangaa kuona watoto wakikumbana na adhabu za vipigo, ukatili wa kingono na hata udhalilishwaji wakiwa shuleni, hali ambayo inaonyesha kuwa mazingira ya baadhi ya shule si salama kwa watoto.

Aidha, wanasema adhabu za viboko shuleni kwa tafiti nyingi zinaonyesha ni kwasababu ya msongo wa mawazo wa walimu na pia kukosa mbinu mbadala za kusimamia nidhamu kwa wanafunzi, wakiamini kuwa adhabu kali za viboko ndio njia pekee inayoweza kusimamia nidhamu ya shule.

Mjadala unaona kwamba kinachosemwa na watetezi hao ni sahihi kwani kinalenga kujenga mazingira salama ya shule kwa watoto ambayo yatamfanya mtoto kujisikia huru na salama katika kufikia malengo yake ya elimu bila kukatishwa tamaa.

Cha msingi ni kufuata sheria inayosimamia masuala ya elimu Tanzania hasa Sheria ya Taifa ya Elimu (National Educations Act, 1978) kwani ndani ya kifungu cha 60 (I) (O) kinampa waziri mwenye dhamana kutengeneza kanuni zitakazoratibu na kusimamia utoaji wa adhabu za viboko shuleni.

Kimsingi kanuni za uratibu na usimamizi wa utoaji wa adhabu shuleni (The National Education (Corporal Punishment) Regulations, 1979, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2000 kupunguza idadi ya viboko toka sita hadi vinne, inafafanua jinsi ya kutoa adhabu hiyo.

Lakini pia bado kuna changamoto kwenye jamii ya kutofuatilia na kukemea adhabu mbaya, kwani utafiti uliowahi kufanywa na HakiElimu kwa kuuliza swali "Shule Salama ni nini"? Umetoa majibu.

Takriban watu 6,000 walishiriki wengi wao waliongelea shule salama kama ni madarasa mazuri, mpangilio, usafi, walimu, vitabu na vyoo. Wachache sana waliongelea mazingira ambayo walimu hawapigi.

Hii inaonyesha taswira ya jinsi gani hata jamii iko nyuma juu ya athari za adhabu zilizopitiliza shuleni, hivyo inahitaji kupewa elimu zaidi ili kutambua na kukemea adhabu za kikatili kwa watoto.

Jamii inapaswa kutambua kuwa kulingana na kanuni za adhabu ya viboko shuleni, ni adhabu inayotolewa kwa kuchapa mwanafunzi fimbo mkononi au matakoni ikiwa ni kwa ajili ya kumrekebisha si kumkomoa.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



# Mbunge ahoji Naibu Spika ziara za viongozi

INATOKA UK. 5

mihimili mitatu na inajitegemea na inafanya kazi, hili Bunge mara nyingi tumekuwa tukiambiwa Bunge dhaifu huko nje. Ni kwa nini Naibu Spika ambaye aliapa.

"Ni kwanini Naibu Spika, muda mwingi anazunguka kwenye ziara za executive akiacha shughuli za Bunge?" aliuliza Mbunge huyo.

Baada ya kumaliza kuomba muongozo huo, Mwenyekiti wa Bunge hilo, Mussa Azan alijibu muongozo ulioombwa na Msigwa akisema:

"Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Msigwa, kwanza hili jambo halijatokea leo mapema Bungeni, pili Naibu Spika ni mteule wa Rais na taarifa zake, nakujibu nikuelimishe tu,sina sababu ya kukujibu. Taarifa zake za kuwapo, kutokuwapo Bungeni anayezijua ni Spika (Job Ndugai) ambaye ni muhimili wa Bunge hili, sio wewe wala mimi."

Mwenyekiti huyo alifafanua zaidi: "Na kwa vile ni mteule wa Rais, muda wowote anaweza kuwa summoned na mamlaka ya juu (akapata wito) kwenda kufanya kazi kutoka mamlaka iliyomteua, lakini vile vile, sikusemi wewe, wala usininukuu kana kwamba nakuambia wewe:

"Kuna maradhi yanaitwa Post Traumatic Stress Disorder (tatizo la kiakili linalosababisha mawazo, baada ya kiwewe)...sisemi wewe unayo," alieleza Mwenyekiti wa Bunge, Zungu (pichani).



# Mvua yakwamisha zaidi ya abiria 1000

INATOKA UK. 4

jana, imesababisha madhara makubwa ikiwamo kuharibu miundombinu ya barabara na baadhi ya nyumba kujaa maji.

Maeneo yaliyoharibiwa na mvua hiyo, ni barabara kuu ya Arusha- Moshi, Arusha –Namanga na barabara za katika ya Jiji la Arusha .

Kunyesha kwa mvua hiyo, kumesababisha maji kujaa barabarani, tukio hilo lilisababisha magari kuzuiwa kupita katika barabara hizo kwa muda.

Kadhalika, mvua hiyo imesababisha baadhi ya wakazi wa Kata za Ungali mtd, Sokoni One, Kimandolu, Engutoto na Kiranyi kuhama makazi yao kwa muda kutokana na nyumba zao kujaa maji na kuvunjika.

Akizungumza na Nipashe Kaimu wa Tanroads, Mkoa wa Arusha, Mhandisi John Kalupale, alisema mvua hiyo imesababisha madhara makubwa ya uharibifu wa miundombinu.

"Barabara ya Arusha kwenda Moshi eneo la King'ori imevunjika na magari madogo yalizuiliwa kwa muda, lakini barabara zilizoharibika utaratibu wa kuzikarabati umeshaanza," alisema Kalipale.

Kalupale alisema maofisa wa Tanroads Mkoa wa Arusha wameanza kutembelea na kukagua barabara zote zilizoathirika ili kutambua ukubwa wa tatizo.

"Tutatembelea barabara zote kuangalia ukubwa wa madhara yaliyosababishwa na mvua hii na baada ya hapo tutatoa taarifa kamili," aliongeza Kalupale.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, pamoja na kikosi cha Zimamoto na Uokoaji walifanya ziara ya kukagua maeneo yaliyoathiriwa na mvua hiyo.

**Imeandikwa na Na Mary Mosha (Hai) na Allan Isack (Arusha)**


COPS AUCTIONMART & COURT BROKERS LTD.

**NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na CRDB BANK PLC, tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini. Mnada wa utafanyika mahali dhamana ilipo baada ya siku 14 kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi/Tangazo hili. .

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Hussein Omary Hussein | Kiwanja Na. 248, Block 'GG', yenye CT Na. 24408- DLR, LO Na. 439075, Kiwanja kipo eneo la Turute, **KONDOA MJINI** | 15/05/2019 | Saa 3:00 Asubuhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA:-**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo (as is where is basis)
2. Mteja anatakiwa kulipia **asilimia 25%** siku ya mnada na **asilimia 75%** iliyobaki amalizie ndani ya siku 14.
3. Endapo mteja atashindwa kumalizia **asilimia 75%** ya kiasi kilicho salia ndani ya **siku 14,** hatarudishiwa kiasi cha fedha alicholipa mwanzo na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zote za kubadili **HATI MILIKI** ni **JUU YA MNUNUZI**
5. Kwa yeyote atakaye haribu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**COPS AUCTION MART & COURT BROKERSLTD**
**S.L.P. 12508**
**DAR ES SALAAM.**
**Mob: 0716 884 999/ 0753 885 050/ 0788 899 099**
**www.copsauctionmart.com**

**Au:**

**CRDB BANK PLC**
**S.L.P 268**
**DAR ES SALAAM**
**Simu: +255 (0)22 211 7441-7**
**http/www.crdbbank.com**

215207402



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA / 04)**

**Mahakama ya Mwanzo ya MANZESE /SINZA**
**Wilaya ya KINONDONI**

**MADAI NAMBARI 332/2018**

**Mimi ANGAZA GIMBI**

**Namdai**

**Mdaiwa ESTHER KROLL**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba

**UNAAMRIWA NA MAHAKAMA KUFIKA BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hiyo MANZESE/SINZA tarehe 20/5/2019 saa 8:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 30/04/2019


# Mbatia awaombea walimu nyongeza mishahara kwa JPM

INATOKA UK. 5

kwa miaka 30 hadi 50 ijayo.

Alisema ukisoma hotuba ya Kambi ya upinzani yote kwa makini utaona ifikapo mwaka 2036, tutakuwa na Watanzania zaidi ya milioni 90, mwaka 2045 tutakuwa na Watanzania zaidi ya milioni 120.

Akiijenga hoja yake hiyo, Mbatia laisema: "Je critical mass ya Watanzania, critical thinkers ya Watanzania watakuwa kwenye hali gani kama hatuondoi itikadi zetu, kama hatuondoi tofauti zetu, tukajikita kwenye kuiangalia Tanzania miaka 30 au miaka 50 ijayo."

Aliongeza, "Elimu bora sawa, shirikishi kwa wote, mfumo wetu rasmi wa elimu wa sasa, kwa mfano Sera ya elimu ya mwaka 2014, elimu ya msingi ukiangalia na mitaala yake, mitaala ya darasa la saba tayari imeshafundishwa, darasa la nne la tano na la sita, ukiangalia Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, kwa nini hatukubali kuwa na mfumo ambao ni shirikishi, ni sawa na ni elekezi kwa wote, badala ya kila Waziri anayekuja na mfumo wake na matamko yake ambayo tuharibu elimu ya taifa la Tanzania."

Alisema ni lazima tuiangalie Tanzania zaidi ya miaka 50 ijayo na kwamba

ni bahati mbaya sana tunazungumzia tu formal education (mfumo ulio rasmi), lakini non formal (mfumo usio rasmi) and informal education tunaiweka kwenye hali ya namna gani.

"We must think big and think globally (lazima tufikiri kwa kuangalia mbali zaidi), namna gani tuna wa 'nature' tunawakuza watoto wetu, namna gani tunawapa walimu wetu ambao ni walezi wakuu wa taifa letu, waweze kuliangalia taifa, waweze kuwa na utulivu, waweze kulea watoto wetu kwa sababu kama mama wewe unamtoa mtoto wako unamkabidhi mwalimu, una mwamini zaidi kuliko hata mfanyakazi wa ndani,"alieleza Mbatia

Alimtaka Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, kuangalia namna anavyoweza kuacha alama katika uongozi wake.

"Joyce Ndalichako, dada yangu ulikuwa kwenye Taasisi ya Elimu, ulikuwa Baraza la Mitihani la Taifa (Necta), umetoka huko umepewa dhamana hiyo, unaacha legacy (alama) ya namna gani kwa taifa la Tanzania kwamba umeanzisha mfumo huu kwamba unaiona Tanzania ya miaka 50, kwamba unaiona Tanzania ya miaka 30 yenye uelewa wa hali ya juu. Kila siku tunapiga kelele hili limetokea hivi, hili limetoea hivi, tumekuwa negative negative, let us think positive, think globally, think big na tuione Tanzania ya miaka 50 ijayo,"alieleza

HABARI KITAIFA

# Wajijengea zahanati baada ya miaka 20

**Na Elizabeth Zaya,** NJOMBE

WANANCHI wa kijiji cha Mafinga kilichopo katika Kata ya Kipengele katika Halmashauri ya Wanging'ombe mkoani Njombe wameushukuru Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kuwajengea Zahanati.

Wananchi hao walisema tangu kuanzishwa kwa kijiji hicho zaidi ya miaka 20 iliyopita hakujawahi kuwapo na kituo cha afya kijijini hapo.

Mkazi wa kijiji hicho, Rafikinjema Mgaya, alisema tangu aolewe kijijini hapo zaidi ya miaka 20 iliyopita wamekuwa wakipata shida ya huduma ya afya kutokana na kukosekana kwa kituo cha afya na badala yake wamekuwa wakilazimika kusafiri zaidi ya kilomita 40 kwenda katika kijiji kingine kufuata huduma hiyo.

Alisema baadhi ya wajawazito wamekuwa wakijifungulia njiani wakati wakienda kufuata huduma ya afya katika kijiji kikinge.

"Mimi mwenyewe nina mtoto wa kidato cha nne Sasa hivi ambaye nilijifungulia njiani wakati nakwenda katika kijiji kingine kwa ajili ya kujifungua. Siku hiyo nilikuwa mimi na mume wangu tu, huwa tunaambiwa kwamba kabla ya siku za kujifungua kufika tuwe tumeenda hospitali," alisema Mgaya na kuongeza:

"Lakini kwa sababu ya gharama kubwa inatubidi tujipange kuhakikisha tunapata pesa ya kutosha, na ndivyo ilivyokuwa kwangu. Wakati nimepata pesa ndiyo tuliondoka na mume wangu, lakini kabla hatujafika kwa sababu ni mbali nilibanwa sana na uchungu ndiyo ikabidi nitandike nguo nikajifungua kabla hata sijafika hospitali halafu baada ya hapo ndipo nikapelekwa kwa ajili ya huduma zaidi."

Alisema TASAF imefanyika kama mkombozi katika kijiji hicho kwa kuwa wananchi watakuwa wanapata huduma kwa urahisi na pia itasaidia wajawazito kuanzia kliniki karibu mpaka wakati wa kujifungua.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wanging'ombe, Joyce Mdemwa, alisema kutokana na ukosefu wa kituo cha afya katika kijiji hicho baadhi ya wanawake hupoteza maisha na kujifungulia njiani.

Mdemwa alisema kituo cha afya kilichopo ni katika kijiji kingine cha Kipengele ambacho kipo zaidi ya kilomita 40 na pia ni cha misheni na gharama za matibabu ni kubwa ambazo baadhi ya wananchi hushindwa kumudu.

"Kutokana na umbali na pia gharama katika kituo hicho cha afya cha Misheni, na nature ya kipato cha wananchi hawa wa vijijini wakati mwingine hushindwa kumudu au kutokana na kukosa pesa ya kutosha wanapata huduma ambayo haitoshelezi," alisema.



Mkurugezi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Sam Kamanga (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uhakiki wa wateja wa bima za maisha wa shirika hilo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# THRDC sasa yataka sheria kulinda watumiaji mitandao

**Na Salome Kitomari**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu nchini (THRDC), umeiomba serikali kuangalia uwezekano kutunga sheria ya kulinda data za watumiaji wa mitandao ya kijamii nchini.

Akizungumza jana wakati wa maadhimisho ya sita ya watetezi wa haki za binadamu, kwa lengo la kutambua na kuenzi haki za binadamu nchini, Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema ajenda kubwa ya mwaka huu ni kulinda nafasi ya watetezi wa haki za binadamu.

"Sasa hivi kuna mitandao mingi na kutembea mitandaoni imekuwa ni haki ya kibinadamu, inasaidia haki zieleweke, zilindwe na ziendelezwe, kwa kuwa duani kote mitandao ndiyo kila kitu katika maisha," alisema. "Kwa sasa data zetu ziko 'uchi' taarifa zetu hazina kokote zinakolindwa , tunataka tuwe na sheria ambayo italinda data zetu. Afrika kwa sasa kuna nchi 20 zina sheria ya kulinda data, na Afrika kuna watu milioni 400 kati ya watu milioni bilioni 1.3 na duniani watu bilioni 4 wako mtandaoni na Tanzania watu milioni 25 wako mtandaoni," alisema.

Alisema maisha mengi yako mitandaoni kwa kuwa imekuwa ni chombo maalum kinachosaidia haki zieleweke, zilindwe, zielimike na zilindwe.

"Ndiyo maana leo tumewatambua watu wanaofanya utetezi wa haki za binadamu mitandaoni, tumewatambua na kuwapa tuzo kwa kutambua mchango wao kwa kuwa juhudi zao zimepaza sauti," alisema.

Alisema kipindi cha uchaguzi ndicho ambacho kunakuwa na matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu, na asasi za kiraia ni waangalizi wa uchaguzi na kwamba watatoa mafunzo kwa makundi yote kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

# Wakulima sasa waboreshewa kupata mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA nchini watapata fursa ya kukopa kutoka katika mabenki na taasisi za kifedha, baada ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kuingia katika makubaliano na Mfuko Kichocheo wa SAGCOT CTF.

Lengo la malibaliano hayo ni kushirikiana katika kuboresha mazingira ya upatikaji wa mikopo yenye tija kwa wakulima ili kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

Akizungumza baada ya kusaini randama ya makubaliano hayo, Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti na Sera wa TADB, Dk. Nyankomo Marwa, alisema makubaliano hayo ni hatua muhimu katika kuleta mageuzi na kuongeza tija katika sekta ya kilimo ambacho ni nguzo inayotegemewa kuchagiza maendeleo ya viwanda.

"Kazi kubwa ya Benki ya Kilimo ni kuchachusha huduma za fedha katika sekta ya kilimo hivyo kupitia makubaliano haya yatasaidia zoezi la utoaji wa fedha kwenye miradi mbalimbali katika sekta ya kilimo na mifugo," alisema Dk. Marwa.

Dk. Marwa alisema mifumo ambayo imewekwa na SAGCOT – CTF itarahisisha zoezi zima la kuwafikia wakulima na hasa katika utoaji wa mikopo yenye lengo la kuijenga na kuimarisha sekta ya kilimo.

"Sisi kama Benki ya Kilimo tunalojukumu la kushirikiana na kufanya kazi na wadau katika sekta hii lengo likiwa ni kumkomboa mkulima na kuleta mageuzi ya kweli katika sekta hii muhimu katika uchumi wa Taifa," alisema Dk. Marwa.

Alisema awali kuliwa na changamoto zilizokuwa zikiwakabili wakulima na hasa wadogo ikiwamo kukopesheka na taasisi za kifedha, lakini kuwapo kwa TADB kumeweza kutatua baadhi ya vikwazo vilivyokuwa vinarudisha nyuma ukuaji wa kilimo.

Katibu Mtendaji wa SAGCOT, Kichocheo, John Kyaruzi, alisema makubaliano hayo yatasaidia kufanikisha maboresho yanayoendelea katika sekta ya kilimo na kuleta unafuu kwa wakulima katika ngazi zote.

"Kama utakumbuka wakulima wamekuwa wakikabiliana na changamoto nyingi hasa upatikanaji wa mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na hata pale walipofanikiwa kupata mikopo hiyo riba yake ilikuwa kubwa na kurudisha nyuma maendeleo ya kilimo," alisema Kyaruzi.

"Kuwapo kwa TADB na makubaliano ambayo wameingia yatakuwa ni mwarobaini kwa wakulima kunufaika na mikopo," alisema na kuongeza kuwa makubaliano hayo yatakuwa na maana kubwa kwa wakulima.

"Sisi tunajihusisha na mambo makuu mawili ambayo kuwatafutia wakulima masoko ya uhakika na kuwekeza kwenye miundombinu wezeshi kwa wakulima kuzalisha kwa wingi na kumfikia mlaji bila kikwazo chochote," alisema.

Kwa mujibu wa Kyaruzi, mfumo kichocheo haupo kwa ajili ya kushindana na taasisi za kifedha bali upo kwa ajili ya kuleta utengamano na kusaidia wakulima wanufaikie na huduma za kibenki kwa kupata mikopo yenye riba nafuu.

# Utandazaji mabomba gesi majumbani mwezi huu

WIZARA ya Nishati imesema kazi ya kutandaza mabomba ya gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani kwa mkoa wa Lindi inatarajia kuanza mwisho wa mwezi huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Waziri wa wizara hiyo, Dk. Medard Kalemani, alipokuwa akijibu swali la nyongeza Mbunge wa Kuteuliwa, Salma Kikwete.

Mbunge huyo alilitaka kujua ni lini wananchi wa Lindi watafikishiwa huduma ya gesi majumbani.

Akijibu, Waziri huyo alisema hatua hiyo inalenga kuhakikisha wananchi wanafurahia rasilimali inayopatikana katika eneo lao.

"Mradi wa gesi ya majumbani unatarajiwa kuifikia mikoa ya Lindi na Mtwara hadi Dar es Salaam na Mkoa wa Lindi kazi ya kutandaza mabomba ya kusambaza gesi majumbani itaanza mwisho wa mwezi Mei," alisema.

Dk. Kalemani aliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuhakikisha inaongeza kasi ya kusambaza gesi ya kupikia ili angalau robo ya nyumba za jiji la Dar es salaam ziwe zimefikiwa na huduma hiyo ndani ya miaka mitatu ijayo.

Katika swali la msingi la Mbunge Newala Vijijini (CCM), Rashidi Akbar, alisema kutokana na takwimu zilizopo, zinaonyesha gesi kutoka Mtwara na Songosongo inatumika kwa asilimia sita tu. "Je, kwa nini kiwanda cha Saluji cha Dangote na Mtwara Cement mkoani Mtwara havijapatiwa umeme wa gesi asilia hadi leo?"

"Pia aliuliza, Je, kwa nini wananchi wa Mtwara wasiunganishiwe gesi asilia kwenye nyumba zao?,"alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema kwa sasa TPDC inaendelea na utekelezaji wa mradi kwa kuagiza na kujenga miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani, viwandani na katika taasisi mbalimbali kwa mikoa ya Mtwara, Pwani na Dar es Salaam.

Alisema awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza gesi asilia mkoani Mtwara imeshaanza ambapo kwa sasa kazi ya ununuzi wa mabomba, mita za kupima gesi pamoja na vifaa vya kupunguza mgandamizo wa gesi inaendelea.

Alibainisha inategemea zaidi kata 120 za awali zitaunganishiwa mabomba ya gesi mkoani Mtwara kwa matumizi ya nyumbani ifikapo Juni mwaka 2019.



Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa (kulia), akikabidhi cheti kwa Mtendaji Mkuu wa wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Mhandisi Peter Ulanga, kwa kutambua mfuko huo kuwafikia wananchi wengi nchini, katika kilele cha maadhimisho ya miaka 10 ya mfuko huo yaliyofanyika Kitaifa katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yakana uchaguzi wa Zanzibar kuingiliwa

BUNGE limeelezwa kuwa si kweli kuwa Serikali imekuwa ikiingilia uchaguzi wa Zanzibar.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, wakati akijibu swali la Mbunge wa Malindi (CUF), Ally Salehe Ally, ambaye alitaka kujua ni lini Serikali ya Muungano itaacha kuwa na maslahi kwenye matokeo ya changuzi za Zanzibar ili mshindi atakayeshinda ndiye atangazwe.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema si kweli kuwa serikali inaingilia uchaguzi wa Zanzibar na kuwa chaguzi zimekuwa zikifanyika kwa sheria na kanuni za uchaguzi.

"Ila mara nyingi kumekuwa na vitendo vya vurugu kila nyakati za uchaguzi na kutokana na hali hiyo na majeshi ya ulinzi na usalama yataimarishwa wakati wa uchugazi ili kukabiliana na vitendo hivyo," alisema.

Aidha, alisema kutokana na chama kikuu cha upinzani Zanzibar ambacho ni CUF kuongoza kwa kukiuka sheria za uchaguzi jeshi la polisi litaendelea kudhibiti hali hiyo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Chwaka (CCM), Bagwanji Maganlal Meisuria, alisema mara nyingi wakati wa chaguzi mbalimbali Zanzibar kunajitokeza hali ya fujo na ukosefu wa amani na kusababisha wananchi kukosa amani na wakati mwingine kutoshiriki katika chaguzi husika.

"Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Zanzibar juu ya suala hilo?"alihoji.


Akijibu, Masauni alisema Serikali kupitia Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua mbalimbali kudhibiti vitendo vya vurugu nyakati za uchaguzi.

Alikiri kuwa nyakati za uchaguzi mkuu hukumbwa na vitendo vya uvunjifu wa amani hususani wakati wa kampeni na wakati wa kupiga kura.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi limekuwa likichukua hatua mbalimbali kudhibiti vitendo vya vurugu nyakati za uchaguzi.

"Napenda kuwafahamisha wananchi kuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha amani na utulivu vinatawala katika nchi wakati wote bila kujali nyakati au majirea mbalimbali katika mwaka," alisema.

Kadhalika, alisema Jeshi la Polisi linaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa askari ya ukakamavu, upelelezi na kuongeza vitendea kazi ili kuwajengea uwezo na weledi wa kuzuia na kukabiliana na vitendo vya uvunjifu wa amani vinavyojitokeza hususani wakati wa uchaguzi.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Wahitimu wa ufundi waahidiwa

SERIKALI imesema vijana ambao wamehitimu vyuo vya mafunzo ya ufundi katika ngazi ya cheti na diploma watakuwa na fursa nzuri kujiajiri na kuajiri pindi Serikali itakapoanzisha mpango kabambe wa kuanzisha vituo vya mafunzo wa vijana 'Incubation Youth Centre'.

Naibu Waziri wa Kilimo, Abdallah Ulega, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu swali Mbunge wa Ngara, (CCM), Alex Gashaza, ambaye alisema zamani kulikuwa na maeneo yaliyokuwa yametengwa kwa ajili ya mifugo na kilimo katika kutekeleza sera ya matumizi bora ya ardhi, lakini kadri idadi ya watu ilivyoongezeka maeneo hayo yamevamiwa na kusababisha migogoro.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema katika jukumu la kuainisha 'scheme' za ufugaji wa kisasa unaozingatia kanuni za ufugaji wa kisasa, Serikali kupitia Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) imeandaa mpango kabambe ambapo vijana waliohitimu vyuo vya mafunzo katika ngazi ya cheti na diploma watapata fursa ya kuanzisha miradi ya wafugaji kwa vitendo kwa muda maalumu chini ya wakala.

Alisema watakapohitimu watakuwa na fursa nzuri ya kujiajiri kupitia ufugaji, pia watakuwa na fursa ya kuanzisha mashamba ya mfano katika maeneo yao.

Naibu Waziri huyo alisema serikali imezindua rasmi mafunzo rejea kwa maafisa ugani na wafugaji kuhusu ufungaji bora nchi nzima. "Mafunzo hayo yanakusudiwa kutolewa kwa halmashauri zote nchini na yameanza kutolewa katika wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara," alisema.

Alibainisha wafugaji 750 na maafisa ugani 32 walipata mafunzo rejea na katika wilaya ya Kailua, mkoani Tabora mafunzo rejea yaliyotolewa kwa wafugaji 438 na maafisa ugani 33.

Alieleza mafunzo hayo yamejikita katika uboreshaji wa kosaafu za mifugo, udhibiti wa magonjwa, matumizi sahihi ya dawa na viuatilifu, uboreshaji viuatilifu, uelewa wa sheria, kanuni na miongozo ya sekta ya mifugo ili kuepukana na migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Alisema mpango huo umelenga kuongeza uzalishaji wa malighafi zitokanazo na mifugo zenye viwango bora ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya nyama, maziwa na ngozi vinavyoendelea kujengwa nchini. Kadhalika, alisema wizara imeendelea kuhamasisha wafugaji kuanzisha maeneo ya kuzalisha malisho bora ili kuongeza uzalishaji. "Wizara imeshaanzisha mashamba darasa ya mfano 365 katika maeneo mbalimbali nchini ili kuchochea wafugaji kujifunza na kuanzisha mbegu na malisho," alisema.

# Mfanyabiashara anyang'anywa maeneo Longido

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MFANYABIASHARA maarufu wa jijini Arusha, Philemon Monaban, ame nyang'anywa maeneo yake yalipo wilayani Longido ambayo anadaiwa kuyavamia kinyume na utaratibu, baada ya tume ya iliyoundwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Frank Mwaisumbe, kubaini hilo. Tume hiyo iliundwa kufuatilia mgogoro wa ardhi uliodumu kwa muda mrefu, kati ya mfanyabiashara huyo na Ismail Kilas, Jackline Bendera, Aisha Mkwawa na Jane Sylvesterna.

Akithibitisha tukio hilo jana wilayani humo, Katibu Tawala Wilaya ya Longido, Toba Nguvila, alisema Tume iliazimia chini ya Mkuu wa Wilaya

kuwa Mollel (Monaban), kuachia hayo maeneo ya watu hao sababu aliyavamia bila kufuata sheria.

Tume hiyo ilihusisha wataalamu mbalimbali kutoka Ofisi ya Mwanasheria, Ardhi, Mkurugenzi Mtendaji, Takukuru, Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi, Katibu Tarafa wa Longido, Ofisa Mtendaji Kata ya Kimokouwa, Mtendaji wa Kijiji cha Eworendeke na Mwenyekiti wa Kijiji cha Eworendeke.

Alisema muongozo uliotumika katika kuchunguza mgogoro huo ni kupitia hadidu tatu za rejea ambazo walipitia mikataba ya umiliki, kujiridhisha kama kanuni za umiliki kwa pande zote mbili zilifuatwa na pamoja na mambo mengine, ambayo kamati ingeona ni vyema kushauri katika mgogoro huo ili haki itendeke.

Hata hivyo, alisema tume iliitembelea eneo la mgogoro na kuwahoji watu muhimu, wakiwamo wahusika wa mgogoro, mashahidi wao, viongozi wa serikali ya kijiji husika, pamoja na wauzaji wa maeneo husika, hivyo watu 19 walifika mbele ya kamati kuhojiwa. Alisema Machi Mosi, mwaka huu, kamati iliwasilisha matokeo ya uchunguzi kwa kamati ya Usalama wilaya na ilipofika Machi 21, pande zote mbili ziliitwa na kusomewa mashtaka pamoja na mapendekezo ya kamati, Mkuu wa Wilaya alikubaliana na mapendekezo sita kati ya nane.

"Kamati ilipendekeza kuwa, viwanja namba 143E ni cha Aisha Mkwawa, 144E cha Jane Sylvester, 145E cha Jackline Bendera na 97E,99E na 101E apewe Ismail kilas, na hii ni baada ya kamati kubaini kuwa viwanja hivyo, ni mali ya wananchi hao," alisema.

Pia kamati ilipendekeza Kilas aonyeshwe eneo la kujenga darasa ili alijenge kwa haraka kama walivyokubaliana na kijiji.

Kilas alisema alipewa viwanja na Serikali ya Kijiji cha Eworendeke mwaka 2008 kwa makubaliano ya ujenzi wa maegesho ya magari.

"Nilipewa kiwanja plot namba tatu na kijiji, lakini waliniambia nijenge darasa moja katika kitongoji cha matiani, nilikubali kufanya hivyo na nikakabidhiwa hati ya umiliki wa kijiji hicho," alisema.

Alisema, hakufanikiwa kujenga darasa hilo kutokana na mvutano baina ya kitongoji cha Matiani na Losoiti, kwa kutaka kila mmoja darasa hilo lijengwe kwake.

"Baada ya kutokea mvutano baina ya vitongoji hivyo, serikali ya kijiji iliniandikia barua ya kusitisha ujenzi huo hadi pale watakapo azimia darasa hilo lijengwe wapi," alidai.

Alidai mwaka 2012, Monaban alivamia eneo hilo, akiwa na askari polisi wenye silaha za moto na kuweka uzio kwa kudai kuwa eneo hilo ni mali yake.

Alisema aliwasiliana na serikali ya kijiji baada ya kutokea hali hiyo na kijiji kilikanusha kumpa Monaban kiwanja hicho.

Alidai kuwa, aliwasilisha uonevu huo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Juma Mhina, pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe na ofisi hizo ziliunda tume ya kuchunguza jambo hilo.



Mtoto Kalebu Ezekiel (12) anaesoma darasa la sita katika Shule ya Msingi ya Twishini, akionyesha kipaji chake kwa kuchora picha mbalimbali, katika eneo la Makumbusho, jijini Arusha jana. Ezekiel alisema alianza kuchora akiwa na umri wa miaka mitatu na anatumia kipindi cha likizo na siku za Jumamosi na Jumapili kufanya shughuli hiyo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Walalamika kuuziwa Vitambulisho vya Taifa 10,000/-

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANANCHI wa Mtaa wa Nyunguu katika Halmashauri ya Mji wa Babati, Mkoani Manyara, wamelalamikia uongozi wa mtaa huo, kuwalazimishkulipia Sh.10,000 ili waweze kupatiwa Vitambulisho vya Taifa.

Malalamiko hayo waliyatoa jana mjini hapa, wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu kadhia hiyo ambayo inaongozwa na ofisi ya mtaa kupitia kwa Ofisa Mtendaji na baadhi ya wajumbe wa serikali ya mtaa.

Mmoja wa wakazi hao, Mustafa Rwamcho, alisema alienda siku moja ofisi ya mtaa huo ili aweze kuchukua kitambulisho chake, lakini alinyimwa kwa madai kwamba anatakiwa achangie mchango wa Shule ya Sekondari Babati Day, Sh. 10,000.

"Mimi baada ya kunidai nitoe fedha niliamua kukiacha na mpaka sasa sijarudi tena na sijui itakuwaje, maana hiki kitambulisho kinahitajika, mfano ukienda nje ya nchi unaweza ukatakiwa uonyeshe kitambulisho hicho, ili kuthibitisha uraia wako," alisema Rwamcho.

Aidha, alisema kwa kuwa hali yake kiuchumi haikuwa nzuri, alikiacha kitambulisho hicho huku akisema kuendelea kukikosa italeta madhara zaidi kwa kuwa mamlaka ya mawasiliano inawataka watumiaji wa simu kusajili laini za simu wawe na vitambulisho hivyo.

"Kwa kuwa rais Magufuli alishasema vitambulisho hivi ni bure,namuomba atusaidie kuwawajibisha viongozi wa namna hii, ambao wanatuuzia vitambulisho wakati vinatakiwa kutolewa bila malipo ya aina yeyote," alifafanua.

Mkazi mwingine, Leah Mapinda, alisema anashangaa ofisi ya mtaa, kuwatoza fedha hizo huku akidai mdogo wake alilipishwa fedha hiyo na kusisitiza kuwa endapo wataendelea kuwatoza wananchi ambao baadhi hawana uwezo hawatapata vitambulisho.

Mapinda alihoji waliopewa mwaka jana hawakutozwa Sh.10, 000, lakini mwaka huu viongozi wanaanza kuwatoza fedha hiyo, ilhali ni haki yao kupata Vitambulisho vya Taifa.

Musa Rajab, aliiambia Nipashe kuwa viongozi kuwatoza fedha wananchi katika kuwapatia vitambulisho ni kukiuka maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani Nchi, Kangi Lugola na rais John Magufuli wanapokuwa kwenye ziara zao.

Nipashe ilipoutafuta uongozi wa mtaa wa Nyunguu, iliwekewa masharti ya kuwa na kibali cha kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Babati ambacho ilipewa kwa maneno.

# Wanawake, wenye ulemavu wanufaika mikopo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

VIKUNDI 47 vikiwamo vya wanawake 36, vijana tisa na wenye ulemavu wawili, wamepatiwa mikopo ya thamani ya Sh. milioni 165.8 na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Mkurugenzi wa halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, akizungumza jana, alisema kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 walitenga Sh. milioni 207.8 kwa ajili ya mikopo hiyo.

Myenzi alisema kiasi cha Sh.milioni 26.2, bado hakijakopeshwa kwa vikundi kutokana na uhakiki wa vikundi ambavyo vimeomba.

Alisema halmashauri hiyo imeweka utaratibu wa kutenga kiasi kisichopungua Sh.milioni 20 kila mwezi, ili kuhakikisha walengwa wananufaika na mikopo hiyo kulingana na sheria.

"Fedha za mikopo bado tunazo kwa ajili ya kuvipatia vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu hivyo ni wao kujipanga na kuchangamkia fursa hiyo kikamilifu," alisema.

Alisema kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Aprili 2019, kumefanyika marejesho ya Sh.milioni 58.4 ambazo zinatumika kwa ajili ya uhamasishaji, ufuatiliaji, uhakiki wa vikundi na kuvikopesha vikundi vingine.

"Changamoto kubwa ni vikundi vya vijana kuwa na wanachama wanaozidi umri wa miaka 35 hivyo kukosa vigezo na vikundi vya wenye ulemavu kuwa vichache, licha ya uhamasishaji mkubwa kufanyika," alisema Myenzi.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kutoa mikopo kwa vikundi hivyo kwa kuwa wametekeleza ahadi ya serikali.

Mnyeti alisema ni Sera ya Serikali Kuu kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu, kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya kila halmashauri ya wilaya.

"Nawapongeza kwa kutoa mikopo hiyo ila idara ya maendeleo ya jamii endeleeni kutoa elimu, ili mikopo itolewe kupitia asilimia nne za wanawake, nne za vijana na mbili za walemavu," alisema.







Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbulu, mkoani Manyara, Hudson Kamoga (kushoto), akifurahia jambo na wazee wa kimila wa Kata ya Dongobesh ambayo ni makao makuu mapya ya halmashauri hiyo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mghwira ataka wajane wasaidiwe

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewataka viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasaidia wanawake wajane baada ya kufiwa na waume zao ili kupata haki zao. Akizungunza na Nipashe, alisema katika Mkoa wa Kilimanjaro, wajane wengi wamekuwa wakinyanyaswa kwa kudhulumiwa mali baada ya waume zao kufariki dunia hali inayopelekea migogoro katika familia.

Alisema wajane wengi wanapoteza haki zao baada ya waume zao kufariki hali ambayo inapelekea kubaki na visasi, huzuni na ongezeko la watoto wa mitaani na magonjwa kutokana na msongo wa mawazo. "Nawaagiza viongozi wote kwanzia ngazi ya kitongoji hadi mkoa kuhakikisha wanasimamia na kutetea haki za wajane baada ya wenzi wao wanapofariki ili kupunguza migogoro dhuluma kwa wajane na watoto," alisema. Alisema umefika wakati kinamama kuwa na sauti moja ya kukemea ukatili, ukeketaji na kurithiwa baada ya waume zao kufariki, hali ambayo inaleta ongezeko la mitafaruku katika familia na kukwamisha maendeleo.

Alisema viongozi wote hasa wa wilaya na mkoa wahakikishe wanafanya kazi ya kuwa wasuluhishi wa migogoro katika kutoa elimu kwa wananchi ili kuondokana na mila na desturi za ukandamizaji wa wanawake katika jamii.

"Nawaomba viongozi wa dini kuombea amani, kuwapa wananchi wa mkoa matumaini mapya kwa kuwapa ushauri, nasaha za kuachana na vinyongo vilivyosababishwa na kudhulumu mali kwa muda mrefu ... kwani vinyongo hasira na mambo yanayofanana na hayo husababisha magonjwa mbalimbali ikiwamo kansa," alisema.

Mmoja wa wajane katika Wilaya ya Moshi, Faustina Msaki, alikiri kuwapo kwa ukatili kwa wajane baada ya wenzi wao wanapofariki na kuiomba serikali kukeme jambo hilo kwa vitendo bila kupokea rushwa kwa wenye nacho.

"Tunaiomba serikali mbali na kushiriki kwenye vikao vya familia na kutoa elimu, pia mahakama zetu zisimamie sheria haki na usawa bila kumtizama mwenye nacho," alisema Elisaria Masawe.

Mkurugenzi wa shirika la kutetea haki na msaada wa kisheria (KWIECO), Elizabeth Minde, alisema ikiwa mkuu wa mkoa pamoja na watendaji wake watasimamia kwa vitendo changamoto zanazowakabili wajane, watasaidia haraka na tatizo la watoto wamitaani litageuka historia mkoani Kilimanjaro.

# Siha yapewa siri kuongeza mapato

**Na Mary Mosha,** SIHA

WAFANYABIASHARA wa soko la Sanya Juu Wilaya ya Siha, wamesema ikiwa Halmashauri hiyo itataka kuongeza mapato ni lazima iweke mikakati ya kuboresha vyanzo ikiwamo kulipa soko hadhi ya wilaya.

Ester Maro, mfanyabiashara wa mazao ya mboga mboga katika soko hilo aliiambia Nipashe kuwa bado miundombiu ya soko hilo sio rafiki kwa wafanyabiashara wa aina zote licha ya halmashauri kukusanya mapato.

"Imefika mahali sasa uongozi wa wilaya hiyo kufanyia ukarabati miundombinu ya soko hilo... tuondokane na kero tunazopata hasa za uwapo wa uchakavu vyoo, ukosefu wa vizimba jambo linalohatarisha usalama wa afya wa watumia soko ," alisema Ester.

Cecilia John, alisema Wilaya ya Siha haijawa tayari kutekeleza mpango wa uchumi wa viwanda kwa vitendo kwa kuwa wanashindwa kuboresha vyanzo vya mapato.

"Hali ya soko la Sanya Juu bado ni mbaya hasa katika upande wa miundombinu, tunamuomba mkurugenzi kuangali uwezekano wa kutenga bageti kwa ajili yetu ili kuweka mazingira bora ya wafanyabiashara kujikusanyia na kuendelea kulipa ushuru," alisema Cecilia. Abeid abdalla, alisema kuwa soko hilo ni moja

kati ya masoko ambayo yakiboreshwa vyema yanaweza kuwasaidia wakulima wanaotoa mboga shambani pamoja na wauzaji wa nafaka. Alisema licha ya kulipa ushuru kila siku, lakini hamna jitihada zozote zinazofanywa na halmashauri katika kulifanyia matengenezo soko hilo.

Nicholous Masaki, mkusanya ushuru katika soko la Sanya Juu, alisema licha ya kuwasilisha malalamiko yao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa hadi sasa.

Akizungumzia hali ya ukusanyaji mapato kwa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo, Valerian Juwal, alisema wapo katika hatua za kufanya marekebisho katika soko hilo na kuwataka wafanyabiasha kuwa watulivu.

"Tutaboresha ukusanyaji wa mapato sanjari na kuboresha miundominu mbali mbali ya kuongeza upatikanaji wa mapato," alisema Mkurugenzi huyo.

# Kampeni upandaji miti yaja

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KIKUNDI cha Amani 9 Arisi Marangu, kilichopo wilayani Moshi Vijijini, kimezindua kampeni maalum ya kupanda miti zaidi 12, 000 katika maeneo mbalimbali zikiwamo taasisi za Serikali, dini, binafsi na maeneo ya wazi ili kurejesha uoto wa asili.

Katibu wa kikundi hicho, Hance Moshi, alisema kampeni hiyo inatarajia kuhifadhi mazingira katika maeneo tofauti ya wilaya hiyo ikiwamo hifadhi ya mazingira yanayozunguka Mlima Kilimanjaro ili kuendelea kulinda theluji yake.

"Katika hatua za awali za kampeni yetu, leo tumeotesha miti 780 katika Shule ya Sekondari Mieresini ili kuwahamaisha wanafunzi kuona umuhimu wa hifadhi mazingira na tunaamini juhudi hizi watazipeleka katika makazi yao," alisema.

Alisema kampeni hiyo inayoendeshwa chini ya shirika la mazingira la Floresta Tanzania, itadumu kwa zaidi ya miaka 20 ili kurejesha uoto wa asili ulipotea kutokana na shughuli za kibadamu katika maeneo tofauti ikiwamo vyanzo vya maji na mito.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Mieresini, Fidelis Barnabas, alitaka kuwapo kwa kanuni za kudumu katika suala la hifadhi ya mazingira ambapo kila mwanajamii atalazimika kuzifuata badala ya kila taasisi kuwa na utaratibu wake.

"Juhudi zinazofanywa na kikundi hiki ni za kuungwa mkono kwa kuwa zimeongeza chachu ya shule yetu katika jitihada ambazo tumeziendeleza kwa muda mrefu, tutajiwekea utaratibu kila mwanafunzi aoteshe mti na kuutunza hadi amalizapo shule," alisema.

Naye mwanachama wa kikundi hicho, Jackson Shao, aliomba viongozi wa serikali za mitaa kuhakikisha kuwa wanatoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira na athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira ili kazi yao iweze kuwa endelevu.



Ukurasa 18

## Guinea Bisau yachagua wabunge

## Burundi inavyohaha kujiunga SADC



Ukurasa 19



RIPOTI YA SIPRI:

## matumizi ya kijeshi yaongezeka duniani

Ukurasa 17


# siasa

JUMATANO MEI 1, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

## Rais Tshisekedi 'anavyoteseka' kuunda serikali

MEI MOSI

# 'MAY DAY'; Jadi inayofifia ya mshikamano wa wafanyakazi

**Na Anil Kija**

MEI MOSI ni siku inayosherehekewa kote duniani kila mwezi wa Mei unapoanza, lakini tofauti na siku zingine maalum zenye itikadi inayoeleweka, 'May-Day' kama inavyoitwa kwa lugha inayofahamika zaidi kote duniani ina hisia tofauti, kulingana na mazingira ya nchi.

Ni sikukuu iliyokuwa na nguvu sana miaka ya 1960 hadi 1980 ilipokwisha, na baada ya hapo imepoteza nguvu na mwelekeo karibu kila mahali duniani.

Sababu ni kuwa iliendana sana na kipindi kilichofuata Vita Vikuu vya Pili ambako nchi za Magharibi ziliingia katika dira ya 'social democracy;' ambayo kimsingi ilichanganya ubepari na malengo mahsusi ya ustawi wa jamii, wafanyakazi.

Hapa nchini kwa mfano, May Day ilikuwa hasa ni siku ya mashirika ya umma, ambako walikuwa wanaonyesha wanachokifanya katika sikukuu nyingine za kitaifa kama Sabasaba (iliyogeuka kuwa ya maonyesho ya biashara) na Nanenane (ya wakulima).

MayDay ilikuwa hasa ni siku ya ainisho la kiitikadi la kuenzi siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, iliyoanza kufifia miaka ya awali

INAENDELEA UK.16



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu Jenista Mhagama. **PICHA: MTANDAO**

## Viongozi Sudan Kusini bado wajitafuta licha ya 'mguso' wa Papa Francis

Ukurasa 15

MEI MOSI

# Sudan 'itakavyoishi' bila Al Bashir

## • Bado anawatumia 'mawaziri wa Kabila' kuiongoza DRC



Rais Felix Tshisekedi wa DRC (kulia), akiwa na mtangulizi wake Joseph Kabila. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

BAADA ya kutwaa madaraka kufuatia Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, Rais Felix Tshisekedi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) bado hajaunda Serikali yake, badala yake anaendeleo kuwatumia waliokuwa mawaziri katika utawala wa Joseph Kabila.

Itakumbukwa kwamba siku chache baada ya ushindi wake, kuapishwa na kuingia Ikulu ya Kinshasa, Rais Tshisekedi aliingia 'makubaliano' na mtangulizi wake, Kabila kuunda serikali ya umoja. Serikali hiyo bado haijaundwa.

Hatua hiyo ilichagizwa zaidi na matokeo ya uchaguzi huo kukiwezesha chama Union for Democracy and Social Progress (UDPS) cha Rais Tshisekedi na muungano wa Union for the Congolese Nation (UNC) kupata viti vichache bungeni huku kilichokuwa chama tawala cha Common Front for Congo (FCC) kilichoongozwa na Kabila kikiwa na wabunge wengi.

Kwa matokeo hayo, Rais Tshisekedi anakabiliwa na hatari ya kutomudu kulidhibiti Bunge la Taifa, hali inayoweza kuufanya utawala wake kushindwa kufikia malengo yanayokusudiwa.

Machi 6, mwaka huu wawili hao, yaani Rais Tshisekedi na Kabila walitoa tamko la pamoja kuthibitisha nia yao ya 'kutawala wakiwa katika serikali ya umoja.'

> Watu wenye silaha waliingia Goma na kuwaua raia wasiokuwa na hatia na hawakutiliwa shaka na polisi wala askari wa jeshi la Taifa.

Hata hivyo, hatua ya Rais Tshisekedi kuchukua nafasi ya Rais Kabila aliyedumu madarakani kwa takribani miaka 18 katika taifa hilo kubwa ndani ya ukanda wa Kusini mwa Afrika, ilitabiriwa kuwa ni changamoto kubwa kwake.

Licha ya muungano wa FCC, ulioongozwa na Rais Kabila kushindwa katika Uchaguzi Mkuu wa Desemba mwaka jana, lakini ulifanikiwa kupata viti vingi kwenye Bunge la Taifa na mabaraza ya majimbo nchini humo.

Kwa hali hiyo, Rais Tshisekedi bado hajaunda Serikali na kwa sasa anaendelea kufanya kazi na waliokuwa mawaziri wa serikali ya Kabila.

Jitihada za Rais Tshisekedi kuunda serikali zinafuatiliwa kwa karibu na raia wa nchi hiyo pamoja na jumuiya za kimataifa kutokana pamoja na mambo mengine, hisia kwamba huenda serikali hiyo ikazidiwa nguvu na ushawishi wa Kabila na hivyo Rais huyo mstaafu akaendelea kutawala siasa za nchi hiyo.

Pamoja na sitofahamu iliyopo kuhusu kuundwa kwa serikali ya Rais Tshisekedi, bado hali ya usalama imeendelea kuwa changamoto kutokana na kukosekana kwa utulivu kwenye baadhi ya maeneo ya nchi hiyo.

Kwa mfano, taarifa zinaeleza kuwa kwenye mji wa Beni uliothiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa ebola kwa takribani miezi 10 sasa na jimbo la Kivu Kaskazini, bado vikundi vya waasi vinaendelea kufanya uovu wao.

Kikundi cha ADF kinachotajwa kuwa na mizizi ya waislamu wenye imani kali kilichoanzia Magharibi mwa Uganda mwaka 1995, kinazidi kuwa imara kwenye eneo la mpaka lenye vikundi vingine vya waasi.

ADF inashutumiwa kwa kuwaingiza na kuwatumia watoto kuua maelfu ya raia wa DRC wasiokuwa na hatia pamoja na waangalizi wa amani wa Umoja wa Mataifa ambao idadi yao imefikia 22.

Ni kwa hali hiyo, Rais Tshisekedi anashauriwa na Msemaji wa wakazi wa Beni, Janvier Kasairyo kwamba anapaswa kufanya uangalizi wa karibu wa kulisimamia jeshi, polisi na idara ya usalama wa nchi hiyo.

Hivi karibuni, Rais Tshisekedi aliwatembelea askari waliojeruhiwa na kupata matibabu kwenye hospitali ya kijeshi iliyopo Beni.

Mbali na askari hao, Daktari wa Shirika la Afya Duniani (WHO), alipigwa risasi na kufa na mwanamgambo aliyeshambulia hospitali iliyopo karibu na mji wa Butembo.

Kwa Rais Tshisekedi, matukio kama hilo ni miongoni mwa ishara anazopaswa kuzifanyia kazi na kuziona kuwa ni changamoto zinazoukabili utawala wake na ndio maana Umoja wa Mataifa umemtaka kuchukua hatua mapema.

"Matarajio ya Wacongoman ni makubwa na hawapaswi kuachwa wakisubiri kwa muda mrefu, ama kukatishwa tamaa," Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa, Leila Zerrougui alikaririwa akiliambia Baraza la Usalama.

Akiwa katika kampeni zilizomuingiza madarakani, Rais Tshisekedi aliwaahidi wakazi wa jimbo la Kivu ya Kaskazini kwamba miongoni mwa mambo ambayo angeyashughulikia kwa haraka ni kuvidhibiti vikundi vya waasi na kurejesha amani ya kudumu kwenye eneo hilo.

Wakati hali ikiwa hivyo, Rais Tshisekedi anatambua ahadi nyingi alizozitoa wakati wa kampeni, ikiwamo kuvidhibiti vikundi vya wanamgambo wa waasi hasa vilivyojikita kwenye jimbo la Kaskazini la Kivu.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, wapo wanaoamini kwamba, wakati akionekana 'kufungamana' na Kabila, Rais Tshisekedi hajaonyesha ishara za kutumia madaraka yake kukabiliana na matatizo sugu yanayoikabili DRC.

Lakini Rais Tshisekedi mwenyewe alikaririwa hivi karibuni akiwaonya watu wanaovisaidia vikundi vya wanamgambo na wanajeshi waasi akisema,

"Ninawaonya watu wote wanaowaunga mkono vikosi vya kijeshi, sheria itachukua mkono wake kwa nguvu zote," anasema na kuongeza:

"Kwa wote waliokamatwa, bila kujali kama ni watunga sheria katika ngazi za taifa ama majimbo, watafikishwa mbele ya vyombo vya sheria na watachukuliwa hatua kwa kusababisha mauaji."

Lakini wachambuzi kadhaa wa masuala ya amani ya DRC wanaeleza kuwa tamko hilo linaonekana kukosa vitendo halisia na utashi wa kisiasa.

Kivu Kaskazini inayopakana na Ziwa Kivu ni eneo lenye utajiri wa madini likikabiliwa na machafuko ya mara kwa mara yanayohusishwa na uwapo wa rasilimali zenye thamani.

Wakati Rais Tshisekedi alipofanya ziara kwenye eneo hilo hivi karibuni, raia mmoja, Manasse Mutabesha alikaririwa akisema, "kuwapo kwa amani kutasababisha mambo yote kuwa sawa, kutokana na amani fedha zitapatikana, kazi zitakuwapo."

Wakati akifanya ziara hiyo, Rais Tshisekedi alijulishwa katika kikao chake na Baraza la Usalama kuhusu kuibuka kwa mapigano kwenye eneo la Goma.

"Watu wenye silaha waliingia Goma na kuwaua raia wasiokuwa na hatia na hawakutiliwa shaka na polisi wala askari wa jeshi la Taifa," Kaimu Waziri wa Mambo ya Ndani Basile Olongo, alidokeza katika kikao hicho.

Waziri huyo alitoa taarifa akisema, Rais Tshisekedi aliwaonya wanasiasa vigeugeu wanaohusishwa na vikundi vya waasi wenye silaha kwamba hawatavumiliwa.

Swali linabaki kuwa, je itamchukua muda gani Rais Tshisekedi kuunda serikali yenye kuakisi muundo wa utawala wake kwa taifa hilo? Pengine ni suala linaloendelea kusubiriwa.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.***

MEI MOSI

# Viongozi Sudan Kusini wajitafuta licha ya 'mguso' wa Papa Francis

**Na Michael Eneza**

HAPATAKUWA na amani ya mara moja kutokana na hatua isiyo ya kawaida ya Papa Francis kuwabusu miguu viongozi wakuu wa Sudan Kusini wanaogombana, Rais Salva Kiir na kiongozi wa upinzani Dk. Riek Machar, Aprili 11.

Ilikuwa ni katika kikao cha viongozi wa dini wa makanisa ya Katoliki, Anglikana na Presbyterian ambako viongozi wa Sudan Kusini walialikwa.

Aliwaasa viongozi hao walioku-wa wamepigwa na butwaa wakati Papa Francis, mwenye umri wa miaka 82 na ni mgonjwa wa miguu, alipochuchumaa kwa taabu na kubusu miguu ya mahasimu hao wanaolazimika kushirikiana kudumisha umoja wa nchi hiyo. Dunia nzima ilitazamia wameelewa.



Papa Francis (aliyeinama), akishika miguu ya Rais wa Sudan, Salva Kiir (wa pili kulia). Kulia ni mpinzani wa Rais Kiir, Dk. Riek Machar. **PICHA: MTANDAO**

Licha ya kutokuwapo amani endelevu katika mazingira ya sasa, inaelekea hatua zilizochukuliwa awali, na hasa kuzingira mali za viongozi hao wawili na labda alikuwa anabanwa zaidi Dk. Machar kwani alikuwa anaishi Afrika Kusini muda wote, hivyo mali zake zikizuiliwa angeweza kupata matatizo.

Ni Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ambayo ilitoa onyo kwa Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya na Rais Yoweri Museveni kuzuia mali za viongozi hao wawili, ambao mashirika ya ujasusi ya Marekani yanafahamu ziliko zote, na hatua za kufikia amani ya kudumu zikaanza kuchukuliwa. Bado kuna mvutano kuhusu muundo wa serikali na nafasi ya Machar.

Sudan Kusini ilifikia hatua ya kujiamulia mambo yake yenyewe ndani ya utawala wa 'Kiarabu' wa Sudan mwaka 2005 baada ya vita ya miaka 22, kuanzia mwaka 1983 iliyoongozwa na hayati Dk. John Garang.

Kutokana na Sudan Kusini kuwa mkusanyiko wa majimbo wa makabila makubwa ya Nuer na Dinka yanayoshindana katika jadi yao hadi sasa.

Majimbo hayo yalikuwa na serikali za ndani chini ya utawala wa jumla wa kijeshi Kaskazini ya nchi hiyo, na tofauti hizo zilibakia katika kipindi cha kufikia kujitawala.

Halafu uadui ukainuka kutokana na kifo cha kutatanisha cha Dk. Garang, ndege yake ikianguka porini akitokea Kampala nchini Uganda kwenda Juba, halafu kundi shindani la kabila la Dinka, likiongozwa na Salva Kiir, kufaidika na kifo hicho badala ya kina Machar, wa-Nuer.

Kuaninisha kuwa suala hilo bado ni kaa la moto katika siasa za Sudan Kusini, mjane wa Dk. Garang, Rebecca Nyandeng Garang de Mabior alirudi Juba kuelekea mwisho wa mwaka jana, na baada ya Marekani kutoa tishio kwa Uganda na Kenya kuhusu mali za mahasimu hao, Rais Kiir akaona amtumie mjane huyo kama 'turufu' dhidi ya Dk. Machar.

Aliondoa mpangilio wa makamu wanne wa rais ambao Machar ameukataa na haina ladha katika majadiliano kidiplomasia, akaweka wawili, yaani Rebecca Nyandeng na Dk. Machar.

Ni wazi kuwa kiongozi huyo wa upinzani hana raha na mpangilio huo, ndiyo maana ameahirisha tena kurudi maskani Juba.

> Kimsingi ni Dk. Machar aliyepoteza uwezo wa kubadili hali ya kisiasa nchini humo kwa mtutu wa bunduki, na si ajabu mabadiliko nchini Sudan yatamgusa kiasi fulani.

Tayari viongozi wa nchi za Jumuiya ya Ushirikiano wa Serikali za Maziwa Makuu (IGAD) wameita mkutano kujadili kukwama kwa uelekeo wa amani na kuundwa kwa serikali ya pamoja Sudan Kusini.

Bila hatua hiyo kufikiwa kunakuwa na wingu la kisheria kuhusu uhalali wa maamuzi ya watawala wa Juba, kwani nchi hiyo tayari ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo ina kanuni za aina ya utawala unaoweza kuiwakilisha nchi na kuweka saini yake katika mikataba.

Ni kanuni ya kawaida ya sheria za kimataifa kuwa serikali inayoweza kuingia mkataba inabidi iwe inatambuliwa na pande zote za nchi, na siyo king'ang'anizi tu.

Wakati IGAD na nchi nyingine hasa EAC na mashirika ya kimataifa wanatazamia kuwa serikali ya umoja wa kitaifa inaundwa mwezi Mei huko Juba, Dk. Machar ametamka kuwa serikali ya umoja wa kitaifa haitakuwa tayari mwezi Mei.

Anataka kipindi cha miezi minane kiongezwe baada ya kipindi cha awali cha miezi sita tangu Marekani itoe tahadhari hiyo mwaka jana, na kulazimisha maafikiano Septemba 2018 kuunda serikali miezi sita kunzia hapo.

Na hivi karibuni Rais Kiir akatangaza mfumo wa kuwa na makamu wa rais wawili kwani hataki kufanya kazi na Dk. Machar kama makamu wa rais tangu amfukuze katika nafasi hiyo mwaka 2011.

Rais Kiir amefadhaishwa na msimamo huo akisema kuwa kuendeleza kipindi cha mpito ni ishara ya kutokuwa na dhamira njema wakati ambapo nchi nzima iko tayari kuanza upya, kuacha mafarakano yaliyochukua miaka mingi.

Licha ya majadiliano yanayoendelea, wako baadhi ya wachunguzi wa habari wasiotazamia kuwa kuna uwezekano wa kufikia mapatano ambako Dk. Machar anakuwa makamu wa rais kamili, kwani dhamira yake ni kutawala pamoja na Rais Kiir, na siyo kumsaidia tu katika kazi zake.

Kwa jinsi hali ilivyoenda, angependelea kuwe na mfumo wa majimbo na shirikisho, lakini chama cha ukombozi ni kimoja na jeshi lilikuwa moja, na walioko na Dk. Machar hawana chimbuko jipya halisi la kisiasa au kizalendo, nje ya dukuduku za kikabila, vyeo.

Wakati mzozo huo wa kuunda serikali ya umoja wa kitaifa unaendelea, nchi hiyo yenye utajiri wa mafuta na mparaganyiko wa miundombinu imeomba nchi wahisani kutoa sehemu kubwa zaidi ya kiasi cha dola milioni 285 (sh. bilioni 650 takriban) kuwezesha utekelezaji kikamilifu wa makubaliano hayo.

Sehemu kubwa ya fedha hizo ni wazi zingetumika katika kuwalipa watumishi serikalini na baadhi ya makada wa upinzani watakaoachwa katika serikali mpya ya umoja wa kitaifa, kama walikuwa wameajiriwa kabla, au wanaacha nafasi za upinzani kijeshi kurudi uraiani.

Hata hivyo, nchi wahisani hazi-ridhishwi na hatua za kuweka sawa matumizi ya serikali na uwazi, hali ambayo inaweza kuleta kiwingu ni kwa kiasi gani fedha hizo zitatolewa au kupatikana - kwa wakati.

Dk. Machar alikimbia jiji la Juba wakati risasi zinarindima mwaka 2016 wakati vipande vya jeshi la nchi hiyo na makundi yake ya 'waasi' walipokuwa wanaelekea kushindwa vita na Juba kudhibitiwa na utawala ulioko madarakani.

Hali hiyo ya mapigano iliendelea huku makamanda wa upinzani wakihama kurudi kuunga mkono serikali na baadhi ya maofisa wa juu wa jeshi la serikali mara kadhaa walihama kujiunga na upinzani.

Ila baada ya tishio la Marekani la kukamata mali za viongozi hao wawili, tishio la vita limepungua na kuna misukumo tu ya kisiasa ya jinsi ya kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.

Kimsingi ni Dk. Machar aliyepoteza uwezo wa kubadili hali ya kisiasa nchini humo kwa mtutu wa bunduki, na si ajabu mabadiliko nchini Sudan yatamgusa kiasi fulani.

Kuonyesha mabadiliko yanayoendelea nchini, ilitoka taarifa ya redio moja huru jijini Juba kuwa askari 3,000 wa upinzani na wale wa serikali wanapewa mafunzo pamoja, ambayo ina maana kurudisha umoja katika ngazi ya jeshi na kuacha wanasiasa 'wamalizane' watakavyoweza.

Na ndicho alichokisema Papa Francis alipochukua hatua isiyo ya kawaida ya kuwabusu miguu yao, akiwaasa kuwa wananchi wa Sudan wamechoshwa na vita na sasa wanataka amani na ustawi wa jamii hiyo.

Halafu kama ilivyokuwa mwanzo wakati wa utawala wa 'Kiarabu,' kuna mvutano mkubwa kuhusu mipaka ya majimbo, kwani kuna kinyang'anyiro cha fedha za mafuta kila jimbo.

MEI MOSI

# ‘MAY DAY’; Jadi inayofifia ya mshikamano wa wafanyakazi



Bendi ya Jeshi la Magereza ikiongoza maandamano ya wafanyakazi katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei mosi)

**INATOKA UK.13**

ya mwongo wa 1980 kutokana na mkwamo wa uchumi uliofuatia vita vya Tanzania na Uganda, licha ya kuwa vilipiganwa kwa miezi takriban nane.

Ni hali iliyolazimisha kuzoa malori yaliyokuwa yanatumiwa na mashirika ya umma, bila kuwepo mifumo ya ukopeshaji, ili vita vilete faida.

Watunza kumbukumbu wanasema kuwa May Day ilianzia Marekani katikati ya karne ya 19 katika kipindi ambacho nchi ya Marekani ndiyo kwanza ilikuwa inaunganishwa baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoondoa mfumo wa kibiashara (kilimo na mazao hasa pamba kwa kutumia watumwa) ili kuiuza nje, hasa Uingereza.

Marekani ikaunganishwa kwa mfumo wa kibepari ambako viwanda vilianza kuchipuka kwa haraka hasa eneo la Kaskazini, wakataka mfumo wa utumwa uondolewe ili kila mtu awe na uhuru wa kuhama na kukaa au kujistawisha kokote atakapo nchini humo.

Majimbo yaliyotetea utumwa yakashindwa, Marekani ikawa moja.

Ndiyo maana ukizungumzia May Day Marekani unazungumzia itikadi hiyo ya awali ya uhuru wa mtu kukaa anapotaka na kufanya kazi, hivyo MayDay ni sikukuu ya wafanyakazi ambao tofauti na nchi za Ulaya, jeraha walilokuwa wanapambana nalo siyo waajiri, bali watumikishaji, mabaki ya umwinyi na utumwa.

> Kwa mfano muda mwingi ulitumiwa kudai haki ya kuunda vyama vya wafanyakazi ambavyo mwajiri anatakiwa ajadiliane navyo ili kufikia maamuzi yanayogusa watu wote.

Nchi za Ulaya zilikuwa na harakati tofauti ambako watu wengi waliondolewa mashambani na kujazana mijini wakati wahodhi ardhi, mamwinyi wakipangisha wafanyabiashara wanaotaka kufuga kondoo kwa manyoya kutumiwa katika viwanda, mwisho wa karne ya 18.

Hivyo ujio wa May Day barani Ulaya ilikuwa ni mapambano na mabepari.

Harakati hizi barani Ulaya zimekuwa na sehemu takriban tatu, zenye umuhimu tofauti kulingana na mazingira ya nchi husika.

Sehemu ya kwanza (ya kale, hasa Uingereza) ikiwa ni ya mwisho wa karne ya 18, kuvunja mashine ambazo ziliharibu uwezo wa mafundi stadi kupata riziki zao. Kwa mfano mashine zinazotumia nguvu ya stimu (maji yanayochemshwa na kubanwa ili kuendesha mtambo, kama treni za zamani zilivyoendeshwa) iliondoa mitambo ya kufuma nguo kwa mikono, iliyokuwa inatoa ajira kwa watu wengi.

Kuvunja mitambo ni kama ugaidi wa enzi hizo, kwani ugaidi wa siku hizi una nia kama hiyo, kutetea jadi inayoharibiwa na uhuru.

Mfumo wa viwanda uliposhika kasi na wazaliwa wa mafundi stadi nao kupoteza kumbukumbu ya kazi za baba zao, na watu kuanza kufurahia maisha ya mijini na siyo kukumbukia vijiji na miji midogo ambako mafundi stadi waliheshimiwa sana, harakati zikabadilika.

Zikaanza harakati za kisasa katikati ya karne ya 19 za kudai maslahi katika eneo la kazi, kutetea haki ya kuundwa kwa vyama vya kisekta au fani husika ili kuweka mshikamano kudai haki zao, hasa kupunguzwa kwa urefu wa saa za kazi.

Katika enzi za ubepari mchanga ‘wa kinyama,’ kazi ya ajira haikuwa tofauti na utumwa kwani mtu alihitajiwa afanye kazi kwa takriban saa 16, halafu zikawa 12, halafu 10 na karne iliyopita, ndipo viwango vya kimataifa vikafikiwa kuwa muda wa kufanya kazi kwa siku ni saa nane tu, basi.

Kila mwongo (miaka 10) katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi ilikuwa na jambo la kutetea haki za wafanyakazi ambalo linakuwa halijaimarika ukilinganisha na maeneo mengine.



Rais John Magufuli akiwasili kuhutubia wafanyakazi katika sherehe za Mei Mosi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kwa mfano muda mwingi ulitumiwa kudai haki ya kuunda vyama vya wafanyakazi ambavyo mwajiri anatakiwa ajadiliane navyo ili kufikia maamuzi yanayogusa watu wote.

Kilichobadilika katika miaka ya mwisho ya karne iliyopita ni maendeleo ya haraka ya teknolojia na kuondolewa kwa mashine zinazohitaji watu wengi pale ‘roboti’ zilipoanza kutumika au mitambo ya kusukuma bidhaa katika mstari wa kuongeza thamani. Chupa TBL zinapita tu zinajazwa, kuzibwa.

Kuna eneo moja la haki za wafanyakazi ambalo ni la mapambano au harakati endelevu lakini hata hivyo nalo limekuwa likififiafifia, kwani mkusanyiko wa wafanyakazi hauna uwezo wa kudai haki hizo kwa pamoja, yaani haki ya kulipwa kima cha chini cha mishahara kinachowezesha mfanyakazi kuishi, yeye na familia yake.

Haki hiyo ilitambuliwa wakati wa ‘social democracy’ ( au Marekani waliita ‘New Deal’) ikaenea kote baada ya Vita Vikuu vya Pili lakini Marekani ilianza wakati wa kutatua hitilafu kubwa ya uchumi, mparaganyiko wa uchumi wa kibepari wakati wa Great Depression (mfadhaiko wa jumla wa uchumi).

Miaka ya 1980 suala hilo lilipauka.

Sababu ni kuwa madai ya kima cha chini cha mshahara huwa yanaongezeka kulingana na wafanyakazi kada za juu wanavyolipwa, ili wale wa chini wasitupwe mbali sana, halafu na kupanda kwa bei za vitu.

Ila kwa wakati huo huo mabadiliko ya teknolojia yaliendelea kurahisisha utengenezaji wa bidhaa na ushindani katika masoko ya ndani na kimataifa kupunguza bei za bidhaa, kiasi kwamba hakuna uhusiano kati ya kima cha chini na uwezo wa kujikimu.

Tatizo linakuja katika ukubwa wa familia na njia zao za kujikimu, au umbali, gharama za usafiri, chakula cha mchana, n.k. Kulipwa kima cha chini inahitaji mfanyakazi akae karibu, alipe pango kidogo tu, aishi.

Kinachomaliza umuhimu wa sikukuu ya wafanyakazi ni kupanuka duniani kote kwa ‘post-industrial state,’ yaani mfumo ambako viwanda vinakuwa vimepitwa na wakati, kwa maana kuwa ni watu wachache tu wanaofanya kazi katika viwanda ukilinganisha na jumla ya watu nchini.

Hata hapa nchini suluhisho la ajira ni kupunguza kodi, kupunguza matumizi ya serikali, kufuta deni la taifa na kuwezesha wawekezaji kutumia raslimali zilizopo kuweka vitega uchumi, kuajiri watu kwa kila aina ya huduma.

Idadi ya watu wanaoishi wakiuza mitumba (nguo za bei ya kutupa) kamwe haiwezi kuwezeshwa upya kwa kufuta mitumba halafu kuwaajiri katika viwanda vya nguo, n.k.

Kutokana na kazi kubadilika na kuwa za muda mfupi, mikataba, au kujishikiza tu hapa na pale kwa kufanya kazi nyumbani kupitia kompyuta pale inapotokea kazi ya kusaidia au kutoa ushauri, mshikamano wa wafanyakazi unakuwa ni jambo la zamani.

Kuna ushindani mkubwa nani anabaki kazini na nani anapunguzwa, na kupata watu mbadala endapo kunatokea mgomo siyo kazi, kwani wahitimu wengi wako barabarani hawana ajira.

Maisha ya kisasa ni rahisi zaidi kwani hayahitaji ajira kamili lakini yanaleta msongo wa mawazo kwani ajira ni utambulisho wa fani ya mtu na umuhimu wake kijamii; kazi za kujishikiza zinavuruga hitaji hili la kutambuliwa.

MEI MOSI



Moja ya silaha nzito katika medani za kivita. Utafiti unaonyesha kwamba matumizi ya kijeshi yaliongezeka mwaka 2018. **PICHA: MTANDAO**

# RIPOTI YA SIPRI: matumizi ya kijeshi yaongezeka duniani

MATUMIZI ya kijeshi duniani yamefikia kiwango chake cha juu mwaka jana katika muda wa miongo mitatu.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Amani ya Stockholm (SIPRI), kwa kiasi kikubwa, hali hii imesababishwa na mataifa ya Marekani na China.

SIPRIinakadiria kwamba matumizi ya dunia ya kijeshi yamefikia jumla ya dola za Marekani trilioni 1.8 kwa mwaka 2018, ikiwa ni juu kwa asilimia 2.6, ikilinganishwa na matumizi ya mwaka 2017.

Idadi hiyo inatafsirika kuwa ni sawa na dola 239 kwa mtu mmoja.

Marekani inabakia kuwa nchi ya kwanza duniani kwa matumizi makubwa ya kijeshi, ikitumia dola bilioni 649 kwa mwaka 2018.

Hilo ni ongezeko la asilimia 4 kwa kuangalia matumizi ya mwaka 2017.

“Ongezeko hilo katika matumizi ya Marekani, limesababishwa na utekelezaji wa mipango mipya ya ununuzi wa silaha chini ya utawala wa Rais Donald Trump wa Marekani,” anasema Aude Fleurant, Mkurugenzi wa Mipango wa SIPRI wa matumizi ya majeshi na ununuzi wa silaha.

Marekani imechangia jumla ya asilimia 36 ya matumizi yote ya dunia kwa mwaka 2018, na ilitumia karibu kiasi hicho kama jumla ya mataifa mengine manane yaliyofanya manunuzi ya juu, SIPRI inasema.

Hata hivyo, matumizi ya Marekani yalikuwa karibu moja ya tano chini kuliko matumizi yake ya juu kabisa yaliyofanyika mwaka 2010.

Matumizi ya nchi iliyoshika nafasi ya pili ambayo ni China, yalikadiriwa kuwa dola bilioni 250, ikiwa sawa na asilimia 14 ya matumizi yote ya dunia.

Matumizi hayo yalikuwa yameongezeka kwa asilimia 5 kwa mwaka 2018, ikiwakilisha ongezeko la chini kwa China kwa mwaka, tangu mwaka 1996 na linaakisi ukuaji wa taratibu wa uchumi.

Mataifa mengi yamenunua silaha ili kujihami na kuwa na silaha bora zaidi.

“Ongezeko la matumizi ya kijeshi kwa China linafuatia ukuaji wa jumla wa uchumi wa nchi hiyo,” mtafiti wa SIPRI, Nan Tian anasema.

Saudi Arabia imebaki katika nafasi ya tatu kwa kutumia dola bilioni 67.6, licha ya kupunguza matumizi ya asilimia 6 ikilinganishwa na mwaka wa 2017.

**SAUDI ARABIA INAFUATIWA NA INDIA, UFARANSA.**

Akizungumza na Sauti ya Ujerumani (DW) mkuu huyo wa kitengo cha utafiti katika SIPRI, Tian alisema hata hivyo kwamba, matumizi haya si mashindano ya silaha:

“Siwezi kusema ni mashindano ya silaha, lakini nchi hizi bila shaka zinaendelea kujihami kwa silaha mpya na zilizo bora, zenye uwezo mzuri zaidi… na silaha hizi mara nyingi ni ghali sana.”

Matumizi ya India yameongezeka kwa mwaka wa tano mfululizo na kwa kiasi kikubwa, hali hiyo ikisababishwa na hali ya wasiwasi dhidi ya China na Pakistan, kwa mujibu wa taasisi hiyo.

Mataifa matano ya juu ya watumiaji wakuu yamechangia asilimia 60 ya matumizi yote ya kijeshi duniani. Urusi imeporomoka hadi katika nafasi ya sita, ikitumia kiasi kinachokadiriwa kufikia dola bilioni 61.4.

Hii ni mara ya kwanza kwa Urusi kutokuwa miongoni mwa nchi tano za juu zenye matumizi makubwa tangu mwaka 2006.

SIPRI inaongeza kuwa matumizi ya Urusi hata hivyo bado yalikuwa juu kwa robo nzima ikilinganishwa na mwaka 2009.

Mataifa 10 ya juu yaliyotumia fedha nyingi kwa ajili ya jeshi ni pamoja na Uingereza, Ujerumani, Japan na Korea Kusini.

Kwa utaratibu wa jumla kwa mujibu wa SIPRI ni kwamba matumizi kwa ajili ya jeshi kama sehemu ya pato jumla la taifa, yamepungua katika kanda zote tangu mwaka 1999.

SIPRI inasema kwamba sita kati ya mataifa 10 ambayo matumizi ya jeshi yanakadiriwa kuchukua sehemu kubwa ya Pato Jumla la Taifa (GDP), ambayo pia yanaelezwa kuwa jeshi ni mzigo, yanapatikana katika Mashariki ya Kati.

Mataifa hayo ni pamoja na Saudi Arabia katika asilimia 8.8, Oman katika asilimia 8.2, na Israel katika asilimia 4.3.

SIPRI inasema kinashindwa kupata data kutoka mataifa kadhaa ikiwa ni pamoja na Syria, Umoja wa Falme za Kiarabu, Qatar na Yemen.

Lakini kwa mujibu wa data zilizopo, mzigo wa jeshi katika Mashariki ya Kati ni asilimia 4.4 ya pato jumla la taifa.

Barani Ulaya, mzigo wa jeshi uko katika wastani wa asilimia 1.6, kiasi kidogo chini ya Afrika na maeneo ya Asia na mataifa ya bahari ya Pacifiki. **DW**

MEI MOSI

# Guinea Bissau yachagua wabunge

## • Sasa yangoja uchaguzi wa urais 1966-1975

**Na Nimi Mweta**

NCHI ya Guinea Bissau katika pwani ya ncha ya Magharibi ya Afrika imemaliza uchaguzi wa wabunge mwezi Machi.

Sasa inangoja kupiga kura ya urais mwezi Juni, ikionyesha kushamiri kwa demokrasia baada ya miongo miwili ya mikasa, mapinduzi, serikali za muda mfupi na vipindi virefu vya utawala wa chama kimoja.

Ni kile cha ukombozi cha PAIGC (chama cha ukombozi wa Guinea Bissau na Cape Verde) ambacho bado ni chama kikubwa zaidi kikiwa na viti 41 bungeni kati ya viti 101.

Ni kielelezo cha nchi ikiparaganyika kutokana na biashara ya dawa za kulevya na kuonekana kama ni dola iliyoshindwa, halafu ijikusanye upya kupitia kura.

Jambo la kushangaza ni kuwa Guinea Bissau imepitia mazingira ya dola iliyoshindwa na kurudi katika demokrasia bila kuhitaji kufanya mkutano wa kitaifa wa kuunda katiba mpya, ila kufanya marekebisho ya katiba yake ya mwaka 1984.

Ni nchi ambayo ilitengwa na taifa pacha la Cape Verde, wakati chama cha PAIGC kilikuwa chama cha pamoja cha kupigania uhuru kutoka ukoloni wa Ureno, ikawa ndiyo nchi ya kwanza ya kundi hilo kupata uhuru baada ya utawala wa kifashisti kuanguka huko Ureno mwaka 1973.

Msumbiji na Angola zilifuata baadaye kidogo, mwaka 1975 licha ya kugubikwa na machafuko, hasa Angola, ikifikia uhuru.

Baadhi ya wachunguzi wa habari wanasema kuwa Guinea Bissau ilitumbukia katika janga la kuwa 'dola ya unga' kwa bahati mbaya wakati ndege ndogo ya kukodi iliyobeba kishehena cha 'unga' ilipoanguka porini.

Mtu mmoja akatoka na mzigo wa unga mweupe asijue hasa ni kitu gani, halafu wakagundua watu kadhaa akiingia mjini, wakampa vijisenti asimwambie mtu, wakabeba mzigo wote wakaanza kuuza.

Polisi walipogundua wakaanza pia kukatiwa 'chao,' na halafu wauza unga wa Colombia (bara la Amerika ya Kusini) wakapeleleza ndege hiyo ilivyoanguka na kilichotokea, wakaona wautumie mtandao huo mpya. Ikawa biashara kubwa, ikaliteka pia jeshi.

Sifa ya Guinea Bissau kuwa 'dola ya unga' ilipanuka katika anga za kimataifa mwezi Aprili 2013 wakati Marekani ilipomkamata José Américo Bubo Na Tchuto, aliyekuwa mkuu wa kamandi ya vikosi vya baharini vya nchi hiyo.

Alikuwa akisimamia usafirishaji wa dawa za kulevya kutoka Amerika ya Kusini kuja ncha ya Magharibi ya Afrika, halafu kutafuta vyombo vya kuipenyeza kupitia ukanda mrefu wa pwani ya Marekani.

Ujasusi wa Marekani ukagundua njia hiyo na kufuatilia wakitumia satelaiti angani, akaonekana akisimamia shughuli hiyo, na aliposafiri akaingia nchi nyingine akakamatwa kwa ombi la serikali ya Marekani kuwa wanamhitaji ajibu kesi.

Baadhi ya wachambuzi wamekuwa wakihoji kama dhana ya 'dola ya unga' inafaa kutumiwa kuhusu Guinea Bissau, wakisema kuwa 'dola ya unga' inatakiwa iwe ni nchi ambayo mamlaka zake rasmi zinakuwa zimepenywa na nguvu na fedha za biashara haramu.



Rais Jose Mario Vaz wa Guinea Bissau. **PICHA: MTANDAO**

> Afrika Kusini ni nchi nyingine yenye mtindo huo, na kwa jumla inaaminika kuwa ina ngazi pevu zaidi ya kidemokrasia kuliko nchi zilizobaki.

Dhana hiyo ilianza kutumika kuelezea nchi baada ya mapinduzi ya kijeshi ya Bolivia mwaka 1980 yakiongozwa na Luis Garcia Meza ambaye alionekana vianzio vyake vya fedha vinatoka kwa watengenezaji na wasafirishaji wa dawa za kulevya.

Pia wataalamu wanatofautisha aina kadhaa za 'dola za unga' kuendana na kiasi gani dola hiyo inakuwa imekamatwa na wasafirishaji, wasambazaji wa 'unga.'

Nchi kama Papua New Guinea na Iran katika miaka ya karibuni zimewekwa katika kundi la dola 'changa' za unga, kwani kiasi cha vijana milioni nne walikuwa tayari wanatumia dawa, au wameathirika kwa njia isiyojificha nchini Iran.

Ni taifa lenye sheria kali kuhusu masuala ya maadili, lakini ina mpaka mrefu na Afghanistan, nchi inayotawaliwa na wana siasa kali lakini imeparaganyika katika uthabiti wake kisiasa, sehemu tofauti za nchi zikidhibitiwa na mamlaka ambayo haitegemei serikali kuu, ila inajumuishwa ili mambo yaende bila vita kuanza kati ya utawala wa jimbo na serikali kuu. Ni katika hali hiyo ambako dawa zinazalishwa zaidi.

Nchi za 'Afghanistan, Guinea Bissau, Korea Kaskazini, Venezuela na Myanmar zilitajwa katika utafiti miaka ya karibuni kuwa ndizo 'zimeendelea' katika ukuaji wa 'dola ya unga,' na kati ya hizo inaelekea juhudi za kimataifa hasa zikiongozwa na Marekani na Umoja wa Ulaya (EU) zimefaulu zaidi Guinea Bissau.

Afghanistan bado iko katika lindi la vita, Korea ya Kaskazini ni ya kiimla na biashara ya unga ina dhamira ya kuingiza fedha za kigeni.

Venezuela imeparaganyika baada ya kuingia madarakani serikali ya kimapinduzi adui wa Marekani, fedha au mitaji ikaanza kuikimbia nchi na jinsi mazingira yalivyoanza kuvurugika, nidhamu ikapwaya, 'unga' ukashamiri.

Cha kushangaza ni kuwa ukiangalia kwa kigezo cha utegemezi wa dola kwa biashara ya dawa za kulevya, hakuna hata moja kati ya nchi tano 'zilizoendelea' kwa biashara hiyo haramu kujikita katika uchumi na utawala wa jumla ni Guinea Bissau iliongoza.

Kiasi cha vijana wake walioathirika na dawa kilikuwa kikubwa kuliko kwingine kwa makisio, lakini baadhi ya wanaharakati walioanza kuona nchi hiyo itabanwa mbavu katika tafiti hizo kwa sababu ni ya Kiafrika, wakaanza kutaka matumizi ya 'dola ya unga' yaelekee katika nchi ambazo ni dola yenyewe inasimamia shughuli hiyo na siyo watu wanaokula rushwa kutokuwakamata 'wauza unga.'

Ni mlengo wa uhakiki unaofanya Uingereza iwe ndiyo 'dola unga' ya kwanza duniani, kwani iliutumia kama silaha zamani.

Kukamatwa kwa ofisa wa ngazi za juu wa jeshi la Guinea Bissau na kufikishwa katika mahakama nchini Marekani mwaka 2013 kulichochea mabadiliko kasi fulani nchini humo, na kuanza kuondoa 'mduara' wa serikali za mpito na mapinduzi ya kijeshi.

Ni katika hali hiyo ambako kiongozi wa sasa pamoja na wabunge walichaguliwa kwa kipindi cha miaka mitano, na hivyo uchaguzi wa rais unatazamiwa kufanyika mwezi Juni na Jose Mario Vaz aliyeko madarakani ana nafasi kuendelea kutawala.

Katika uchaguzi wa Bunge mwezi Machi, chama cha miaka mingi kimepoteza mvuto kiasi lakini bado ndiyo kina wabunge wengi, na kinaweza kutoa nafasi ya ushirikiano na chama cha mrengo wa ujamaa (PAIGC kwa jadi ni ya kimapinduzi) ili kuunda serikali.

Cha kushangaza pia ni kuwa licha ya kuwa demokrasia ya Guinea Bissau ni changa inafanana sana na Israel ambayo majuzi imefanya uchaguzi wa Bunge ambako chama cha Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu (Likud, uhafidhina) kilipata viti 35 na washindani wao wa 'nyeupe na bluu' viti 256 vile vile, lakini Likud wana uwezo wa kushirikiana na vyama vingine vya kihafidhina au kidini, iunde serikali. Inaelekea pia kuwa tatizo la dawa za kulevya limegawa jamii katika matabaka ya kimaisha na mwelekeo wa kisiasa ambao siyo tena wa kimajimbo, hivyo kuwezesha mpangilio wa kupiga kura za vyama na siyo kwa kutanguliza mgombea wa eneo, mfumo wa uwakilishi wa uwiano (proportional representation).

Afrika Kusini ni nchi nyingine yenye mtindo huo, na kwa jumla inaaminika kuwa ina ngazi pevu zaidi ya kidemokrasia kuliko nchi zilizobaki.

Hivyo ni hatua kubwa kwa Guinea Bissau kujizatiti na kuweka mazingira ya demokrasia halisi, ingawa bado 'unga' haujaondolewa mitaani.

MEI MOSI

# Burundi inavyohaha kujiunga SADC

Na Mwandishi Wetu

JE, Burundi inataka kuyakimbia au kupunguza ushiriki wake katika matatizo na migogoro ya kidiplomasia inayoikabili kanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)?

Ama inataka kutanua wigo wa manufaa ya kiuchumi yanayotokana na ushirikiano wa kikanda?

Hivi sasa Burundi inasukuma nia yake ya kutaka kujiunga ili kuwa nchi mwanachama wa 16 wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Tayari taifa hilo lenye eneo dogo la kijiografia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), limewalika wataalamu wa SADC kuitembelea na kutathmini utayari wake wa kujiunga huko ili kutoa taarifa kwenye mkutano wa wakuu wa nchi wanachama kadri ya taratibu zinavyohitajika.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Burundi, Ezechiel Nibigira, hivi karibuni alimtembelea Mwenyekiti wa SADC ambaye pia ni Rais wa Namibia, Hage Geingob, akimhakikishia kuwa nchi yake ipo tayari kuwapokea wataalamu hao Mei mwaka huu.

Mwaka 2017, Burundi na Comoros ziliomba uanachama wa SADC, lakini baada ya 'kuchunguzwa', maombi ya Burundi yaliwekwa kando wakati yale ya Comoro yalikubaliwa na kuvifanya visiwa hivyo kuwa mwanachama wa 16 wa SADC.

Nibigira akasema nchi hiyo imeongeza kiwango cha utulivu tangu mwaka 2015, ilipokumbwa na machafuko ya kisiasa yaliyosababisha vifo vya takribani watu 1,000 na kuwaacha mamia kadhaa wakikosa makazi.

Maombi ya Burundi ya mwaka 2017 yalitathiminiwa kwanza na Kamati ya Siasa na Diplomasia ya SADC inayohusika na mambo ya siasa, ulinzi na usalama.

Baraza la mawaziri la SADC lilikutana Februari 2017 na kuiweka kando Burundi kwa madai kwamba haina utulivu wa kisiasa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 8(2) cha Mkataba wa kuanzishwa SADC, kujiunga kwa nchi mwanachama kunaweza kuathiriwa na makubaliano ya pamoja ya mkutano wa wakuu wa nchi za jumuiya hiyo.

Mwaka 2003, baada ya mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam, nchi wanachama wa SADC zilipitisha sifa mpya ya kujiunga mwanachama mpya.

Sifa hizo zinajumuisha hali ya kanuni za demokrasia, haki za binadamu, utawala bora na utawala wa sheria, kwa mujibu wa tamko la Umoja wa Afrika (AU) kuhusu haki za binadamu na watu.

Kama maombi yake yatakubaliwa, Burundi itakuwa nchi ya pili katika ukanda wa EAC kujiunga SADC. Nchi pekee ya EAC iliyopo SADC ni Tanzania.

Lakini wachunguzi wengine wa masuala ya ushirikiano wa kikanda wanasema maombi ya Burundi kwa SADC yanachagizwa na uhusisano mbovu wa kidiplomasia uliopo dhidi ya `jirani yake wa damu' Rwanda na wakati mwingine Uganda.

Ingawa Burundi ina kiu ya kujiunga SADC lakini uwezo wa kiuchumi wa taifa hilo kuchangia michango ya wanachama unaweza kuitatiza.



Rais Pierre Nkurunziza wa Burundi. **PICHA: MTANDAO**

> Mwaka 2003, baada ya mkutano uliofanyika jijini Dar es Salaam, nchi wanachama wa SADC zilipitisha sifa mpya ya kujiunga mwanachama mpya.

Kwa mfano takwimu zinaonyesha kwamba katika uanachama wake kwa EAC pekee, Burundi inadaiwa zaidi ya Dola milioni 10 za Marekani.

Wataalamu hao wa SADC walipangiwa kuitembelea Burundi mwaka jana ili kufanya tathmini ya maombi yake lakini serikali ya Rais Pierre Nkurunziza iliomba kuahirishwa kwa ziara hiyo kwa vile walikuwa katika mchakato wa Katiba mpya.

Kwa upande mwingine, gazeti la Obsever la Uganda liliripoti kwamba jitahada za Burundi kuusaka uanachama wa SADC zilimfikisha Nibigira nchini Zimbabwe hivi karibuni na kukutana na Rais Emmerson Mnangagwa.

Alipokutana na Rais Mnangagwa, Nibigira, akimwakilisha Rais Nkurunziza, aliwaambia waandishi wa habari kwenye Ikulu ya Harare kwamba Burundi inatafuta kuungwa mkono na taifa hilo (Zimbabwe) ili kujiunga SADC.

"Zimbabwe ni nchi dada kwetu sisi, ni nchi ambayo tuna uhusiano nayo wa kihistoria na mweleekeo unaofanana ndio maana tunataka kujihusisha na nchi hii kwa namna ya pekee," akasema.

Anaongeza, "kama mnavyojua Burundi imeomba kujiunga SADC na maombi yetu yapo katika hatua nzuri...tunaamini kwamba baada ya kutathiminiwa na wataalamu wanaotarajiwa kuja Burundi mwishoni mwa Mei, tunaamini uamuzi utatuwezesha kuwa mwanachama na kwamba Zimbabwe itazidi kutuunga mkono."

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje nchini Zimbabwe, Kindness Paradza, akasema Zimbabwe inaunga mkono jitihada hizo za Burundi.

Akasema kukubaliwa kwa Burundi kuwa mwanachama wa SADC kutasaidia kurahisisha biashara kati ya nchi hizo kama ilivyo katika Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) ambako mataifa hayo mawili ni wanachama.

"Burundi ni sehemu ya COMESA kama ilivyo Zimbabwe ambayo hivi karibuni Bunge la nchi hiyo liliridhia tamko la eneo huru la kibiashara barani Afrika, hivyo tunaondoa vikwazo vyote vya kibiashara ndani ya bara letu na itakuwa vema kama viongozi wetu wa SADC wataikubali Burundi ambao ni ndugu zetu," akasema Paradza.

Hata hivyo, si Wazimbabwe wote wanaodaiwa kuunga mkono nia hiyo ya Burundi kujiunga SADC ama nchi hiyo kuisadia (Burundi) katika nia yake.

Miongoni mwa wanaoipinga Burundi ni Mkurugenzi wa taasisi ya Human Rights Watch, Dewa Mavhinga, anayeielezea nchi hiyo kuwa yenye viwango duni vya haki za binadamu.

Kwamba uamuzi wa kuibadili Katiba ya mwaka 2015 uliomuwezesha Rais Nkurunziza kuwania urais kwa kipindi cha tatu, ulisababisha machafuko na mauaji nchini humo.

Mavhinga anasema SADC inapaswa kupima kwa uzito rekodi ya ukiukwaji haki za binadamu ya Burundi, kabla ya kufikia uamuzi wa kuikubali kuwa mwanachama.

"Kuna matatizo makubwa yanayotokea nchini Burundi yakihusiana pia na ukiukwaji wa haki za binadamu na hilo ndilo linaloilazimisha (Burundi) kutuma ujumbe wao Zimbabwe kuisaidia kujiunga SADC," anasema Mavhinga.

Lakini Paradza anasema shutuma za ukiukwaji wa haki za binadamu zinazoelekezwa kwa Burundi zinapaswa kutolewa na AU.

"Burundi ni sehemu ya AU na COMESA, kama kuna jambo baya linaloathiri haki za binadamu linapaswa kushughulikiwa na AU. Inajulikana kwamba hata katika AU kuna tume ya haki za binadamu, sasa nadhani tusichanganye mambo," anasema Paradza

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Maoni 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com***

MEI MOSI

# Giza nene Kushner akimaliza kazi mpango amani Mashariki ya Kati



Mkwe wa Rais Donald Trump wa Marekani, Jared Kushner (katikati), akiwa na Rais Trump (kushoto) na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

NCHI ya Peru katika bara la Amerika ya Kusini ilitangaza siku tatu za maombolezo ya kitaifa kutokana na kifo cha rais mstaafu Alan Garcia, aliyekuwa na umri wa miaka 69 wakati alipokufa kwa kujipiga risasi.

Taarifa zilisema kuwa polisi walikuwa wanaelekea nyumbani kwake kumkamata ili afunguliwe kesi mahakamani kwa madai ya rushwa.

Kwa wengi kati ya raia wa nchi hiyo Alan Garcia hakuwa mtu wa kawaida, kwani alionyesha kipaji cha siasa akiwa bado mtoto, akatoa hotuba ya kusisimua kumsifu mwanzilishi wa chama cha Aprista ambacho kilimfikisha madarakani baadaye. Alitawala katika vipindi tofauti, kwanza Julai 1985 hadi Julai 1990 halafu Julai 2006 hadi Julai 2011, kuonyesha kuwa hakuwahi kuchuja katika siasa za Peru, akichaguliwa angali bado kijana.

Kuelewa mazingira ya rais huyo mstaafu kufikia uamuzi huo labda siyo suala gumu kisaikolojia, kuwa hakutaka kuingia katika mazingira ya aibu, lakini kwa vile siyo jambo la ajabu kwa wanasiasa kutuhumiwa kwa rushwa, inawezekana yako maeneo mengine yaliyomtia uchungu, si tuhuma peke yake.

Kwa upande mwingine, nchi aliyoiongoza siyo maskini hata kidogo, kwani kwa takwimu za Benki ya Dunia uchumi wa nchi hiyo ni wa 39 kwa ukubwa duniani, na kipato chake cha wastani ni cha kati ya ngazi za juu, zaidi ya dola za Marekani 12,000 kwa kila mwananchi.

Kimsingi imefuata misingi ya kiliberali ya uchumi ila kuna misuguano hivyo kunakuwapo vipindi tofauti vya mwelekeo wa utawala, vya kutetea uchumi wa ndani (haki za wafanyakazi, kampuni za ndani) na vipindi vya uhafidhina (soko huria, haki ya kila mjasiriamali, wa ndani au nje). Garcia alikuwa kundi la kwanza.

> Mwezi Novemba mwaka jana mahakama ilimzuia kusafiri nje kutokana na kashfa ya Odebrecht iliyokuwa inaendelea kuchunguzwa.

Akiwa kijana, Garcia alisoma sheria katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Peru, na akapata shahada katika Chuo Kikuu cha San Marcos (Mtakatifu Marko) mwaka 1971.

Aliondoka Peru kwenda Hispania kusoma shahada ya juu (uzamivu) ambayo alisema aliipata lakini ushahidi wa baadaye unaashiria kuwa hakumaliza masomo hayo (sababu mojawapo ni kuwa alikuwa mwanamapinduzi, na enzi hizo Hispania inaongozwa na Jeneralissimo Francisco Franco, mtawala wa kiimla asiyetaka harufu ya mapinduzi hata kwa kilomita moja.

Garcia aliendа Ufaransa ambako nyakati hizi fikra za kimapinduzi zilikuwa zinashamiri, akasoma katika chuo kikuu cha Pantheon Sorbonne, moja ya vyuo vikuu vikongwe na vyenye sifa za hali ya juu nchini Ufaransa.

Licha ya kuwa Garcia alikuwa kimsingi ni mwanamapinduzi, aliposhika usukani wa madaraka lengo lake halikuwa ni kuondoa mfumo wa kibepari au 'ukoloni mamboleo' kama wanaharakati wanavyoita bali kuingiza mabadiliko katika mifumo ya kodi na matunizi ya fedha za serikali, kutatua changamoto zinazowakabili wananchi walio wengi.

Takwimu za Benki ya Dunia (WB) zinaonyesha kuwa umaskini nchini Peru ulipungua kwa kasi kubwa, kutoka asilimia takriban 60 ya wananchi wote mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 25.8 mwaka 2012.

Ni takwimu za mwaka uliotanguliwa Garcia kutwaa madaraka kwa mara ya pili, na mwaka uliofuata alipoondoka.

Vipindi vyake vya utawala nchini humo vilitofautiana sana, kwani kipindi cha kwanza, mwaka 1985 hadi 1990 kiligubikwa na hali ngumu ya uchumi (enzi ambako mfumo wa fedha bara la Amerika ya Kusini uliparaganyika kutokana na mabadiliko ya thamani katika uchumi wa dunia, kufanya madeni yao yasilipike).

Hata hivyo, jina lake lilibaki katika midomo ya wananchi wa Peru baada ya kutoka madarakani, na mwaka 2001 akashindwa katika duru ya pili ya uchaguzi wa rais, nyuma ya mhafidhina Alejandro Toledo. Miaka mitano baadaye akawa ndiyo 'shushu' wa wapiga kura hasa wa hali ya kawaida akaingia madarakani, lakini kipindi hiki kilikuwa kigumu kwake kutokana na mifarakano hasa na watu wa makabila ya jadi kutaka maeneo yao yasiguswe na 'wakuja.'

Pia kulikuwa na tatizo la rushwa ambalo viongozi wengi wanaharakati wanajaribu kupambana nalo lakini wa jumla wanakwama, kwani siasa inategemea sana kuchangiwa na watu wenye ushawishi katika maeneo tofauti ya uchumi na jamii.

Wana maslahi halisi wanayotazamia kuwa anayeingia madarakani kwa ridhaa au misaada na wawezeshaji wao atayafanyia kazi, na akichukua hatua hizo siyo ajabu ipatikane njia ya kumhusisha kutumikia 'wenye mali,' kama aliyokuwa akisema Mwalimu Nyerere katika maongezi na waandishi wa habari mwaka 1995.

Ni katika kufuatilia sera za kiliberali na mkazo katika kodi ambako alikuwa upande wa wawekezaji katika mzozo na wenyeji wa maeneo tofauti, na hivyo kulauimiwa kufumbia macho matukio ya uvunjaji wa haki za binadamu.

Garcia alikuwa mshiriki wa siasa za uadui na urafiki kati ya wanamapinduzi na wahafidhina katika bara hilo, ambalo alikuwa na uelewano mzuri na rais mwanaharakati wa Brazil, Luiz Ignacia Lula da Silva, ambaye sasa anatumikia kifungo cha miaka 12 kwa madai ya rushwa.

Garcia alijaribu tena kugombea mwaka 2016 akapata asilimia 5.8 ya kura mzunguko wa kwanza, hivyo akafikia tamati yake kisiasa.

Vyombo vya habari nchini Peru viliripoti kuwa mwezi Mei 2012, akiwa ameondoka madarakani, alipewa dola 100,000 kutoa hotuba kwa viongozi wa kibiashara nchini Brazil, huko Sao Paulo, ambayo baadaye vyombo vya habari vikasema ni milungula kutoka kwa kampuni ya ujenzi ya Brazil, Odebrecht.

Mzunguko huo wa tuhuma umeendelea hadi majuzi ambako polisi walitumwa nyumbani kwake kwenda kumkamata, akajiua kwa risasi kabla ya kuingizwa hali ya ufungwa.

Mwaka 2016 na 2017 mawaziri wake watano wa zamani walifunguliwa mashtaka ya rushwa na mfumo wa sheria wa nchi hiyo, ambako hakimu jaji ndiye anaitisha uchunguzi ili afungue kesi, na siyo lazima polisi au mamlaka nyingine ifikishe kesi kama hiyo mahakamani.

Mawaziri hao ni Yehude Simon (aliyekuwa waziri mkuu), Rosario Fernandez (sheria), Mercedezs Cabanillas (mambo ya ndani), Antero Flores Araoz (ulinzi) na Luis Nava (uzalishaji).

Mwezi Novemba mwaka jana mahakama ilimzuia kusafiri nje kutokana na kashfa ya Odebrecht iliyokuwa inaendelea kuchunguzwa.

Aliingia maskani ya balozi wa Uruguay jijini Lima hapo Novemba 17 mwaka jana lakini ombi lake la hifadhi ya kisiasa lilikataliwa.

Ni kashfa ambayo imelazimu kukamatwa marais wa zamani wa Peru walio hai waliokuwa madarakani kuanzia mwaka 2000 ambao ni Alejandro Toledo, Ollanta Humala na Pedro Kucyzynski.

Ni hali aliyoshindwa kuizoea akajiua April 17.

Ni mazingira ambayo bado yanaleta mijadala miongoni mwa wanaharakati na wasomi wa masuala ya katiba, suala la kuwapo katiba inayowezesha nusu ya serikali iliyotangulia kukamatwa kwa madai ya rushwa, na katika hili la Peru, marais wastaafu watatu waliotawala tangu 2000 wote wanakamatwa kuhusiana na rushwa.

Badala ya kuwa kielelezo cha kuenea kwa rushwa nchini Peru inakuwa ni kielelezo cha udhaifu wa katiba na mifumo ya sheria, hasa kutokana na kanuni ya kimapinduzi ya hakimu au jaji kuidhinisha mashtaka, na siyo lazima yatoke chombo rasmi kinachoweza kuendesha mashtaka ya jinai, kama polisi au idara ya upelelezi, tume ya rushwa, n.k.

Kwa njia hiyo mahakama zinakuwa ni washikadau wa siasa, kufungua kesi kwa kuangalia wasichokitaka.



## Maji yatesa wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa kike wanaoishi bwenini katika Shule ya Sekondari ya Usongwe Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wanalazimika kwenda kuomba maji kwenye makazi ya watu mitaani kutokana na shule hiyo kukabiliwa na uhaba mkubwa wa maji.

Wakizungumza na Nipashe, wanafunzi hao walisema hulazimika kutoka kwenda vijijini kwenye makazi ya watu kusaka maji kwa ajili ya matumizi yao kama kuoga, kufua na kutumia vyooni kutokana na maji yaliyopo kutokukidhi mahitaji yao.

Zuela Ramadhani, mwanafunzi wa kidato cha sita, alisema hali hiyo imekuwa na athari kubwa kwao kwa vile wakati mwingine husababisha kukosa vipindi darasani na kuchelewa kupata chakula.

"Tulikuwa tunakosa hata maji ya kuoga, muda mwingine hata maji ya kunywa, tunalazimika kutoka kwenda huko vijijini kutafuta maji tunachelewa muda wa kula na kusababisha kukosa baadhi ya vipindi darasani na kusababisha tufanye vibaya katika masomo yetu," alisema Zuela.

Hata hivyo katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeanza kuchimba kisima kirefu shuleni hapo ili kukabiliana na changamoto hiyo. Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema shule hiyo yenye wanafunzi zaidi ya 2,000 ina mahitaji makubwa ya maji kiasi kwamba maji yanayotolewa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya hayakidhi mahitaji.

Alisema baada ya kufikishiwa kero ya wanafunzi hao, aliwasiliana moja kwa moja na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbalawa, ambaye bila kuchelewa aliamua kuifanyia kazi. Njeza aliishukuru Serikali kwa kuchukua hatua za haraka za kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuamua kuanza kuchimba kisima kirefu shuleni hapo ili wanafunzi wawe na uhakika wa upatikanaji wa maji muda wote.

Njeza alisema kisima hicho ni mkombozi mkubwa kwa shule hiyo yenye wanafunzi wengi na pia kitasaidia na wanafunzi wa shule za jirani ambao pia wanakabiliwa na kero ya upatikanaji wa maji.

Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Benedict Mahenge, aliishukuru serikali kwa kuwachimbia kisima hicho kwa madai kuwa kitasaidia kutatua changamoto zote za maji zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi hao.

# JPM aeleza nia ya serikali kuboresha afya

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

RAIS John Magufuli amesema Serikali imeongeza bajeti ya dawa kwa ajili ya hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini kutoka Sh. bilioni 31 mpaka bilioni 270 ili kuwawezesha Watanzania kupata huduma bora za afya.

Alitoa kauli hiyo juzi wilayani Kyela alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Ipinda ukiwa mwendelezo wa ziara yake ya siku nane mkoani hapa ambapo alisema lengo la Serikali ni kuhakikisha inaboresha huduma za afya.

Alisema pamoja na ongezeko hilo la bajeti, Serikali inaendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati katika maeneo mbalimbali ili kusogeza huduma karibu na makazi ya wananchi ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu.

Rais Magufuli alisema mpaka sasa Serikali imejenga vituo vya afya 352 nchi nzima na kwamba Mkoa wa Mbeya pekee umepata vituo 14 ambavyo vimegharimu zaidi ya Sh. bilioni sita na hospitali tatu za wilaya.

Alisema moja ya vituo vya afya vilivyojengwa katika Mkoa wa Mbeya ni cha Kata ya Ipinda ambacho ni miongoni mwa vituo bora, na kwamba pia Serikali inatarajia kutoa fedha kwa ajili ya dawa na vifaa tiba pamoja na kuajiri madaktari na wahudumu wengine.

"Namuagiza Waziri wa Tamisemi yupo hapa, ashughulikie suala la dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kituo hiki na vituo vingine, tunataka hata upasuaji mdogo mdogo ufanyike katika kituo hiki, sio mtu anasumbuliwa na busha anaanza kwenda hospitali ya wilaya.

Awali Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema Kituo cha Afya cha Ipinda ni kituo bora na cha mfano kwa taifa zima.

Alisema Serikali ilishatoa maelekezo kwa Halmashauri mbalimbali nchini kwenda kutembelea kituo hicho na kujifunza ili zinapotekeleza miradi kama hiyo ikitumie kama mfano.

Waziri Jafo alisema Kituo hicho kilijengwa na wananchi wenyewe wa Kata ya Ipinda kupitia mfumo wa Akaunti ya dharura, na Serikali ilitoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi huo.

"Mheshimiwa Rais, tunashukuru kwa namna unavyowajali Watanzania katika kituo hiki ulitoa shilingi milioni 500, lakini wananchi wa Kata hii walijitolea nguvu zao na kukamilisha ujenzi na kituo ni bora mno, sasa hivi kilichobakia ni vitu vidogo vidogo ambavyo pia tutakamilisha," alisema Jafo.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Dk. Harrison Mwakyembe, aliishukuru Serikali kwa kuwajali wananchi wa wilaya hiyo na kuwapelekea miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya huduma za afya na barabara.

Mwakyembe ambaye pia ni Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, alisema mbali na Serikali kujenga Kituo cha Afya cha Ipinda, pia wananchi wa Kyela wanaomba kukarabatiwa Hospitali ya Wilaya ambayo alidai imechakaa.

Vilevile, aliishukuru Serikali kwa kujenga Barabara ya Kikusya- Ipinda Matema ambayo ilizinduliwa na Rais Magufuli kwa kiwango cha lami kwa madai imesaidia kupunguza changamoto ya usafiri na usafirishaji katika eneo hilo.

Alisema kabla ya barabara hiyo kujengwa kwa kiwango cha lami, wananchi walikuwa wanatumia zaidi ya saa sita kusafiri, lakini sasa wanatumia nusu saa pekee na hivyo imechochea shughuli za maendeleo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (kulia), akikabidhi Tuzo na Cheti kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Masha Mshomba, wakati wa ufunguzi rasmi wa maonesho ya Usalama na Afya mahala pa kazi jijini Mbeya. WCF imekuwa mshindi wa kwanza katika masuala ya afya na usalama kazini baina ya taasisi za bima na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Siku saba mkandarasi kutekeleza mradi maji

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, amemwagiza Mkandarasi Kampuni ya Leostart Engineering Company anayetekeleza mradi wa Maji wa Kapapa uliopo katika Kijiji cha Kapapa Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya kukamilisha mradi huo ndani ya siku saba.

Waziri Mbarawa alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kukagua mradi huo ambao unatarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wananchi 31,000 wa vijiji nane vya Wilaya ya Kyela ambapo alisema mradi huo umesuasua kwa muda mrefu na kuanza kuwakatisha tamaa wananchi.

Alisema kutokana na maelezo ya mkandarasi huyo kwamba kilichobaki ni kutandaza mabomba, ndio maana aliamua kuagiza kazi hiyo ifanyike ndani ya siku saba kwa madai hiyo kazi ni rahisi tofauti na zingine zilizokwishakamilika.

"Mradi huu ulianza kujengwa mwaka 2014 na sasa huu ni mwaka wa tano bado haujakamilika, sasa taarifa za mkandarasi ni kwamba atakamilisha mradi mwezi juni, kazi ya kutandaza mabomba haiwezi kuchukua zaidi ya siku saba kwahiyo nataka badala ya Juni akamilishe ndani ya siku saba," alisema Prof. Mbarawa.

Meneja Ufundi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA), Ndele Mengo, alisema mradi huo umechelewa kukamilika kwa sababu ulikosewa mara ya kwanza kwenye hatua ya usanifu hali iliyopelekea chanzo kujengwa sehemu ambayo sio sahihi.

Alisema wakati huo ulikuwa unasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na baada ya kubaini makosa waliamua kumtimua mkandarasi aliyekuwa anajenga na kisha kuukabidhi kwa Mbeya- WSSA na mkandarasi akatafutwa mwingine ambaye ndiye anajenga mpaka sasa.


Mengo alisema baada ya kubadili mkandarasi walifanya upembuzi upya na kukihamisha chanzo kutoka kilipokuwa awali na kukishusha kidogo ili kiendane na mazingira ya eneo husika.

"Mradi huu unagharimu Sh. bilioni 3.8 na kwa utafiti uliofanyika ni kwamba una uwezo wa kuhudumia watu wasiopungua 31,000 hivyo tuaamini kuwa utasaidia kupunguza tatizo la huduma hii kwa wananchi wa Kyela," alisema Mengo.

Alisema wamekuwa wakimsimamia kwa ukaribu mkandarasi huyo ili kuhakikisha anakamilisha kwa wakati mradi huo na wananchi wanaanza kunufaika huku akidai kuwa mradi unatekelezwa kwa kiwango kizuri.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kyela waliipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huo pamoja na miradi mingine kwa madai kuwa itawasaidia kuondokana na adha ya maji inayowakabili kwa sasa.

Obed Mwalusamba alisema mradi huo ukikamilika utakuwa





# Mikoa mitano yapuliziwa dawa kuua viluilui vya mbu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAYA 500,000 nchini zimepuliziwa dawa kwa ajili ya kuuwa viluwiluwi vya mbu wanaosababisha ugonjwa wa malaria.

Mikoa ambayo imepuliziwa dawa hiyo ni Kagera, Geita, Kigoma, Lindi na Mtwara.

Akizungumza jijini hapa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema zoezi hilo limefanyika katika mikoa hiyo kuhakikisha malaria inatokomezwa.

Alisema ziro ya malaria inaanzia nyumbani kwa kila Mtanzania hivyo kila mmoja anapaswa kutambua umuhimu wa kujikinga.

Alifafanua kuwa lengo ni kuona vifo vitokanavyo na malaria vinapungua kwa asilimia kubwa.

Alisema Mkoa wa Dodoma umefanikiwa kupunguza maambukizi ya malaria kutoka asilimia moja hadi kufijia 0.6.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa halmashauri zote nchini zinatakiwa kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kununua viuawadudu ikiwa ni katika kupambana na maambukizi ya malaria katika maeneo yao.

Mwalimu alisema kwa kipindi cha miaka miwili ya utawala wa Rais Magufuli, Tanzania imepunguza maambukizi ya malaria kwa asilimia 50 kutoka wastani wa asilimia 14 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia saba.

Alisema serikali imekuwa na mikakati mingi ya kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa kugawa vyandarua pia wanapulizia dawa katika mikoa yenye kiwango kikubwa cha maambukizi.

Mwalimu alisema mkakati wa serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2020 angalau wajawazito 80 kati ya 100 waweze kuhudhuria kliniki angalau mara nne hivyo kutoa fursa ya kufanyiwa vipimo mbalimbali ikiwamo malaria.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa na ambaye ni Mratibu wa malaria mkoa wa Dodoma, Francis Bujiku, alisema Mkoa wa Dodoma umepunguza maambukizi ya ugonjwa huo kutoka asilimia moja mwaka 2015 hadi kufika asilima 0.6, ikiwa Mpwapwa ina asilimia 1.3 huku Chamwino ni asilimia 0.4.

# Wamlilia mbunge wao kupatiwa maji

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

WAKAZI wa vijiji vya Godegode na Pwaga, wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, wamemlalamikia Mbuge wa Viti Maalum, Mariam Ditopile, kutokana na kukabiliwa na kero ya kukosa huduma ya maji kwa muda mrefu hali inayo sababisha shughuli za uzalishaji mali kudhorota.

Mbunge huyo amewataka wakazi hao kuwa wavumilivu wakati serikali inaendelea kukabiliana na tatizo la ukosefu wa maji kama ilivyoahidi.

Mbunge huyo akiwa katika mwendelezo wa ziara ya kamati ya utekelezaji ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mkoa wa Dodoma ya kutembelea tarafa zote zilizopo mkoani hapa, alisema serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015/2020 iliahidi kumtua mama ndoo kichwani kwa kufikisha huduma hiyo karibu na wananchi jambo ambalo linaendelea kutekelezwa.

"Kilio chenu nimekisikia nawaomba muwe wavumilivu wakati suala hili linashughulikiwa, niwaahidi nitahakikisha nashirikiana na uongozi wa ngazi za juu akiwamo Waziri wa Wizara ya Maji ili kutatua changamoto hii kwa haraka," alisisitiza mbunge huyo.

Pia aliwataka wananchi hao kuendelea kuchapa kazi kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji hicho ili kuleta maendeleo kwa haraka kwa kuwa hakuna mafanikio yanayopatikana kirahisi.

Awali mmoja wa wananchi hao, Pili Machela, mkazi wa kijiji cha Godegode, alisema wamekuwa wakipata shida kutafuta maji kwa muda mrefu na kuiomba serikali iwaboreshee miundombinu yake.

"Tatizo hili limekuwa sugu na husababisha shughuli zingine kushindwa kuendelea, tunaomba upokee kilio chetu," aliomba mwananchi huyo.

Pamoja na changamoto hiyo alibainisha pia ukosefu wa kituo cha afya katika vijijini hivyo hali inayosababisha wagonjwa kwenda kutibiwa katika kituo cha afya cha Mpwapwa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa UVCCM mkoani Dodoma, Bill Chidabwa, alisema kutokana na Rais John Magufuli kuhamishia makao makuu ya serikali Dodoma, vijana wote wanatakiwa kuchangamkia fursa zilizopo ili kuweza kuleta maendeleo yenye tija katika mkoa na taifa kwa ujumla.

Aliwataka vijana kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika kujenga taifa lenye usawa kwa kila mtu na kuongeza kuwa hakuna mwenye hati miliki ya uongozi.

"Kuna kasumba sasa hivi imetokea mtu akigombea eneo fulani basi yeye ni adui hapana msifanye hivyo, chama hiki kimebadilika, ni cha wanyonge,' 'alisema Chidabwa.

Mariam alitoa mifuko 10 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo katika Shule ya Sekondari Godegode na kutoa ahadi ya madawati 20 katika shule hiyo na bandari moja ya mabati ili kusaidia kuendeleza ujenzi wa Shule ya Msingi Maswaga .



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Serikali Mtandao, Dk. Jabiri Bakari (kulia), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, wakati wa kutoa taarifa ya utendaji wa ofisi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ERMS kuunganisha taasisi katika mfumo mmoja

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Serikali Mtandao nchini, umebuni mfumo shirikishi wa kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS), ambao unaunganisha shughuli mbalimbali za taasisi kuwa katika mfumo mmoja ambao utawezesha kufuatilia, kusimamia ukaguzi na tathimini ya utekelezaji kwa ufanisi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Serikali Mtandao, Dk. Jabiri Bakari, alisema wameamua kutengeneza mfumo wa ERMS ambao ni dirisha moja linalounganisha shughuli zote ndani ya taasisi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma bora kwa umma.

Dk. Bakari alisema ERMS ina moduli 18, zinazounganisha shughuli mbalimbali za utendaji kazi ambazo zinategemeana na kuwezesha kubadilishana taarifa miongoni mwa idara, vitengo na kusimamia rasilimali kama vile watu fedha na vitendea kazi.

Alifafanua zaidi kuwa mfumo huo pia unawezesha ushughulikiaji wa miamala kutoka Idara moja hadi nyingine kama vile ankara za bidhaa na huduma, mapato na majukumu ya watumishi ikiwamo ufuatiliaji wa miradi.

"Inaweza kutoa pia hali ya matumizi ya fedha, taarifa zinazosaidia katika upimaji wa utendaji wa watumishi katika utoaji wa matumizi sahihi," alisema Dk. Bakari.

Alifafanua kuwa ERMS inaweza kuunganishwa na kubadilishwa taarifa za mifumo mingine mikuu ya serikali kama vile uhasibu, usimamizi wa taarifa za rasilimaliwatu, malipo ya serikali ya kielektroniki, barua pepe serikalini na ofisi mtandao.


Akieleza mifumo mingine iliyotengenezwa na wakala katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao nchini, alisema ni pamoja na kuhusishwa kwa iliyokuwa tovuti ya serikali na kuwa tovuti kuu ya serikali.

Alisema kutokana na hilo hivi sasa kazi za mtandao zitakuwa zikifanyika kwa ufasaha zaidi ikiwamo kwa ufanisi kutokana na kurahisishwa.

Dk. Bakari alisema baada ya kubuni mfumo huo kila kitu kitakwenda sawa katika utendaji kazi wa mtandao kutokana na mfumo huo mpya ambao umebuniwa ili kusaidia kurahisisha kazi zao za kila siku.

Alisema mfumo huo ambao umetengenezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ambao ni wasimaizi wakuu ni mfumo wa malipo ya serikali kielektroniki ambao unalenga kuongeza udhibiti katika usimaizi wa ukusanyaji wa mapato serikalini.

Aidha, alisema mfumo wa e-Vibali unatumiwa na taasisi 389 katika kuomba na kupata vibali vya kusafiri nje ya nchi kwa safari za kikazi na binafsi kwa watumishi wa umma, na kuongeza kuna mfumo wa ukusanyaji taarifa za miradi ya TEHAMA serikalini ambao unatumiwa na taasisi takribani 77.





Wachuuzi wakiwa wametandaza bidhaa zao hadi katika Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala Sokoni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa magari na waenda kwa miguu. **PICHA: JOHN BADI**

# Wenye matatizo ya mishipa ya hisia waitwa matibabu ya bure

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka China, imewataka wananchi kwenda hospitali ya Mnazi Mmoja kupata huduma muhimu za matibabu ya maradhi ya mkojo na matatizo ya mishipa ya hisia bila ya malipo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi mafunzo na utafiti wizara hiyo, Mwinyi Mselem, alisema huduma za maradhi hayo zinatolewa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na hakuna haja ya kufuatilia matibabu nje ya nchi.

Alisema timu ya madaktari bingwa kutoka China wamefanikiwa kutoa huduma za matibabu ya maradhi ya mkojo, uvimbe mkubwa na matatizo ya mishipa ya hisia (kiharusi) na wagonjwa hao wanaendelea vizuri.

"Kulikuwa na mgonjwa ana saratani na tatizo la haja kubwa madaktari wa kichina walimfanyia upasuaji na kuondoa tatizo, pia kwa kutumia njia ya adpancha wameweza kumtibu mgonjwa aliyekuwa hana hisia ambae hawezi kuzungumza na wakafanikiwa, na sasa anaendelea vizuri," alieleza mkurugenzi huyo.

Mkurugenzi Mwinyi aliwataka wananchi kuiamini Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja kwa vile huduma zake zimeboreshwa sana na wagonjwa ambao matatizo yao yameshindikana katika vituo vidogo vya afya kuitumia hospitali hiyo.

Naye kiongozi wa timu ya Madaktari hao, Dk. Zhang Zhen, alisema wamefanikiwa kufanya matibabu ya maradhi mbali mbali yaliyokuwa yakionekana hayawezi kutibika Zanzibar.

Alisema timu hiyo imeanzisha upasuaji kwa kutumia njia ya matundu kuondosha tatizo la tezi dume bila ya kupasua sehemu kubwa ambayo ni nzuri na rahisi katika kutoa huduma za maradhi ya aina hiyo.

Timu ya 28 ya madaktari kutoka China yenye madaktari 18 wataendelea kuwapo Zanzibar hadi mwezi Julai mwaka huu na wanatoa huduma katika Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee Mkoani na wanasaidia vituo vyengine vya afya Unguja na Pemba.

# Watendaji watakiwa kuratibu rasilimali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, wametakiwa kushughulikia na kuratibu maliasili zote ziliopo nchini ikiwamo uchimbaji wa mawe na kokoto kwa ajili ya kudhibiti mwenendo wa rasilimali hizo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, wakati akizungumza na watendaji wa Wizara hiyo pamoja na kutembelea mashimo ya uzalishaji wa mawe na kokoto.

Alisema imebainika hakuna usimamizi mzuri wa kazi za uchimbaji wa rasilimali ya mawe na kokoto katika machimbo yanayomilikiwa na Serikali.

Aidha, alisema hivi sasa baadhi ya machimbo yanayomilikiwa na Serikali yamechukuliwa kiholela na watu binafsi kwa kujimilikisha.

'"Tumebaini kwamba hakuna usimamizi mzuri wa uchimbaji wa rasilimali ya kokoto na mawe katika machimbo ya Serikali...yapo baadhi yanamilikiwa na watu binafsi kwa kujimilikisha'," alisema.

Mjawiri alipata nafasi ya kuyatembelea machimbo ya mawe na kokoto huko Kibele Wilaya ya Kati Unguja pamoja na Kitumba na kujionea uharibifu mkubwa wa rasilimali hiyo.

Nae Mkurugenzi wa Maliasili zisizorejesheka, Soud Mohamed, alisema machimbo ya rasilimali ya mawe na kokoto yameanza kuhakikiwa kwa ajili ya kuyatambua rasmi.

Alieleza kuwapo kwa tatizo la watu binafsi kujimilikisha machimbo ya rasilimali ya mawe na kokoto kinyume cha sheria na njia pekee ya kuepukana na tatizo hilo ni uhakiki.

"Mchakato wetu ni kufanya uhakiki wa machimbo yote yaliopo Unguja na Pemba na kuyatambua ili kuwapo mfumo na utaratibu unaofahamika kwa mujibu wa sheria'," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi, Mariyam Abdalla Juma, alisema kitendo cha wizara kushindwa kuyatambua machimbo hayo kwa kiasi kikubwa kumechangia kuwapo kwa uharibifu wa mazingira na Serikali kukosa mapato.

''Tunakosa mapato kutokana na kushindwa kuhakiki machimbo ya rasilimali ya mawe na kokoto, huku watu wengine wakijimilikisha kinyume cha sheria," alisema.

# AG atakiwa kurekebisha sheria 'mfu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, ameitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati ambazo baadhi yake hazifanyi kazi tena.

Suleiman alisema hayo wakati akiagana na wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali huko Mazizini kufuatia kutenganishwa kwa Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu, Ofisi ya Mwanasheria mkuu ilifanya kazi kubwa ya kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati.

Alizitaja sheria zilizofanyiwa marekebisho katika kipindi chake ni pamoja na sheria ya ushahidi ambayo ilikuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu.

"Mafanikio yangu makubwa katika kipindi cha miaka mitatu nilipokuwa Waziri wa katiba na sheria ni kufanyiwa marekebisho kwa sheria ya ushahidi ambapo sasa ushahidi wa mtoto unatambuliwa," alisema.

Aidha, aliyataja marekebisho mengine yaliyofanyika katika sheria ambazo zilionekana kikwazo katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ni sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ya mwaka 2017.

Alisema sheria hizo kwa kiasi kikubwa zimeleta mabadiliko makubwa na kudhibiti matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kutambuwa ushahidi unaotolewa na mtoto ambaye hajafikia umri wa miaka 18.

''Naipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kazi kubwa ya kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati ambazo ni kikwazo katika kutekeleza majukumu ya wananchi," alisema.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hassan Said Mzee, alisema wataendelea kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati ambazo hazina manufaa kwa jamii.

"Ofisi ya Mwanasheria mkuu moja ya vipaumbele vyetu ni kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati ambazo hazina tija kwa jamii," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Bakari Mshibe, alisema zipo sheria ambazo zinahitaji marekebisho makubwa zikiwa na lengo la kuleta mabadiliko ya sheria.

"Miongoni mwa kazi tunazotarajiwa kuzifanya ni kurekebisha sheria zilizopitwa na wakati na kutunga mpya ili kuleta mabadiliko makubwa ya wakati uliopo'," alisema.

# Makamu wa Rais Kenya aibiwa mayai shambani

**NAIROBI,** Kenya

WAFANYAKAZI wanne wamekamatwa kwa kutuhumiwa kuiba mayai yenye thamani ya dola za Marekani 25 kutoka shambani mwa Makamu wa Rais wa Kenya, William Ruto.

Taarifa kutoka Jeshi la Polisi ilieleza kuwa msimamizi wa shamba hilo lililopo eneo la Sugoi katika mkoa wa bonde la ufa alitoa taarifa kuwa kuna mayai yaliyopotea.

"Uchunguzi wetu wa awali umefichua kwamba wafanyakazi wanne wanaoishi ndani ya shamba hilo walihusika katika wizi huo lakini wote wamekana kuhusika na tukio hilo," alisema afisa wa polisi katika eneo hilo Zachariah Bittok.

**Washukiwa hao sasa watafikishwa mahakamani na trei hizo za mayai zilizopatikana zitatumika kama ithibati au ushahidi kortini.**

Imeelezwa kuwa washukiwa hao wanaume wawili na wanawake wawili wanashikiliwa katika kituo kimoja cha polisi katika eneo hilo ambako wanahojiwa.

Bitok ameliambia gazeti la The Standard kwamba msimamizi katika sehemu ya ufugaji kuku kwenye shamba hilo aligundua kwamba mayai yenye thamani ya Sh. 2,500 za Kenya yalipotea ndipo akaamua kutoa taarifa kituo cha polisi.

"Wafanyakazi wote wamekana kufahamu chochote kuhusu mayai hayo yaliopotea na meneja huyo akaanza kuyatafuta na kuwashutukia washukiwa hao wanne wakiwa wamezificha trei hizo kwenye sehemu moja ya shamba," alisema Bitok.

Taaifa hizo zimepokelewa kwa hisia tofauti Kenya huku baadhi wakikejeli na kusema kwamba kuna mambo yalio muhimu zaidi kuangaziwa katika vyombo vya habari kuliko taarifa za kupotea kwa trei 10 za mayai.

Baadhi ya wananchi walieleza kwamba kuna kila haki ya kuliripoti tukio hilo maana ni haki ya mtu huku baadhi wakipuuza na kulalamika kwamba ni kupoteza rasilimali nguvu za polisi.

Washukiwa hao sasa watafikishwa mahakamani na trei hizo za mayai zilizopatikana zitatumika kama ithibati au ushahidi kortini. **BBC**

## Sintofahamu yaibuka jeshi, waandamanaji

**KHARTOUM,** Sudan

WATAWALA wa kijeshi pamoja na viongozi wa waandamanaji Sudan wametofautiana kuhusu muundo wa baraza la pamoja, hali inayoashiria kuwa pande hizo mbili licha ya makubaliano waliyofikia mwishoni mwa juma bado wanatofautiana.

Mazungumzo yaliyofanyika mwanzoni mwa wiki kati ya wanajeshi na wawakilishi wa waandamanaji, yalifanyika baada ya Jumamosi iliyopita kukubaliana kuundwa kwa baraza la pamoja.

Baraza la kijeshi kupitia msemaji wake Luteni Jenerali Shamseddine Kabbashi, lilipendekeza kuundwa kwa baraza la watu10, ambapo wanajeshi watakuwa saba na raia watakuwa watatu, pendekezo ambalo limepingwa vikali na waandamanaji.

Awali viongozi wa waandamanaji hao walipendekeza baraza la watu 15 ambalo lingejumuisha raia nane na wanajeshi saba.

Licha ya mazungumzo ya hapo jana kumalizika bila muafaka, viongozi hao wamekubaliana kukutana tena huku kila upande ukiwa umefikiria mapendekezo ya kila mmoja. **RFI**



Aliyekuwa Rais wa Sudan, Omar al-Bashir.



Wafuasi wa Bobi Wine wakitawanywa na polisi katika eneo la Busabala nchini Uganda. Kwa sasa kiongozi huyo anashikiliwa gerezani na amenyimwa dhamana. **PICHA: AFP**

# Bobi wine anyimwa dhamana, arudishwa rumande

**KAMPALA,** Uganda

MBUNGE na mwanamuziki maarufu nchini Uganda, Robert Kyagulanyi, 'Bobi Wine,' amezuiliwa katika Gereza la Luzira, Jijini Kampala, baada ya kukamatwa na polisi Jumatatu, asubuhi.

Polisi walimkamata Bobi Wine akiwa safarini kuelekea makao makuu ya upelelezi jijini Kampala, alikotakiwa kuhojiwa kuhusiana na madai ya polisi ya kwamba alikuwa anachochea ghasia wakati wa maadimisho ya Pasaka.

Wine ameshitakiwa kwa kushiriki katika maandamano haramu mnamo mwaka jana ya kupinga kodi ya kutumia mitandao ya kijamii maarufu Uganda kama OTT.

Alionekana akitembea huku akiwa amefungwa pingu mikononi kabla ya kuingia ndani ya basi la magereza kuelekea katika gereza kuu la Luzira mjini Kampala. Hata hivyo, alionekana mwenye tabasamu akiwa ndani ya basi hilo lenye vizuizi vya chuma.

Wine aliwapungia mkono wafuasi wake waliokuwa wakiimba wimbo aliotunga wiki iliyopita akiwa ndani ya kizuizi cha polisi nyumbani kwake, wimbo aliowaimbia polisi, wenye ujumbe kwamba hapigani na polisi, ila anawapigania kuboresha maisha yao na familia zao.

Haya yanafanyika siku chache baada ya kuwa katika kifungo cha nyumbani.

Wine ameshitakiwa kwa kuandaa maandamano ya umma kinyume na sheria na alizuiwa siku ya Jumatatu katika kituo cha polisi cha Naggalama kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi.

Msemaji wa idara hiyo Fred Enanga alisema Wine aliongoza maandamano hayo mwaka jana pasipo kuomba ruhusa kutoka kwa polisi.

Kampeni mpya imeanzishwa katika mitandao ya kutaka Bobi Wine aachiliwe huru huku baadhi wakizungumzia hatua hiyo kama ya kutia wasiwasi.

Mashirika ya kutetea haki za binaadamu likiwamo la Marekani, Tom Lantos Human Rights Commission, na shirika linaloshinikiza uongozi wenye maadili na demokrasia kwa wote - Vanguard Africa, yameshutumu hatua hiyo ya serikali ya Uganda.

Katika ujumbe kwenye mtandao wa kijamii, mashirika hayo yametaka serikali iheshimu uhuru wa kujieleza na kushinikiza kuachiwa kwa mwanasiasa huyo wa upinzani.

Aliyekuwa Waziri Mkuu wa New Zealand, Helen Clark amejiunga katika kutoa ujumbe huo wa kutaka Bobi Wine aachiwe kwa kuitisha mshikamano wa kitaifa katika kulinda maisha na afya ya mwanasiasa huyo wa Uganda.

Bobi Wine aliwekwa katika kizuizi cha nyumbani katika kile ambacho polisi walisema ilikwa ni hatua ya kumzuwia mwanasiasa huyo wa upinzani kufanya mikutano iliyo kinyume cha sheria.

"Hizo zilikuwa ni hatua zilizochukuliwa chini ya sera ya kuzuwia ili kulinda sheria na utulivu wa umma. Wakati bado anatishia kufanya mikutano kinyume cha sheria, maafisa wetu wa ujasusi watatusaidia kumpata na tutaweza kuona ni nini kitakachofuatia," alisema Enanga na kuongeza.

"Hata hivyo hadi sasa tutaendelea pale majeshi yetu kwa sababu hili limekuwa ni suala la usalama wa taifa"

Wine alikuwa ametangaza mpango wa kufanya maandamano ya umma kote nchini kupinga hatua ya polisi kuendelea kuweka vikwazo dhidi ya matamasha yake ya muziki na ukatili dhidi ya wanasiasa wa upinzani.**BBC**



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Kiluwa Group, Mohamed Kiluwa (kushoto) na Rais wa Kamisheni ya Uchumi na Biashara kati ya China na Afrika, Huan Zhaojin, wakitia saini ya makubaliano ya ushirikiano na uwakilishi jijini Beijing mwishoni mwa wiki, ambapo kampuni hiyo, itajenga maeneo maalum ya viwanda za katika nchi nane za Afrika. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ongezeko la wajane Dar 80% kwa miaka 17

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema mkoa huo una ongezeko la asilimia 80 ya wajane katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2019.

Makonda aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na watendaji wote wa mkoa huo na kusema kuwa takwimu hizo zimetokana na mkutano wake aliofanya na wajane Aprili 4, mwaka huu.

Makonda alisema takwimu hizo ni kwa mujibu wa ripoti inayoandaliwa na wataalamu wakiwamo wanasheria waliowaajiri na kuzungumza na wajane hao katika mkutano uliowakutanisha wajane wote wa mkoa huo.

"Kwa sasa ripoti bado haijatoka inaendelea kuandaliwa, isipokuwa takwimu nilizopewa kuna ongezeko la asilimia 80 ya wajane wa mkoa huu katika kipindi cha miaka 19 hii inaonyesha kuwa wanaume wanakufa zaidi na kuacha wanawake wakiteseka na watoto," alisema Makonda.

Alieleza zaidi kuwa wamebaini pia kuna upungufu katika sheria ya mirathi ya mwaka 1892 ambayo atakutana na Waziri mwenye dhamana kwa ajili ya kuomba ifanyiwe marekebisho.

Alisema kutokana na sheria hiyo kuwa kandamizi wajane wengi wamekuwa wakidhulumiwa miradhi hali inayowafanya waishi katika mazingira magumu na kuacha watoto wakiteseka mitaani.

Makonda alisema awali alianzisha mkakati wa kuwakamata watoto ombaomba wa mitaani lakini kazi hiyo ilishindwa kufanikiwa kwa sababu ya sheria iliyopewa inayowataka kulipa faini ya Sh. 30,000 na kuachiwa huru.

"Ilibidi sasa nikutane na wajane ambao kwa asilimia kubwa watoto wao ndio wanakuwa wapo mitaani baada ya kupoteza baba zao na kudhulumiwa mirathi na ndugu, baada ya kukutana na wajane sasa tutawasilisha ripoti yetu ambao itakuwa na majibu ya nini kifanyike ikiwamo kuomba kubadilishwa kwa sheria ya mirathi," alisema Makonda.

# ...afichua kiini

INATOKA UK.2

haraka ili ujenzi uanze.

"Ninafahamu wapo watu wanaotakiwa kulipwa fidia, ninawaeleza ukweli wapo watakaolipwa na ambao hawatalipwa, wale waliondani ya mita 22.5 kila upande wa barabara hawastahili kulipwa, walio nje ya mita 22 watalipwa," alisema.

Alisema ujenzi wa kituo hicho umegusa mashamba na maeneo ya watu ambao wote watalipwa na ameagiza suala hilo lifanyike kuanzia mwezi ujao baada ya mikakati ya ulipaji wa Sh. bilioni 3 kupangwa. Aliwataka wakulima mbeya kuchangamkia fedha za mikopo inayotolewa na Benki ya Wakulima kwa sababu licha ya kuwa na kiwango kikubwa cha uzalishaji lakini takwimu zinaonyesha ukopaji wao haujafikia bilioni moja.

Kuhusu changamoto ya ukatikaji umeme maeneo hayo, Rais Magufuli amemuagiza waziri husika kulishughulikia mara moja.

"Suala la kukatika katika umeme huwa linaumiza sana unakuta unaangalia mpira kidogo unakatika na hapo ukute wakati unakatika goli ndiyo linakuwa linaingia," alisema.

Alisema suala la upatikanaji wa umeme wa kujitosheleza Tanzania litapigwa vita kwa sababu mabeberu hawapendi.

"Tunataka tuwe na umeme wa kutosha na tunajua tutapigwa vita tu mabeberu hawataupenda, kwa sababu ni umeme wa kujikomboa kiuchumi, ukiwa na umeme wa kutosha utakuwa na viwanda na utauuza," alisema na kuongeza:

"Wafanyabiashara kutoka Ulaya watakuja kuanzisha viwanda hapa kwa sababu gharama zipo chini, hawawezi wakafurahi wanataka mazao yetu tuwe tunayauza kama malighafi, ukiuza kama malighafi umeliwa, utalipwa fedha utakuwa mtumishi wao."

Rais Magufuli alisema unaposafirisha malighafi nje maana yake unatengeneza ajira kwao na bei ya soko watalipanga wao. Alitolea mfano zao la kokoa ambalo awali lilikuwa likiuzwa kwa kilo Sh. 800, lakini baada ya kuchachamaa bei imefikia Sh. 5,000.

Rais Magufuli aliwaagiza mawaziri wawili ambao ni wa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha eneo hilo la Kyela ambalo lina biashara nyingi linakuwa na viwanda.

Alisema fedha hizo zimetokana ya serikali kuwabana mafisadi na wala rushwa na kueleza kuwa wasingewabana wasingefanikiwa.

Katika hatua nyingine Rais Magufuli aliwaagiza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wajitahidi kushughulikia kero za wannachi badala ya kusubiri Rais aende. Pia alitoa siku 15 sakata la mtu mmoja wa ushirika wilayani humo ambaye inadaiwa aliandika Vyama vya Kuweka na Kukopa (Saccos) tofauti na matakwa ya sheria ili kujimilikisha, lifikishwe mahakamani.

Naye, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alisema serikali imetaifisha mali za umma ambapo hadi sasa zaidi ya nyumba saba zimetaifishwa na kushikilia zaidi ya Sh. bilioni 20 za benki mbalimbali

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
01/05/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe **01/05/2019** kampuni ya **SIMBA LOGISTICS EQUIPMENT LIMITED** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MTWARA kupitia NANGURUKURU.** Gari hizo zenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

1. **T232 DET/T 928 DEQ 2. T974 DNB/T110 DMU**
**3. T169 DNC/T106 DMU**
**4. T126DNC/T101DMU 5. T987DNB/T132DMU**
**6. T181DNC/T254DMW 7. T212CAJ/T560ANP**
**8. T908DGB/T788DKM 9. T945AWV/T470AAZ**
**10. T226DET/T306BPE 11. T731DLE/T448DGS**
**12. T240DNB/T941DGX 13. T827DPX/T507DPU**

**UREFU 22.0 UPANA 2.7 KIMO 4.6**

2. Gari hizo zitatoka DAR ES SALAAM kuelekea MTWARA kupitia NANGURUKURU. Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115207202

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
01/05/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 01/05/2019 kampuni ya **HIGHLAND ESTATE LIMITED** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **MWANZA** kuelekea **MTWARA kupitia DAR ES SALAAM**. Gari hizo zenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

**T 898 DBQ / T 718 AFU**
**UREFU 20.0 UPANA 2.88 KIMO 5.2**

2. Gari hilo litatoka MWANZA kuelekea MTWARA kupitia DAR ES SALAAM. Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi No. 92/2019**

Ombi la **IMELDA A. LUPOGO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **JOHN JACOB MIHAMBO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 07/05/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 11/04/2019

215204402

**NOTIC E OF DATE OF HEARING/ MENTION**
**(Rules 13(Civil procedure of Summons and Pleadings)**
**Rules. 1955 G: N......No.....**
**Cap: 2supp, 64**
**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**MATIRIMONIAL CASE NO.5 OF 2019**
**JANE RAPHAEL MSYALIHA APPLICANT**
**VERSUS**
**HERRY EDWARD SITIMA RESPONDENT**

**TO HERRY EDWARD SITIMA (0719624669) DODOMA**

Take notice that the mention of above case suit has been set down on 6/5/2019

You must produce on that day all the witness upon whose evidence and all document upon which you intend to sup [port of your case.

**Give under my hand and seal of the court this 25/5/2019.**

215204702

**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAM A**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya MWANZO DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi NA. 27/2019**

Ombi la **LEWIS LADISLAUS MSHANGA**
Msimamiliz wa mirathi ya marehemu **LADISLAUS MSHANGA**
Kwa yeyote anayehusika ...

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 13/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa

Tarehe 23/04/2019

215204102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA144 YA 2014**
**BAINA YA:**
**MUSTAFA JUMA TARANDU.............................................MUOMBAJI**
DHIDI YA
1. SHABANI ABDI
2. ABUSHEE ISSA JANKA
3. LEODGARD LEONARD SWAI
4. MCHINGA AUCTION MART AND REAL CO.LTD.

**KWA:- ABUSHEE ISSA JANKA NA MCHINGA AUCTION MART AND REAL CO. LTD**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA KUWA:** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo yanapatikana katika Baraza hili.

**KWA HIYO** unatakiwa/mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 8.05.2019 saa 3.00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kawa umepokea Hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri wa baraza hii leo tarehe 29 ya mwezi aprili,2019.

215204502

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF**
**AT ARUSHA**
**CIVIL/APPEAL/CASE NO 1 OF 2017**

**ZAITOON SADICK JAFFER...............PLAINTIFF/APPELLANT**
**VERSUS**
**PETER DAWSON SALEWA &ANOTHER........ DEFENDANT /RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING MENTION**

**TO : PETER DAWSON SALEWA**
**OF ARUSHA.**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 15th day of May 2019 at 08:30am O'clock in the forenoon.

You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produced on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FUTHER NOTICE** that in default of your appearance on that day time, before mention or hearing the Court may proceed in your absence.

Given under my hand the seal of the court this 5th day of December 2018

215204002

TANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI




**EMMANUEL PHILIBERT** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari Kom chenye Index No s-2652-0087 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2015

Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa polisi: MOS/RB/2709/19**

115205802

### CHETI KIMEPOTEA



**SUFIANI S. HASSANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0497-0041 kilichotolewa na TEMEKE YOUTH MUSLIM SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBT/RB/3209/19.**

115205702

### KUPOTEA KWA CHETI



**Aziza Ally Holaki** anatangaza kupotea kwa cheti cha Post Graduate Diploma in Accountancy (PGDA) kilichotolewa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) mwaka 1996. Na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba S. 311/13 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1979 katika Shule ya Sekondari Forodhani.

**Yoyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa BUG/RB/10303/99.**

115201202

### CHETI KIMEPOTEA




**GLORIA DOMINIC MUNISI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0236/0020** kilichotolewa na **KILIMANJARO ACADEMY SEKONDARI** mwaka 2008.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: MOS/RB/2646/19.**

115200602

### KUPOTEA KWA CHETI



**Claud Elia** Mwakalinga anatangaza kupotea kwa cha kidato cha nne chenye index namba **S0418/0115** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa katika Shule ya Sekondari Lutengano mwaka 1994.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chpochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: 4354/2019**

215199302

**FORM II**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: KARABAGAINE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 4/2019**

**Ombi la 1. DORISI RUKAMBA 2. MSHUMBU RUKAMBA 3. RAYMOND BYEHALILO 4. LONGINO H. KARUGABA. Usimamizi wa mirathi ya Marehemu EMANUEL RUKAMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 30/05/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 15/04/201

115206002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HEMED JUMA MRISHO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 862 DJW LAND CRUISER.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **OB/RB/8117/2019.**

115206602

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GAETAN FRANCIS MWIKEVE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 192 APE** AINA YA **TOYOTA STOUT** PICKUP RANGI NYEUPE. CHASSIS NAMBA **YK11OOOO4177** ENGINE **NAMBA 4YO227651.** YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MB/RB/47/2019.**

115207002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HEZRON K SANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 701 AJV** AINA YA **TOYOTA HILUX.** CHASSIS NAMBA **LN1060049320** ENGINE NAMBA 3L2525753. YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **MB/RB/3984/18.**

115206902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BUKOBA, KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 39 YA 2019**
**(JALADA ASILIA NO. 24/2018**

**RUTASINGWA JOHN..................MDAI**

**DHIDI YA**

**THEREZA STANISLAUS.........................MDAIWA**

**KWA: THEREZA STANISLAUS - (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na. 39/2019 imepangwa kutajwa tarehe 10.06.2019 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, E. Mogasa saa 2:00 asubuhi, mahali – Bukoba Mjini. Hivyo unaamriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 29.04.2019.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA

115205902

### KUPOTELEWA NA LISTI ZA KULIPIA KODI YA KIWANJA

**KOLONEL MABULA BENEDICTO**

Anatanagza kupotelewa na listi za kulipia kodi ya kiwanja kitaro L (HD) 79 za mwaka 2017 kilichopo Malunga kiwandani katika Wilaya ya kahama,hati ya mauziano ya kiwamnja kitaro L (HD) 79 na hati ya mauziano ya **Bw. Marco Bundala na Alex Donard Mageni**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo karibu yake

**Au piga simu namba;**
**0682-878-487**
**0743-177-040**

**Taarifa ya Polisi.**

**KAH/RB/1892/2018.**

215204602

### KUPOTELEWA NA KADI ZA TRAILER

**GODFREY KIZZA JACKSON** anatangaza kupotelewa na kadi za Trailer zenye namba za usajili **T. 625 DNU. T. 628 DNU. T. 636 DNU na T. 640 DNU.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/180/2019.**

115205602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
KINGOLWIRA

**Usimamizi wa mirathi No;14/2019**

Ombi la AMIRI SUDI AMIRI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu KASHINDE BORI NGOMA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe............./20.....

215203901

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Zuhura Rashid Mtwale** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T424 AUN** aina ya MITSUBISH-CANTER, yenye chasis namba FE538BD53D934, engine namba **4D35G63770.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**UD/TR/RB/3665/2019**

215204302

### KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**WU ZHOU INVESTMENT COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi pikipiki yenye namba za usajili **MC 542 BQA** model SANLG. Yenye chasis namba **LBRSPJB5H9004440** na Injini namba SL15FMI17903651.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi:
**MOR/TR/RB/379/2019.**

215204202


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DE GEA AICHOSHA UNITED, YAMTENGEA DAU OBLAK

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeripotiwa kuandaa euro milioni 120 zinazohitaji ili kuvunja mkataba wa Jan Oblak kufuatia mustabali wa baadaye wa David De Gea hapo Old Trafford kuwa shakani, kwa mujibu wa ESPN.

De Gea amekuwa katika kiwango kibovu kisichoeleweka kwa 'Mashetani Wekundu' hao, akifanya makosa ya wazi ikiwamo katika mechi dhidi ya Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Chelsea.

United imekuwa ikiweka kando kujadili mkataba mpya na kipa huyo wa kimataifa wa Hispania, huku ikielezwa ni mbali kabisa na suala la mshahara wake anaoutaka.

De Gea anataka kuwa kipa anayelipwa zaidi duniani kwa kulipwa pauni 300,000 kwa wiki, wakati klabu hiyo ikionekana kutokuwa tayari kumlipa kiasi hicho anachotaka.

Na uchezaji wake msimu huu unadaiwa unatokana na De Gea kutoridhika na hali hiyo, na ESPN sasa inaripoti kuwa Manchester United inamuwinda kipa wa Atletico Madrid, Oblak kama wazo lao la kumfanya kuwa mbadala.

Oblak kwa umri wake wa miaka 26 ni chaguo dogo kuliko Mhispania mwenzake mwenye umri wa miaka 28, na licha ya kusaini hivi karibuni mkataba mpya na klabu yake ana kifungu kinachomruhusu kuuvunja kwa euro milioni 120 baada ya hivi karibuni kuongezeka kwa euro milioni 20.

ESPN imeeleza kuwa Manchester United inaamini ada hiyo ni sahihi kwa kipa ambaye anachukuliwa kama mmoja wa makipa bora duniani.

Tetesi hizo zimedai kuwa De Gea ataruhusiwa kuondoka, na Juventus, Paris Saint-Germain na Real Madrid zimekuwa zikihusishwa naye.

# Davies asaini mkataba mpya hapo Everton

**LIVERPOOL,** England

KIUNGO wa Everton, Tom Davies amesaini mkataba mpya utakaomuweka hapo Goodison Park hadi mwaka 2023.

Mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 21, amekuwa na Toffees hao tangu akiwa na miaka 11, alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwa nahodha wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa 3-1 kwenye Kombe la Carabao dhidi ya Rotherham United Agosti mwaka jana.

Ameichezea mechi 19 kwenye mashindano yote msimu huu katika kikosi hicho cha kocha, Marco Silva.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ameonyesha kufurahishwa baada ya kusaini mkataba huo na amebainisha wazi kwamba kwa sasa akili yake ni kuichezea klabu hiyo kufikia kwenye mafanikio makubwa.

"Nimeamua kusaini mkataba mpya. Hicho ndio nilichokuwa nataka tangu nikiwa mdogo na nina furaha kubwa.

"Nahisi klabu ina imani na mimi na wameonyesha hilo kwa kunipa mkataba mpya. Naendelea vizuri na klabu na najihisi furaha kuendelea kucheza hapa na nina imani nitaimarika zaidi."





# *Suarez aitabiria makubwa Liverpool*

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez anaamini kwamba kuna majaliwa mazuri ya baadaye ya Liverpool, ingawa nyota huyo wa Barcelona hana mpango wa kuionea huruma klabu yake hiyo ya zamani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya leo Jumatano.

Barcelona na washindi hao wa pili msimu uliopita, watacheza kwenye mchezo wa nusu fainali na Suarez atacheza dhidi ya timu yake hiyo ya zamani kwenye dimba la Camp Nou.

Suarez alitumia miaka mitatu pale Liverpool, akishinda Kombe la EFL hapo Merseyside, kabla ya kujiunga na miamba hao wa La Liga, Barca mwaka 2014.

Chini ya Jurgen Klopp, Liverpool imekuwa tishio kubwa kwenye Ligi Kuu ya England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Liverpool imepitwa pointi moja na Manchester City huku mechi mbili zikiwa zimebaki kwenye Ligi Kuu na Suarez ameliambia Gazeti la Express: "Liverpool sasa ipo kwenye nafasi nzuri ambako majaliwa yake ya baadaye yanaonekana kuwa mazuri zaidi.

"Mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu ni nzuri na Liverpool na Manchester City yoyote anaweza kuwa bingwa."

Suarez akiwa hapo Barcelona ameshinda mataji manne ya La Liga na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# GUARDIOLA AJIAMINI MAN CITY ITAIFUNGA LEICESTER

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City itaifunga Leicester kuhakikisha wanabaki kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England siku ya mwisho wa msimu huu.

Guardiola amebainisha kwamba Man City itaifunga Leicester kwenye siku hiyo ya mwisho ya kumalizika kwa msimu wa Lgi Kuu baada ya ushindi dhidi ya Burnley kwenye Uwanja wa Renault Super Jumapili.

Kikosi hicho cha Guardiola kilirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kikiishusha Liverpool baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Burnley kwenye dimba la Turf Moor, kwa bao la Sergio Aguero.

Na bosi huyo wa City anahisi kwamba kikosi chake kilikuwa na bahati kuweza kupata bao hilo na kurudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

Guardiola alisema: "Katika kipindi cha pili tulitawala mchezo na tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga tatu nne au tano.

"Tulikuwa na nafasi ya kupata penalti na tulikuwa na nafasi ya wazi ya kufunga, lakini tulikosa, ingawa baadaye tulipata bao lililoturudisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu."

Na sasa Guardiola ana uhakika kwamba kweye mchezo wake wa mwisho Jumatatu ijayo dhidi ya Leicester watapata ushindi ambao kwa uhakika mkubwa unaweza kuwatawaza kuwa mabingwa wa ligi hiyo msimu huu.

# Benitez aionya Liver isitarajie mteremko

**LONDON,** England

RAFAEL Benitez ameionya klabu yake ya zamani Liverpool kutotarajia huruma wakati watakapokutana kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England na Newcastle United.

Huku mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo zikielekea mwisho, kikosi hicho cha Jurgen Klopp kipo nafasi ya pili na kitavaana na Newcastle Jumamosi kikijaribu kurudi kileleni mwa msimamo.

Lakini Benitez, ambaye aliiongoza Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA katika kipindi chake cha miaka sita, alisema kikosi chake hakina mpango wa kuisaidia klabu yake hiyo ya zamani.

"Tutafanya kile tunachotakiwa kufanya na kujaribu kushinda mchezo," alisema Benitez wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo.


"Tutacheza nyumbani mbele ya mashabiki wetu na tutajaribu kucheza kwa ubora wetu. Tutakuwa kwenye ubora wetu.

"Unatakiwa kukumbuka kwamba timu zote zina mechi 38 na zinatakiwa kucheza kwa uwezo wetu.

"Ni majukumu yetu kuangalia kila mchezo uliopo mbele yetu na hatutakuwa na nafasi ya kuangalia nafasi ya timu nyingine zaidi ya sisi wenyewe tu."

Newcastle ipo nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu na imejiweka nafasi ya kubaki kwenye ligi hiyo msimu ujao.






# Pogba amjibu Keane

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, amemjibu nahodha wa zamani wa klabu hiyo, Roy Keane akidai kwamba "anaweza kusema atakacho."

Keane amemshutumu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa akimtaja yeye kuwa ni 'tatizo' ndani ya timu ya Man United.

Lakini Pogba, ambaye amefunga mabao 16 msimu huu na alitajwa kwenye kikosi cha mwaka cha msimu, amesema hana muda wa kukifikiria kile kinachozungumzwa na watu kwenye televisheni pamoja na maoni ya Keane.

"Hakuna tatizo," alisema akiiambia RMC baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Chelsea Jumapili.

"Wanalipwa kusema kitu mbele ya kamera. Mimi nimejikita zaidi kwa kile kinachotokea uwanjani.

"Wanaweza kusema chochote wanachotaka, wanalipwa kwa hilo. Mimi silipwi kwa kuzungumza. Nalipwa kwa ajili ya kuwa uwanjani kwa ajili ya kuipigania timu yangu. Hilo ndio pekee ninalolijua na ninalotakiwa kulifanya ninapokuwa uwanjani."

Baada ya kufungwa mabao 4-0 na Everton, Pogba alijitokeza hadharani kuomba msamaha akidai kwamba wachezaji hawakuitendea haki timu.

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA





# VAN DIJK: MESSI ATAKABIKA TU LEO

### Ni mchezaji bora duniani, lakini hatukabi mmoja dhidi ya mmoja, tunazuia wote pamoja...

**LIVERPOOL,** England

BEKI kisiki wa Liverpool, Virgil van Dijk, amesisitiza hahofii changamoto atakazozipata kwa kujaribu kumkaba Lionel Messi na Barcelona wakati wa mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya leo.

**Liverpool itashuhudiwa ikishuka katika Uwanja wa Camp Nou katika mechi ya mkondo wa kwanza wa michuano hiyo dhidi ya mabingwa hao wa La Liga.**

Messi ameisaidia Barca kutwaa ubingwa wa La Liga misimu miwili mfululizo- na hii ikiwa ni mara ya 10 kubeba 'ndoo' hiyo ya Ligi Kuu akiwa hapo Camp Nou - na sasa mabingwa hao wa Hispania wanatazama uwezekano wa kumaliza msimu na mataji matatu.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'], amefunga mabao 46 msimu huu, 10 kati ya hayo akifunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini Van Dijk hamhofii Messi.

"Nadhani ni mchezaji bora duniani," Van Dijk, ambaye wiki hii ametwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka England, PFA, alisema. "Lakini unaona namna gani tunacheza na namna tunavyozuia. "Hatuzuii mmoja dhidi ya mmoja, tunazuia wote pamoja na tunashambulia wote pamoja pia hivyo tutaona. Tutakuwa tayari.

"Hali ilivyo ni kwamba tupo nusu fainali dhidi ya Barcelona na tunakwenda kukabiliana na mchezaji bora duniani, lakini si yeye pekee, timu nzima ina ubora mkubwa.

"Tutajiandaa vizuri na pia tunayo timu nzuri hivyo tunaweza kushindana pale. Si kama tunakwenda pale kama likizo."

Wanafainali hao wa Ulaya msimu uliopita, Liverpool, wapo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu na Manchester City, mbio ambazo zinaonekana zitaamuliwa mwisho na Van Dijk aliongeza: "Ninaona tulicho nacho. Ninaona wachezaji tulionao, ninaona uongozi na kwa namna tunavyocheza soka, hivyo hakuna kikubwa cha kushangaza lakini bado tunapaswa kufanya hilo Jumatano [leo].

"Itakuwa ngumu kwa sababu Barcelona ni moja ya timu kubwa duniani, lakini lolote linaweza kutokea. Unahitaji kuwa tayari kwa matatizo na tutakuwa. Tutakwenda kujaribu kila kitu kufuzu fainali."

## ZISIKUPITE

### OBLAK APANDIWA DAU UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kutoa pauni milioni 104, zinazohitajika ili kuvunja mkataba wa kipa wa Atletico Madrid, Msloveni Jan Oblak, 26. ***(ESPN)***

### DE GEA ANUKIA PSG

PARIS St-Germain itatoa ofa ya pauni milioni 90 kwa kipa wa Manchester United, David de Gea, 28, anayejiandaa kulipwa pauni 450,000 kwa wiki na mabingwa hao wa Ufaransa. ***(Star)***

### VAN DIJK AMTAKA DE LIGT LIVER

JURGEN Klopp ameambiwa amlete Liverpool beki wa Ajax, Matthijs de Ligt na raia mwenzake anayeichezea miamba hiyo ya Anfield, Virgil van Dijk. ***(Express)***

### MADRID YAMFUATA ZIYECH

MSHAMBULIAJI Ajax na Morocco, Hakem Ziyech, anatakiwa na Real Madrid, wakati pia klabu kibao za Ulaya zikivutiwa na mshambuliaji Mbrazil David Neres. ***(Mail)***

### NDOMBELE AMULIKWA MADRID

REAL Madrid imefanya mazungumzo ya awali na Lyon kuhusu kumpata kiungo wao, Mfaransa Tanguy Ndombele, 22. ***(AS)***

### SOLSKJAER AMKOSOA MARTIAL

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekosoa mtazamo wa winga Mfaransa, Anthony Martial, wakati wa mechi dhidi ya Chelsea. ***(Mail)***

### FERDINAND KUPEWA KAZI UTD

BEKI wa zamani wa Manchester United na England, Rio Ferdinand, amekutana na Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Ed Woodward, kujadili kuhusu uwezekano wa kuwa mkurugenzi wa michezo Old Trafford. ***(Mail)***

### CAVANI ATAKA KUTUA EPL

CHELSEA na Manchester United zinamfuatilia mshambuliaji wa PSG na Uruguay, Edinson Cavani, ambaye anataka kutua Ligi Kuu England. ***(Calciomercato)***

### CHAMBERLAIN KUFUNGWA LIVER

LIVERPOOL inataka kumtunuku Alex Oxlade-Chamberlain mkataba mpya utakaomfanya kuitumikia klabu hiyo hadi 2023 - ikiwa ni siku chache tu tangu kiungo huyo aliporejea kutoka kuuguza majeraha. ***(Mirror)***

### DANILO AIVUTIA INTER

INTER Milan inaendelea kuzungumza na beki Mbrazil Danilo, 27, kuhusu kujiunga nao kwa pauni milioni 18 akitokea Manchester City. ***(Mail)***

### LINDELOF AWINDWA WOLVES

Wolves itamfuata beki wa Manchester United, Msweden Victor Lindelof, 24, baada ya kushindwa kukamilisha mchakato huo majira ya joto yaliyopita. ***(Teamtalk)***

### LIGT AJISHUSHA BEI SOKONI

BEKI wa Ajax, Mholanzi Matthijs de Ligt, 19, ametabiri hatagharimu kiasi kikubwa cha fedha sokoni kama mchezaji mwenza Frenkie de Jong, aliyenunuliwa na Barcelona kwa pauni milioni 65, wakati huu tetesi zikiendelea. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# Ndayiragije mguu ndani nje KMC FC

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

ZIKIWA zimebakia siku chake ili kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2018/19, Kocha Mkuu wa KMC FC, Mrundi Etienne Ndayiragije, amesema bado hajafanya uamuzi kuwa msimu ujao ataifundisha timu gani hapa nchini.

Ndayiragije ametajwa kuhusishwa kuhamia kwa mabingwa wa michuano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame, Azam FC.

Mrundi huyo alitajwa kuhusishwa na Azam FC baada ya matajiri hao wa Azam Complex jijini Dar es Salaam kutangaza kuachana na Mholanzi, Hans van der Pluijm, kutokana na kushindwa kuipa timu hiyo matokeo mazuri kama walivyotarajia.

Akizungumza na gazeti hili mapema wiki hii, Ndayiragije alisema mkataba wake na KMC FC unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu huu na bado hajaweka wazi kama atasaini mpya na klabu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Ndayiragije pia alikataa kuweka wazi kama amefanya mazungumzo ya awali na Azam FC na kueleza kwamba anauheshimu mkataba wake na waajiri wake wa sasa.

"Hapana, kama ni tetesi au ni maneno ya mjini yaache yabaki hivyo hivyo, mimi niko na KMC mpaka mwisho wa msimu, mkataba wangu utakapomalizika ndipo nitaanza mazungumzo na klabu yoyote itakayonihitaji, kwa sasa fahamu ni mtumishi wa KMC FC," alisema kocha huyo.

Alisema anaendelea kuwanoa wachezaji wake waweze kufanya vema katika mechi zao tano za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobaka pamoja na mchezo wa hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la FA ambapo watakutana na Azam FC.

KMC FC ina pointi 42 baada ya kucheza mechi 33 na katika msimamo wa ligi iko katika nafasi ya saba wakati vinara ni Yanga yenye pointi 74 na African Lyon yenye pointi 22 wanaburuza mkia.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 33 | 24 | 5 | 4 | 52 | 23 | 77 |
| 2. Simba | 28 | 23 | 3 | 2 | 58 | 11 | 72 |
| 3. Azam | 33 | 19 | 9 | 5 | 49 | 20 | 66 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. KMC | 33 | 9 | 15 | 9 | 33 | 25 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 11. Singida Utd | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 33 | 9 | 12 | 12 | 28 | 35 | 39 |
| 13. JKT Tanzania | 33 | 9 | 12 | 12 | 20 | 28 | 39 |
| 14. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Alliance | 33 | 9 | 10 | 14 | 24 | 36 | 37 |
| 17. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara United | 32 | 8 | 10 | 14 | 22 | 31 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# MAGUFULI AMSHUKIA MWAKYEMBE VIPIGO SERENGETI BOYS AFCON U-17

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli, ameeleza namna alivyokereka na kuumia baada ya timu ya Taifa ya Vijana ya Tanzania chini ya miaka 17, 'Serengeti Boys' kufungwa mechi zake zote ikiwa uwanja wa nyumbani kwenye michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon U-17).

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika wilayani Kyela, Mbeya jana, Rais Magufuli alimweleza Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, kwamba hajui ataifutaje aibu hiyo kwa taifa lenye idadi ya watu milioni 55.

"Kwenye timu ya vijana Serengeti Boys, Waziri Mwakyembe umeniangusha hili nalisema kwa dhati yaani mpira uchezwe uwanja wako, timu yako alafu unatandikwa hapo hapo, mara mabao manne, ni nafuu ungechukua timu ya Kyela usingefungwa," alisema.

**Aliongeza: "Sijajua, labda kufungwa ni mchezo mzuri, ila katika vitu 'vinaniboa' ni timu zangu kufungwa huwa ninaumia, najisikia ovyo, mpo watu milioni 55 unafungwa na timu ambayo kwao kuna idadi ya watu milioni 10," alisema.**

Aidha, Rais Magufuli alimweleza waziri huyo kuwa aibu ya timu ya taifa kufungwa aibebe mwenyewe.

"Waziri hii aibu sijui utaifuta lini, unakuta nchi ina watu milioni 55, hapa maana yake tunaaibika wote, sifahamu hili litaliwekaje, sasa hivi tuna timu ya Taifa Stars inajiandaa [na michuano ya Afcon], sijui mchezo wa kwanza watafungwa?" alihoji.

Rais Magufuli alisema anatamani siku moja awe waziri wa michezo ili timu aipange mwenyewe.

Katika michuano ya Afcon U-17, ambayo Tanzania ilikuwa mwenyeji na kumalizika kwa Cameroon kuibuka mabingwa baada ya kuifunga Cuinea kwa mikwaju ya penalti 5-3 kufuatia sare tasa katika muda wa kawaida, Serengeti Boys ilimaliza mkiani baada ya kupoteza mechi zake zote za Kundi A lililokuwa likiundwa na Angola, Uganda na Nigeria iliyomaliza kileleni.

Serengeti Boys ilianza kwa kichapo cha mabao 5-4 dhidi ya Nigeria, kisha 3-0 na Uganda kabla ya kuhitimisha kwa kipigo cha mabao 4-2 kutoka kwa Angola.




Mmoja wa makocha wa Southampton, akiwanoa makocha wa Tanzania katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, wakufunzi hao wapo nchini chini ya udhamini wa SportPesa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Wakufunzi wa Southampton, SportPesa kunoa makocha 32*

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya makocha 32 wameanza mafunzo maalum ya ukocha yaliyoandaliwa na Kampuni ya Kubashiri Matokeo Michezoni ya SportPesa Tanzania chini ya wakufunzi kutoka klabu ya Southampton inayoshiriki Ligi Kuu ya England, EPL.

Mafunzo hayo yanafanyika chini ya wakufunzi, Andy Martino na Jason Holmes wa Klabu ya Southampton.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo, James Newbigin, amesema mafunzo hayo ni mwendelezo wa taaluma ya mpira wa miguu na makocha hao watajifunza mambo mbalimbali mapya ya mpira wa miguu yanayotokea hivi sasa.

Newbigin alisema mpira wa miguu una mambo mapya kila kukicha hivyo ni fursa pekee kwa makocha Watanzania kunoa ujuzi wao katika ufundishaji.

Alisema kusoma ni suala lingine na ufundishaji ni jukumu la makocha, hivyo kuwaomba makocha hao kusambaza elimu hiyo kwa makocha ambao hawajapata fursa hiyo na wachezaji.

"Ni somo kwetu sisi na makocha pia, kwani ujio wetu umetupa nafasi na kupanua wigo wa ufundishaji wa mpira. Naishukuru SportPesa kwa kutuongezea wigo wa kukutana na makocha wa Tanzania na jukumu lao ni kuona nchi inapata mafanikio zaidi," alisema Newbigin.

Alisema kuna maendeleo ya mchezo huo hapa nchini na hasa baada ya Timu ya Taifa, 'Taifa Stars' kufuzu fainali za Afcon 2019 zitakazofanyika nchini Misri na vile vile hatua ya nchi kuandaa fainali za Afcon U-17.

"Makocha nao wana viwango vizuri, kinachotakiwa sasa ni kujiendeleza na kufundisha ili kuleta matokeo chanya, kocha lazima awe na uchu wa kuleta matunda," alisema.

Mkurugenzi wa Utawala na udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema kuanza kwa kozi hiyo inathibitisha jinsi gani SportPesa Tanzania ilivyokuwa mdau wa kweli wa maendeleo ya mpira wa miguu nchini.

Tarimba alisema zoezi hilo ni endelevu kwani ujio wa timu ya Everton pia ulitoa fursa ya makocha na wachezaji chipukizi kujifunza na pia mchezaji wa zamani wa Everton, Steven Pienaar aliendesha mafunzo kwa wachezaji vijana.

Michezo

Jumatano Mei 1, 2019

Nipashe



Van Dijk: Messi atakabika tu leo HABARI UK.30

## HAWATOKI LEO...



Mshambuliaji Mohamed Salah (kulia) na beki wa kati, Virgil van Dijk, wakiwa mazoezini. Wachezaji hao watakuwa sehemu ya kikosi cha Liverpool kitakachoivaa Barcelona kwenye mechi ya nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya itakayopigwa Uwanja wa Camp Nou leo usiku. **HABARI UK. 30**

## Msolla kuisuka Yanga kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga ikitarajia kufanya uchaguzi mkuu Jumapili wiki hii, mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti, Dk. Mshindo Msolla amesema endapo atachaguliwa, atatumia uzoefu wake wa michezo wa miaka 40 kuifanya klabu hiyo kuwa ya kisasa kwa kuendeleza mchakato wa mabadiliko ya mfumo na uendeshaji kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 56 ya Katiba ya Yanga iliyorekebishwa ya mwaka 2010.

Kampeni za kuwania uongozi katika Klabu ya Yanga zilifunguliwa rasmi jana kabla ya uchaguzi kufanyika Jumapili ambapo wanachama wa klabu hiyo watapata fursa ya kuchagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

Akizungumza makao makuu ya Yanga jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni yake, Msolla alisema amedhamiria kuleta mabadiliko ndani ya Yanga ili kutatua changamoto mbalimbali ikiwamo sula la uongozi ambalo limekuwa likiathiri ufanisi wa klabu hiyo.

"Kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na changamoto ya kiuongozi na matokeo yake changamoto hiyo imefanya kuwe na ombwe la uongozi, nimeamua kugombea nafasi ya mwenyekiti wa klabu kwa sababu nina uzoefu wa kutosha hasa baada ya kuwa kwenye tasnia ya mpira kwa muda wa miaka 40 katika nyanja mbalimbali.

"Nitahakikisha ninajenga umoja ndani ya klabu kwa wanachama na wapenzi wa Yanga na kuirudisha timu kwa wananchi kwa kuimarisha matawi yaliyopo, kuanzisha matawi mapya, matawi kupelekewa katiba ili wawe na uelewa wa katiba ya klabu yao na kuendeleza mchakato wa maboresho ya mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji wa klabu.

# Simba rasmi kuivaa Sevilla

## SportPesa yawezesha, yatoa sababu kuitosa Yanga, Dilunga anogesha raha kwa kuichapa JKT...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Shirikisho la Soka nchini (TFF), limeichagua Simba kuivaa Sevilla Mei 23, mwaka huu katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyoandaliwa na Kampuni ya SportPesa itakayopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Mabingwa hao mara tano wa Uefa Europa League, Klabu ya Sevilla watakuwa nchini kwa ziara ya kimichezo ya siku tatu inayokwenda kwa jina la "La Liga World SportPesa Challenge" inayodhaminiwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa kwa ushirikiano wa karibu na La Liga.**

Katibu Mkuu wa TFF, Kidao Wilfred, akitangaza uamuzi huo jana, alisema kigezo kikubwa kilichotumika kuichagua timu ya kucheza mchezo huo, wametazama timu ya Tanzania iliyofanya vizuri katika mashindano ya SportPesa ambapo Simba ilifika hatua ya nusu fainali.

Alisema ratiba ya Ligi Kuu imebana, hivyo kimetumika kigezo cha mashindano ya SportPesa kumpata muwakilshi wa kucheza na Sevilla.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abas, awali alisema kulikuwa na wazo la kuzikutanisha Simba na Young Africans ili kupatikana timu moja itakayocheza na Sevilla, lakini ratiba imekuwa ngumu kuzikutanisha timu hizo au kuchezwa michezo miwili.

Ameongeza kuwa kigezo cha kutumia mashindano ya SportPesa kinaondoa ugumu wa kupatikana timu ya kucheza na Sevilla.

Sevilla ambayo itatua na kikosi chake kamili Mei 21, mwaka huu wakiwamo nyota kama Wissam Ben Yedder, Jesus Navas, Munir El Hadad, Quincy Promes na wengine wengi, kabla ya kuivaa Simba watashiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii pamoja na kuendesha kliniki za soka kwa wachezaji na wadau mbalimbali wa soka nchini.

### YAICHAPA JKT

Katika mechi yao ya jana, licha ya Simba kukosa mabao mengi kwenye mchezo huo, Emmanuel Okwi alifanya kazi kubwa ya kuwatoka walinzi wa JKT Tanzania na kutoa pasi kwa Hassan Dilunga aliyeujaza wavuni, akiipatia timu hiyo bao pekee katika dakika za majeruhi, baada ya mwamuzi Elly Sasi kuongeza dakika saba za nyongeza kutokana na wachezaji wa JKT Tanzania kupoteza muda mwingi kwenye mechi hiyo.

Mashabiki wa Simba waliokuwa wamenyong'onyea kwa muda mrefu, baadhi yao wakiwa wameshatoka uwanjani, walisubiri dakika ya sita kati ya saba za nyongeza kupata bao hilo lililoamsha hoi hoi na nderemo uwanjani hapo.

Ushindi huo wa bao 1-0, unaifanya timu hiyo kufikisha pointi 72 na kubakisha pointi tano tu kuifikia Yanga yenye alama 77 kileleni. Katika mechi hiyo iliyokuwa kali na ya kusisimua, Simba ilikosa mabao mengi, Okwi aliongoza kukosa mabao takriban matatu ya wazi, huku Meddie Kagere akikosa bao moja baada ya kugongesha mlingoti.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >